/ISSN 0856 – 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 10*** ***19th October, 2023***

***SPECIAL BILL SUPPLEMENT***

*To The Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 43 Vol. 104 Dated* ***19th October, 2023***
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

# SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Jina*

SURA YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Kanuni, maelekezo na notisi.
5. Maeneo ya uchaguzi.
6. Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine.
7. Maafisa waandikishaji.
8. Uteuzi wa waratibu wa uchaguzi.

SURA YA PILI
UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

SEHEMU YA KWANZA
SIFA NA KUKOSA SIFA ZA KUANDIKISHWA KUWA MPIGA KURA NA KUPIGA KURA

9. Sifa za kuandikishwa.
10. Kukosa sifa za kuandikishwa.
11. Daftari la Awali la Wapiga kura.
12. Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
13. Uandikishaji wa wapiga kura Tanzania Zanzibar.

14. Mahali pa kupigia kura na kukosa sifa za kupiga kura.
15. Kubadili jina.

SEHEMU YA PILI
UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

16. Muda wa uandikishaji.
17. Wakala wa uandikishaji.
18. Kadi ya mpiga kura.
19. Kubadili makazi.
20. Kupotea, kufutika au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura.
21. Marekebisho ya taarifa.
22. Tamko kuhusu kupotea au kuharibika kwa kadi ya mpiga ya kura.
23. Kukataliwa kwa maombi.

SEHEMU YA TATU
PINGAMIZI DHIDI YA UANDIKISHAJI AU KUENDELEA KUANDIKISHWA

24. Ukaguzi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura.
25. Kuingizwa kwa jina katika Daftari la Awali la Wapiga Kura.
26. Pingamizi.
27. Utaratibu wa kuweka pingamizi.
28. Uchunguzi na uamuzi wa afisa mwandikishaji.
29. Mweka pingamizi au mtu aliyewekewa pingamizi anaweza kukata rufaa.

SEHEMU YA NNE
RUFAA NA KUONGEZWA AU KUFUTWA KATIKA DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA

30. Rufaa kwenda Mahakama ya Wilaya.
31. Masharti yatokanayo na kuongezwa au kufutwa katika Daftari la Awali la Wapiga Kura.

SURA YA TATU
UCHAGUZI WA RAIS

SEHEMU YA KWANZA
UTEUZI WA WAGOMBEA WA KITI CHA RAIS NA MAKAMU WA RAIS

32. Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais.
33. Idadi ya wadhamini.
34. Uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais.
35. Dhamana.
36. Kukataa uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais.
37. Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais.
38. Mgombea pekee wa kiti cha Rais.
39. Kujitoa ugombea.
40. Kifo au kukosekana kwa wagombea.

SEHEMU YA PILI
TARATIBU ZA UCHAGUZI WA RAIS NA SIFA ZA MGOMBEA

41. Siku ya uchaguzi wa Rais.
42. Watu wanaostahili kupiga kura katika uchaguzi wa Rais.
43. Sifa za wagombea katika uchaguzi wa Rais.
44. Matumizi ya Sura ya Sita.
45. Majumuisho ya kura katika uchaguzi wa Rais.
46. Marudio ya upigaji kura.
47. Uchaguzi wa Rais kuchukuliwa kuwa uchaguzi wa Makamu wa Rais.

SURA YA NNE
UCHAGUZI WA WABUNGE

SEHEMU YA KWANZA
SIFA ZA MGOMBEA UBUNGE

48. Sifa za wagombea katika uchaguzi wa ubunge.

SEHEMU YA PILI
UTEUZI WA WAGOMBEA

49. Siku ya uteuzi.
50. Uteuzi wa wagombea ubunge.
51. Dhamana.
52. Mgombea kuteuliwa kwa jimbo moja tu.
53. Pingamizi na uamuzi kuhusu uhalali wa fomu ya uteuzi.
54. Mgombea pekee nafasi ya ubunge au kukosekana kwa mgombea.
55. Picha.

SURA YA TANO
UCHAGUZI WA MADIWANI

SEHEMU YA KWANZA
KUENDESHA UCHAGUZI NA MUDA WA KUWEPO MADARAKANI KWA MADIWANI

56. Uchaguzi wa madiwani.
57. Uchaguzi mdogo.
58. Uwakilishi katika kata na muda wa madiwani kuwa madarakani.

SEHEMU YA PILI
SIFA ZA WAGOMBEA UDIWANI

59. Sifa za mgombea katika uchaguzi wa udiwani.
60. Kukosa sifa ya uteuzi.

SEHEMU YA TATU
UTEUZI WA WAGOMBEA UDIWANI

61. Siku ya uteuzi.
62. Uteuzi wa mgombea.
63. Dhamana.
64. Mgombea kuteuliwa kwa nafasi moja tu.
65. Pingamizi na uamuzi kuhusu uhalali wa fomu ya uteuzi.
66. Mgombea pekee nafasi ya udiwani.
67. Picha.

SURA YA SITA
UCHAGUZI, UTARATIBU WA KUPIGA KURA NA UTEUZI WA WABUNGE NA MADIWANI WANAWAKE VITI MAALUM

SEHEMU YA KWANZA
SIKU YA UCHAGUZI

68. Wagombea walioteuliwa na siku ya uchaguzi.
69. Tangazo la uchaguzi.

SEHEMU YA PILI
KUJITOA, KIFO AU KUTOKUWEPO KWA WAGOMBEA

70. Kujitoa au kukoma kwa ugombea.
71. Kufariki kwa mgombea.
72. Kutokuwepo kwa wagombea.

SEHEMU YA TATU
KAMPENI ZA UCHAGUZI

73. Kampeni za uchaguzi.
74. Upatikanaji na wajibu wa vyombo vya habari vya umma.

SEHEMU YA NNE
UTARATIBU WA UCHAGUZI

75. Siku na muda wa kupiga kura.
76. Mpangilio wa chaguzi zinazoshindaniwa.
77. Mawakala wa upigaji kura.
78. Masanduku ya kura.
79. Muundo wa karatasi za kura.
80. Katazo la kuweka wazi kura.

SEHEMU YA TANO
UTARATIBU WA KUPIGA NA KUHESABU KURA

81. Watu wanaostahili kupiga kura.
82. Kupoteza sifa za kupiga kura.
83. Mahali pa kupigia kura.
84. Utaratibu wa kupiga kura.

85. Kuruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura.
86. Tuhuma za ukiukwaji wa taratibu.
87. Tamko la wapiga kura.
88. Kuahirishwa kwa upigaji kura wakati inapotokea vurugu.
89. Kufunga zoezi la upigaji kura.
90. Utaratibu wa kufunga upigaji kura.
91. Wakala wa upigaji kura kuwa wakala wa kuhesabu kura.
92. Mahali pa kuhesabia kura.
93. Kuhesabu kura.
94. Watu wanaoweza kuwepo wakati wa kuhesabu kura.
95. Taratibu za kuhesabu kura.
96. Karatasi ya kura ambayo haitahesabika kuwa halali.
97. Uthibitisho wa msimamizi wa uchaguzi.
98. Karatasi za kura zilizokataliwa.
99. Kufungana kwa kura na kurudia kuhesabu katika uchaguzi unaoshindaniwa.
100. Wagombea au mawakala wa kuhesabu kura wanaweza kuomba kurudia kuhesabu kura.
101. Uamuzi wa msimamizi wa kituo.
102. Wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura.
103. Majumuisho ya kura katika uchaguzi wa wabunge.
104. Majumuisho ya kura katika uchaguzi wa madiwani.
105. Kutangaza matokeo ya ubunge.
106. Kutangaza matokeo ya udiwani.
107. Utunzaji wa nyaraka.
108. Mamlaka ya wasimamizi wasaidizi wa vituo.
109. Mamlaka ya wagombea.
110. Kutokuwepo kwa mawakala hakutabatilisha mwenendo.
111. Chaguzi zilizofanyika kwa wakati mmoja.

SEHEMU YA SITA
UTEUZI WA WABUNGE NA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUM

112. Uteuzi wa wabunge wanawake wa viti maalum.
113. Uteuzi wa madiwani wanawake wa viti maalum.

SURA YA SABA
MAKOSA NA ADHABU

SEHEMU YA KWANZA
MAKOSA YANAYOHUSU UANDIKISHAJI NA UTEUZI

114. Makosa yanayohusu uandikishaji.
115. Kutumia wadhifa kushawishi watu wengine ili wasiombe kuteuliwa.
116. Mwenendo usiofaa wa mtendaji wa uchaguzi.
117. Kufidia hasara.
118. Tafsiri ya mtendaji wa uchaguzi.
119. Makosa yanayohusu Daftari na kadi ya mpiga kura.
120. Mwenendo usiofaa wa maafisa waandikishaji.
121. Makosa yanayohusu fomu ya uteuzi au karatasi za kura.
122. Matangazo ya uongo ya kujitoa.
123. Vishawishi vya rushwa kwa ajili ya kujitoa.

SEHEMU YA PILI
MAKOSA MENGINEYO YA UCHAGUZI

124. Makosa mengineyo.
125. Utunzaji siri katika chaguzi.
126. Adhabu ya hongo, takrima, n.k.
127. Adhabu ya kujifanya mtu mwingine.
128. Kupoteza sifa kwa kuhukumiwa kwa kosa la kitendo cha rushwa au kitendo haramu.
129. Watu wanaodaiwa kuwa na hatia ya ushawishi mbaya.
130. Hongo, rushwa na ushawishi mbaya kwa wajumbe na maafisa wa Tume.
131. Watu wanaochukuliwa kuwa na hatia ya kujifanya watu wengine.
132. Adhabu kwa watu wenye hatia ya vitendo vya rushwa na vitendo haramu.
133. Kuingilia mikutano halali ya hadhara kuwa ni kitendo haramu.
134. Katazo la kufanya mikutano siku ya uchaguzi na kuonesha nembo eneo la karibu na kituo cha kupigia kura siku ya uchaguzi.
135. Kuchafua matangazo.
136. Nyaraka kuwa na jina na anwani ya mpiga chapa na mchapishaji.

## SURA YA NANE
## KUPINGA MATOKEO YA UCHAGUZI KWA NJIA YA SHAURI LA UCHAGUZI

### SEHEMU YA KWANZA
### SHAURI LA UCHAGUZI KUPINGA MATOKEO YA UBUNGE

137. Kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya shauri la uchaguzi.
138. Makosa yanayotendwa na watendaji wa uchaguzi.

### SEHEMU YA PILI
### UTARATIBU NA MAMLAKA YA MAHAKAMA KUU

139. Mashauri yanayosikilizwa na Mahakama Kuu.
140. Shauri na taratibu za kuweka dhamana ya gharama.
141. Nafuu zinazoweza kuombwa.
142. Uthibitisho wa uhalali wa uchaguzi.
143. Taarifa ya Mahakama kuhusu vitendo vya rushwa au vitendo haramu.
144. Muda wa kuwasilisha na kuamuliwa kwa shauri la uchaguzi na rufaa.
145. Kura zinazoweza kuondolewa wakati wa uchunguzi.
146. Kanuni za Mahakama.

### SEHEMU YA TATU
### SHAURI LA UCHAGUZI KUPINGA MATOKEO YA UDIWANI

147. Kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya mashauri ya uchaguzi.
148. Kusamehewa kwa kutenda au kutokutenda matendo fulani.
149. Mashauri yanayosikilizwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi.
150. Mashauri na kuweka dhamana ya gharama.
151. Nafuu zinazoweza kuombwa.
152. Uthibitisho wa mahakama juu ya uhalali wa uchaguzi.
153. Muda wa kuwasilisha na kuamuliwa kwa shauri la uchaguzi.
154. Kura zinazoweza kuondolewa wakati wa uchunguzi.
155. Kanuni za mahakama.

SURA YA TISA
MASHARTI YA JUMLA

156. Maelezo yasiyo sahihi.
157. Mamlaka ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na wasimamizi wa uchaguzi kutaka taarifa.
158. Malipo ya watendaji.
159. Gharama kulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.
160. Utoaji wa taarifa.
161. Kanuni.
162. Kanuni za Maadili ya Uchaguzi.
163. Msamaha wa ushuru wa stempu
164. Maelekezo.
165. Kubadilishwa Daftari n.k
166. Matumizi ya teknolojia.

SURA YA KUMI
KUFUTA KWA SHERIA NA MASHARTI YA MWENDELEZO

167. Kufutwa kwa Sheria.
168. Masharti ya mwendelezo.

**NOTISI**

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni unachapishwa kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma pamoja na maelezo ya madhumuni na sababu zake.

Dodoma,
18 Oktoba, 2023

MOSES M. KUSILUKA,
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

***Muswada***
*wa*

**Sheria inayoweka masharti ya kusimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kufuta Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, 1979 na kuweka masharti mengine yanayohusiana nayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SURA YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023, na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atateua kwa notisi katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2**. Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, na kwa uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara.

Tafsiri

**3**.-(1) Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwandikishaji" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 7 na inajumuisha afisa

mwandikishaji msaidizi;

Sura ya 258

"chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa;

"Daftari" maana yake ni Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililoanzishwa chini ya kifungu cha 12;

"Daftari la Awali la Wapiga Kura" maana yake ni daftari lililoanzishwa chini ya kifungu cha 11;

"dhamana ya gharama" maana yake ni kiasi cha fedha kinacholipwa mahakamani na mlalamikaji kabla shauri lake halijapangwa kusikilizwa;

"Diwani" maana yake ni diwani aliyechaguliwa katika kata na inajumuisha madiwani wanawake wa viti maalum;

"elimu ya mpiga kura" maana yake ni usambazaji wa taarifa zinazohusiana na mchakato na taratibu za uchaguzi;

"eneo la uchaguzi" maana yake-

(a) kwa uchaguzi wa Mbunge, ni eneo au sehemu ya jimbo iliyogawanywa kwa mujibu wa kifungu cha 5(1), (2) na (3); na

(b) kwa uchaguzi wa Diwani, ni kata iliyotangazwa kwa mujibu wa kifungu cha 5(4);

"Halmashauri" maana yake-

(a) kuhusiana na wilaya, halmashauri ya wilaya;

(b) kuhusiana na jiji, halmashauri ya jiji;

(c) kuhusiana na manispaa, halmashauri ya manispaa;

(d) kuhusiana na mji, halmashauri ya mji;

Sura ya 287 na 288

iliyoanzishwa au kuchukuliwa kuanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"Jaji" maana yake ni Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu;

"jimbo" maana yake ni jimbo la uchaguzi kwa madhumuni ya uchaguzi wa Mbunge;

"kadi ya mpiga kura" maana yake ni kadi iliyotolewa chini ya masharti ya Sheria hii ikithibitisha kwamba mtu aliyetajwa katika kadi hiyo

ameandikishwa kuwa mpiga kura;

Sura ya 287 na 288

"kata" maana yake ni mgawanyo wa mamlaka katika mamlaka za serikali za mitaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

"kipindi cha kampeni" kuhusu uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, maana yake ni kipindi chote kuanzia mara baada ya siku ya uteuzi mpaka siku kabla ya siku ya uchaguzi;

"kituo cha kupigia kura" maana yake ni kituo kilichobainishwa chini ya masharti ya kifungu cha 69;

"kufunga upigaji kura" maana yake ni muda wa mwisho wa kupiga kura katika kituo cha kupigia kura kuhusiana na uchaguzi wowote;

Sura ya 287 na 288

"mamlaka ya serikali za mitaa" maana yake ni mamlaka ya Wilaya iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) au mamlaka ya Mji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"Mbunge" maana yake ni Mbunge wa jimbo na inajumuisha Wabunge wanawake wa viti maalumu;

"mgombea" maana yake ni mtu anayegombea katika uchaguzi wa Rais au Wabunge au Madiwani;

"Mgombea wa Urais" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na chama cha siasa kugombea kiti cha Rais;

"mjumbe" maana yake ni diwani aliyechaguliwa katika mamlaka ya serikali za mitaa na inajumuisha madiwani wanawake Viti Maalum;

"mkazi wa kawaida" maana yake ni mtu anayeishi kwa muda mrefu au mfupi katika eneo la uchaguzi kwa madhumuni ya makazi kama sehemu ya utaratibu wa kawaida wa maisha yake kwa wakati huo:

Isipokuwa kwamba-

(a) mtu hatahesabiwa kuwa mkazi wa kawaida

katika eneo la uchaguzi kwa sababu anamiliki au kuhodhi nyumba ya kuishi katika eneo hilo;

(b) mbunge wa jimbo hataacha kuwa mkazi wa kawaida katika jimbo husika, ikiwa sababu ya kutokuwepo kwake katika eneo la jimbo inahusiana na utekelezaji wa majukumu yake; na

(c) mtu ambaye ni mgonjwa katika taasisi yoyote inayotoa huduma ya matibabu kwa wagonjwa au ambaye amefungwa gerezani au yuko chini ya ulinzi mwengine kisheria mahali popote, hatachukuliwa kwa sababu hiyo kuwa mkazi wa kawaida katika eneo husika;

"Mkurugenzi wa Uchaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na itajumuisha mtu ambaye kwa kipindi hicho anatekeleza majukumu yoyote ya Mkurugenzi wa Uchaguzi;

"mpiga kura" maana yake ni mtu yeyote mwenye sifa za kupiga kura katika uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"msimamizi msaidizi wa kituo" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa msimamizi msaidizi wa kituo cha kupigia kura chini ya masharti ya kifungu cha 76(b);

"msimamizi wa kituo" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 76(c) kuwa msimamizi mkuu wa kituo cha kupigia kura;

"msimamizi wa uchaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 6 na inajumuisha msimamizi msaidizi wa uchaguzi;

"mtazamaji" maana yake ni mtazamaji wa ndani au wa kimataifa aliyesajiliwa na Tume;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na inajumuisha Makamu Mwenyekiti au mtu yeyote kwa wakati huo atakayekuwa anatekeleza majukumu ya Mwenyekiti;

"mtendaji wa uchaguzi" inajumuisha mratibu wa

uchaguzi wa mkoa, msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi, afisa uchaguzi, msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo, mratibu wa uandikishaji mkoa, afisa mwandikishaji, afisa mwandikishaji msaidizi, mwandishi msaidizi, mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki, karani mwongozaji na mtu mwingine yeyote atakayeteuliwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Tume;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani;

"sifa" au "kuwa na sifa" maana yake ni-

(a) inapotumika kuhusiana na mtu anayedai kuwa na sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, ana sifa zinazostahili au sifa za kuwa mpiga kura;

(b) inapotumika kwa mtu anayedai kuwa na sifa za kuwa mgombea wa uchaguzi wa kiti cha Rais, ana sifa au anastahili kuwa mgombea wa kiti cha Rais;

(c) inapotumika kuhusiana na mtu anayedai kuwa anastahili kuwa mgombea katika uchaguzi wa Mbunge, ana sifa au anastahili kuwa mgombea wa ubunge katika jimbo linalohusika;

(d) inapotumika kuhusiana na mtu anayedai kuwa anastahili kuwa mgombea katika uchaguzi wa diwani, ana sifa au anastahili kuwa mgombea wa uchaguzi katika uchaguzi wa diwani katika kata husika;

"siku ya uchaguzi" maana yake ni siku iliyopangwa chini ya kifungu cha 68 au siku yoyote mbadala wa siku hiyo kwa mujibu wa masharti ya kifungu hicho;

"siku ya uteuzi" maana yake ni siku iliyopangwa kuwa siku ya uteuzi wa wagombea;

"Tume" maana yake ni Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba;

"uchaguzi" maana yake-

(a) iwapo ni kumchagua Rais, ni uchaguzi wa Rais;

(b) iwapo ni kumchagua Mbunge, ni uchaguzi wa Mbunge na utajumuisha uchaguzi mdogo; na

(c) iwapo ni kumchagua Diwani, ni uchaguzi wa Diwani na inajumuisha uchaguzi mdogo;

"uchaguzi unaoshindaniwa" maana yake ni uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mbunge katika jimbo au Diwani katika kata ambapo kuna wagombea zaidi ya nafasi zilizo wazi;

"Uchaguzi wa Rais" maana yake ni uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;

"uteuzi" maana yake ni uteuzi wa wagombea kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na inajumuisha uteuzi wa wabunge na madiwani wanawake wa viti maalum;

"wakala wa kuhesabu kura" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa wakala wa kuhesabu kura chini ya masharti ya kifungu cha 91;

"wakala wa upigaji kura" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa wakala wa upigaji kura chini ya masharti ya kifungu cha 77;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uchaguzi.

Kanuni, maelekezo na notisi

**4**. Kanuni, maelekezo na notisi zote ambazo Tume ina mamlaka ya kuandaa au kutoa zitachukuliwa kuwa zimeandaliwa au zimetolewa kihalali endapo zitaandaliwa au zitatolewa zikiwa na saini ya Mwenyekiti wa Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi.

Maeneo ya uchaguzi

**5**.-(1) Tume itagawa kila jimbo katika maeneo ya uchaguzi na itachapisha notisi katika Gazeti la Serikali, itakayoainisha maeneo hayo ya uchaguzi.

(2) Endapo mipaka ya jimbo lolote itabadilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 74(6)(c) ya Katiba au kwa mazingira yoyote ambayo Tume itaona inafaa, Tume inaweza kubadili idadi na maeneo ya uchaguzi ndani ya jimbo na baada ya mabadiliko hayo, Tume itachapisha notisi katika Gazeti la Serikali itakayoainisha mabadiliko.

(3) Endapo kutokana na kuanzishwa kwa jimbo au mabadiliko katika mipaka ya jimbo, eneo ambalo lilikuwa ni eneo la uchaguzi katika jimbo moja lote lipo katika jimbo lingine, Tume inaweza kutangaza kuwa eneo hilo

litakoma kuwa eneo la uchaguzi katika jimbo lililotajwa awali na kuwa eneo la uchaguzi katika jimbo lililopo.

Sura ya 287 na 288

(4) Endapo Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ataanzisha kata kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) au Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), kata hiyo itakuwa ni kata kwa madhumuni ya uchaguzi wa madiwani chini ya Sheria hii.

Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine

**6.**-(1) Kwa madhumuni ya uchaguzi utakaofanyika chini ya Sheria hii, kila Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya atakuwa msimamizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata na msimamizi huyo wa uchaguzi anaweza kuwa msimamizi wa uchaguzi kwa jimbo zaidi ya moja.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kuteua kwa kuzingatia nafasi aliyonayo mtu katika ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa watumishi wa umma wenye sifa sawa na za Mkurugenzi aliyerejewa katika kifungu kidogo cha (1), idadi ya wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2), Tume inaweza, pale ambapo mazingira yatahitaji na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, kuteua mtu yeyote kutoka katika ofisi ya umma kwa jina au kwa nafasi yake kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi katika jimbo au kata yoyote badala ya yule aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (1) na (2), na iwapo mtu huyo anateuliwa, Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya au afisa, kwa kadri itakavyokuwa, atakoma kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi wa jimbo au kata hiyo katika uchaguzi huo.

(4) Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria hii, Tume inaweza kumteua mtu yeyote kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume yanayohusiana na

mchakato wa uchaguzi.

(5) Msimamizi wa uchaguzi, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 76 na maelekezo ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, anaweza kuteua watendaji kwa idadi inayohitajika kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata.

(6) Kila msimamizi wa uchaguzi na msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo, ataapa kiapo cha kutunza siri na kutoa tamko la kujitoa au kutokuwa mwanachama wa chama cha siasa, mbele ya Hakimu kwa kutumia fomu itakayoainishwa.

Maafisa waandikishaji

**7**.-(1) Kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura chini ya Sheria hii, kila Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji, na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya atakuwa ni afisa mwandikishaji kwa madhumuni ya kuandikisha wapiga kura katika jimbo au kata na anaweza kuwa afisa mwandikishaji wa jimbo zaidi ya moja.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kuteua mtu kwa kuzingatia nafasi aliyonayo katika ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa watumishi wa umma kuwa mratibu wa uandikishaji wa mkoa au afisa mwandikishaji msaidizi kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura kama itakavyoona inafaa.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), pale ambapo mazingira yanahitaji na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, Tume inaweza kuteua mtu yeyote kutoka katika ofisi ya umma kwa jina au kwa kuzingatia nafasi aliyonayo katika ofisi kuwa afisa mwandikishaji katika jimbo au kata yoyote badala ya yule aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (1) na endapo mtu huyo anateuliwa, Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji au Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya atakoma kuwa afisa mwandikishaji katika jimbo au kata husika.

(4) Afisa mwandikishaji, kwa kuzingatia maelekezo ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, anaweza kuteua idadi ya watendaji kama watakavyohitajika kwa

madhumuni ya kuandikisha wapiga kura katika jimbo au kata.

(5) Watendaji watakaoteuliwa na afisa mwandikishaji chini ya kifungu kidogo cha (4) wataapa kiapo cha kutunza siri na kutoa tamko la kujitoa au kutokuwa wanachama wa chama cha siasa, mbele ya afisa mwandikishaji kwa kutumia fomu itakayoainishwa.

(6) Kila mratibu wa uandikishaji wa mkoa, afisa mwandikishaji afisa mwandikishaji msaidizi kabla ya kuanza kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo, wataapa kiapo cha kutunza siri na kutoa tamko la kujitoa au kutokuwa wanachama wa chama cha siasa, mbele ya Hakimu kwa kutumia fomu itakayoainishwa.

(7) Afisa mwandikishaji atawajibika katika masuala yote yanayohusu uandikishaji wa wapiga kura katika eneo la mamlaka yake.

Uteuzi wa waratibu wa uchaguzi

**8**.-(1) Wakati wa uchaguzi, Tume inaweza kumteua mtu kwa kuzingatia nafasi aliyonayo katika ofisi au kwa jina kwa kila mkoa, kuwa mratibu wa uchaguzi wa mkoa kwa ajili ya kuratibu taarifa, upatikanaji wa vifaa, rasilimali na masuala mengine muhimu kwa ajili ya kuendesha uchaguzi kwa ufanisi katika majimbo ya uchaguzi na kata katika mkoa husika.

(2) Mtu yeyote mwenye wadhifa katika ofisi ya umma, atakapohitajika na Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi au mratibu wa uchaguzi wa mkoa, atasaidia au atatekeleza jukumu lingine lolote kama itakavyohitajika kwa madhumuni ya kuwezesha uendeshaji wa uchaguzi.

## SURA YA PILI
## UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

### SEHEMU YA KWANZA
### SIFA NA KUKOSA SIFA ZA KUANDIKISHWA KUWA MPIGA KURA NA KUPIGA KURA

Sifa za kuandikishwa

**9**.-(1) Mtu yeyote ambaye ni raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane na ambaye

hajapoteza sifa chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote, atastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), na kwa kuzingatia uthibitisho wa umri, Mtanzania yeyote ambaye hajapoteza sifa chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote, ambaye wakati au kabla ya tarehe ya uchaguzi atakuwa ametimiza umri wa miaka kumi na nane, atastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya Sheria hii.

Kukosa sifa za kuandikishwa

**10**.-(1) Mtu hatakuwa na sifa ya kuandikishwa au hataandikishwa kuwa mpiga kura chini ya Sheria hii ikiwa-

(a) yuko chini ya kiapo cha utii kwa nchi nyingine tofauti na Tanzania;

(b) katika sheria yoyote ile inayotumika Tanzania, imethibitika kuwa hana akili timamu au amewekwa kizuizini kama mhalifu mwenye ugonjwa wa akili au amewekwa kuzuizini kwa ridhaa ya Rais;

(c) ametiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo au anatumikia kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake inazidi miezi sita iliyotolewa na mahakama au kama ilivyobadilishwa na mamlaka yenye dhamana; au

(d) amepoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya masharti ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote inayotumika kuhusu makosa yanayohusiana na uchaguzi wowote.

(2) Kwa madhumuni ya aya (c) ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) adhabu mbili au zaidi zinazopaswa kutumikiwa kwa kufuatana zitachukuliwa kuwa ni adhabu tofauti iwapo hakuna adhabu moja kati ya hizo inayozidi miezi sita, na endapo mojawapo ya adhabu hizo inazidi miezi sita, zitahesabika kuwa ni adhabu moja; na

(b) hakuna kitakachozingatiwa kwa adhabu ya

kifungo iliyotolewa kama mbadala wa, au kwa ukiukwaji wa malipo ya faini.

(3) Endapo mtu yeyote aliyeandikishwa chini ya Sheria hii atapoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura jina lake litafutwa katika Daftari:

Isipokuwa kwamba, jina halitafutwa katika Daftari, ila kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya Tatu na Nne ya Sura hii au kwa taarifa ya mahakama kuwa mtu huyo ametiwa hatiani kwa vitendo vinavyomsababisha kupoteza sifa za kuandikishwa au kupiga kura.

(4) Mtu hataandikishwa kuwa mpiga kura katika jimbo au kata zaidi ya moja au katika eneo la uchaguzi zaidi ya moja katika jimbo au kata.

Daftari la Awali la Wapiga kura

**11**.-(1) Kwa madhumuni ya utayarishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Tume itaandaa Daftari la Awali la Wapiga Kura.

(2) Daftari la Awali la Wapiga Kura litatumika kwa ajili ya-

(a) uwekaji wazi ili kukaguliwa na umma;
(b) marekebisho yanayohusu kubadilika kwa makazi au taarifa nyingine zozote za mpiga kura;
(c) uwekaji pingamizi dhidi ya uandikishwaji wa mpiga kura yeyote;
(d) kuingiza au kufuta jina la mpiga kura katika Daftari; na
(e) kufanya masahihisho au marekebisho kama itakavyohitajika chini ya Sheria hii.

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

**12**.-(1) Kwa kuzingatia kifungu hiki na kwa madhumuni ya Sheria hii, kutakuwa na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Jamhuri ya Muungano ambalo litakuwa katika sehemu, sura au mgawanyo mwingine kama Tume itakavyoamua.

(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi ataweka, atatunza na kuboresha Daftari lililoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Daftari litakuwa na majina ya watu wote ambao wameandikishwa kuwa wapiga kura katika eneo la

uchaguzi.

(4) Daftari litaonesha bayana kwa kila mpiga kura aliyeandikishwa, namba ya kadi ya mpiga kura iliyotolewa, jinsi na anwani ya makazi ya kawaida ya mpiga kura na taarifa nyingine kama Tume itakavyoelekeza.

(5) Tume itasimamia utunzaji wa Daftari lililoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

(6) Mkurugenzi wa Uchaguzi anaweza kutoa maelekezo kwa afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi kuhusu masuala yanayohusu uandikishaji wa wapiga kura, yaliyomo katika Daftari au masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Uandikishaji wa wapiga kura Tanzania Zanzibar

**13**.-(1) Bila kujali masharti ya kifungu cha 12 na kwa madhumuni ya uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge kwa upande wa Tanzania Zanzibar, sheria inayohusu uandikishaji wa wapiga kura na daftari la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, pamoja na mabadiliko yatakayofaa, itakuwa ndiyo sheria ya uandikishaji wa wapiga kura na daftari la wapiga kura Tanzania Zanzibar kwa madhumuni ya Sheria hii.

(2) Tume itamwandikisha mtu yeyote aliyepo Tanzania Zanzibar ambaye anastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mahali pa kupigia kura na kukosa sifa za kupiga kura

**14**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, mtu aliyeandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo lolote la uchaguzi atastahili kupiga kura katika uchaguzi wowote katika eneo hilo la uchaguzi na mtu huyo atastahili kupiga kura katika kituo cha kupigia kura alichopangiwa katika eneo hilo la uchaguzi.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo chochote cha kupigia kura hatamruhusu mtu yeyote kupiga kura katika kituo hicho cha kupigia kura isipokuwa kama mtu huyo atamthibitishia msimamizi wa kituo au, kwa kadri itakavyokuwa, msimamizi msaidizi

wa kituo, kuwa yeye ndiye mpiga kura kama anavyodai kwa kuonesha kadi ya mpiga kura iliyotolewa kwake au uthibitisho mwingine wa utambulisho wake kama Mkurugenzi wa Uchaguzi atakavyoelekeza kwa wakati huo kuwa ni uthibitisho wa kutosha wa utambulisho wa mtu anayedai kuwa anastahili kupiga kura.

(3) Mtu aliyeandikishwa kuwa mpiga kura chini ya Sheria hii hatastahili kupiga kura katika uchaguzi wowote ikiwa mazingira yatajitokeza kuhusiana na mtu huyo ambayo, kama asingekuwa ameandikishwa, yangesababisha mtu huyo kupoteza sifa za kuandikishwa chini ya Sheria hii.

(4) Bila kujali masharti mengine ya Sheria hii, Mkurugenzi wa Uchaguzi au mtu yeyote aliyeidhinishwa kwa niaba yake anaweza, kwa hati aliyoisaini, kumuidhinisha mpiga kura aliyeandikishwa ambaye ni mgombea wa uchaguzi katika jimbo au kata, kupiga kura kwenye uchaguzi wa jimbo au kata hiyo katika kituo kilichoainishwa kwenye hati hiyo, iwe mgombea huyo ameandikishwa au hajaandikishwa kuwa mpiga kura kwenye kituo hicho cha kupigia kura.

(5) Bila kujali masharti mengine yoyote ya Sheria hii, endapo mpiga kura aliyeandikishwa katika eneo la uchaguzi ataajiriwa kuwa msimamizi wa uchaguzi, msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo, karani mwongozaji, mlinzi wa kituo au katika wadhifa mwingine wowote katika kituo cha kupigia kura katika eneo hilo la uchaguzi tofauti na kituo cha kupigia kura alichopangiwa, Mkurugenzi wa Uchaguzi au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi anaweza, kupitia hati aliyoisaini, kumuidhinisha mpiga kura huyo kupiga kura katika kituo kingine chochote cha kupigia kura katika eneo hilo la uchaguzi, na kituo hicho, kwa madhumuni ya Sheria hii, kitachukuliwa kuwa kituo cha kupigia kura alichopangiwa mpiga kura huyo.

(6) Mtu ambaye anatumikia adhabu ya kifungo anaweza, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kuandikishwa kuwa mpiga kura au kupiga kura katika uchaguzi iwapo tu ataruhusiwa kwa sheria inayosimamia

kifungo cha mtu huyo:

Isipokuwa kwamba, hakuna chochote katika kifungu hiki kidogo kitakachotafsiriwa kumuidhinisha mtu huyo kupiga kura katika kituo chochote tofauti na kituo alichopangiwa.

Kubadili jina

**15**. Mtu aliyeandikishwa kuwa mpiga kura ambaye jina lake limebadilika kutokana na ndoa au kwa sababu nyingine yoyote baada ya kuandikishwa, iwapo hajapoteza sifa za kupiga kura chini ya kifungu cha 14, atastahili kupiga kura kwa jina ambalo ameandikishwa.

## SEHEMU YA PILI
## UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

Muda wa uandikishaji

**16**.-(1) Tume itakuwa na jukumu la kupanga muda wa kuandikisha na kuboresha taarifa za wapiga kura katika kila eneo la uchaguzi ndani ya jimbo au kata.

(2) Mtu anayestahili kuandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo lolote la uchaguzi na ambaye hajaandikishwa, anaweza kwenda yeye mwenyewe katika eneo ambalo huduma ya uandikishaji inapatikana katika eneo la uchaguzi linalohusika.

(3) Bila kujali masharti mengine yoyote ya kifungu hiki yanayoelekeza vinginevyo, itakuwa halali kwa Tume kuelekeza kuwa uandikishaji wa wapiga kura katika maeneo yote au eneo lolote la uchaguzi katika jimbo au kata iliyoainishwa katika maelekezo hayo, usitishwe kwa kipindi ambacho Tume inaweza kuelekeza iwapo, kwa maoni ya Tume, itaona inafaa kusitisha uandikishaji wa wapiga kura.

(4) Endapo maelekezo chini ya kifungu kidogo cha (3) yametolewa kuhusiana na eneo lolote la uchaguzi, hakutakuwa na uandikishaji wa wapiga kura utakaofanyika katika eneo hilo la uchaguzi kwa kipindi kilichoainishwa katika maelekezo hayo.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, uboreshaji wa Daftari utakuwa mara mbili kati ya kipindi kinachoanza mara baada ya uchaguzi mkuu na kabla ya siku ya uteuzi.

Wakala wa uandikishaji

**17**.-(1) Chama cha siasa kinaweza kumteua mtu mmoja kuwa wakala wa uandikishaji kwa kila kituo cha uandikishaji katika jimbo au kata, kwa madhumuni ya-

(a) kuwatambua watu wenye sifa za kuandikishwa; na

(b) kumsaidia mwandishi msaidizi kutekeleza ipasavyo sheria na taratibu zinazohusu mwenendo wa uandikishaji wa wapiga kura bila kuingilia majukumu yake.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), kila chama cha siasa, kupitia taarifa ya maandishi, kitamtaarifu afisa mwandikishaji kuhusu uteuzi ndani ya muda wa siku saba kabla ya tarehe iliyopangwa kuanza uandikishaji wa wapiga kura au ndani ya kipindi kifupi kama Tume itakavyoruhusu.

(3) Taarifa itakayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) itaainisha jina la wakala aliyeteuliwa na jina na anwani ya kituo cha uandikishaji ambacho wakala huyo amepangiwa.

(4) Chama cha siasa kinaweza, katika taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2), kumteua wakala mbadala wa uandikishaji anayeweza kuwepo na kutekeleza ama kwa muda wa kudumu au muda mfupi majukumu yoyote ya wakala wa uandikishaji wakati ambapo wakala wa uandikishaji hayupo katika kituo cha uandikishaji.

(5) Endapo wakala wa uandikishaji atafariki au atashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, chama cha siasa kinachohusika kinaweza kumteua wakala mwingine wa uandikishaji badala yake, na mapema iwezekanavyo kitatoa taarifa ya maandishi kwa afisa mwandikishaji kuhusu jina na anwani ya wakala wa uandikishaji aliyeteuliwa na kituo cha uandikishaji ambacho amepangiwa.

(6) Mwandishi msaidizi, kwa kusaidiwa na kushirikiana na wakala wa uandikishaji, mapema iwezekanavyo atashughulikia malalamiko yatakayotolewa na mtu yeyote mwenye nia ya kuandikishwa mbele ya wakala katika kituo cha uandikishaji.

(7) Kila wakala wa uandikishaji na wakala mbadala wa uandikishaji kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake ataapa kiapo cha kutunza siri mbele ya afisa mwandikishaji.

Kadi ya mpiga kura

**18**.-(1) Endapo mtu ataomba kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 16, mtu huyo, kama atamthibitishia afisa mwandikishaji au afisa mwingine yeyote mwenye jukumu la kuandikisha wapiga kura kwa wakati huo kuwa ana sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo la uchaguzi lililo katika mamlaka ya afisa mwandikishaji au afisa mwingine, ataandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo hilo la uchaguzi na baada ya kuandikishwa atapewa kadi ya mpiga kura kwa namna itakavyoainishwa.

(2) Tume inaweza kumtaka mtu yeyote anayeomba kuandikishwa kuwa mpiga kura kujaza fomu kama itakavyoainishwa.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu hiki, Tume inaweza kuweka utaratibu wa kuwaandikisha wapiga kura walioandikishwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Kubadili makazi

**19**.-(1) Endapo mpiga kura aliyeandikishwa katika eneo moja la uchaguzi anakuwa mkazi wa kawaida katika eneo lingine la uchaguzi, mpiga kura huyo anaweza, kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 14, kuomba kwa afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura katika eneo la uchaguzi ambalo mtu huyo atakuwa mkazi wa kawaida, na afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura-

(a) baada ya kujiridhisha kuwa mwombaji-
  (i) ana sifa za kuandikishwa; na
  (ii) ni mkazi wa kawaida wa eneo la uchaguzi ambalo anafanya maombi; na

(b) baada ya mwombaji kurejesha kadi yake ya kupigia kura au baada ya mwombaji

kumthibitishia afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura kuwa kadi ya mpiga kura imepotea au imeharibika,

atamuandikisha mwombaji huyo katika fomu iliyoainishwa kwa ajili ya eneo la uchaguzi na kumpa kadi nyingine ya mpiga kura.

(2) Endapo afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura atamwandikisha mwombaji chini ya kifungu hiki, afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji huyo ataifuta mara moja kadi ya mpiga kura iliyorudishwa na mwombaji.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu cha 18(1) au kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, iwapo kwa sababu ya-

(a) mabadiliko yoyote ya jina la jimbo au kata;
(b) mabadiliko yoyote ya idadi ya majimbo au kata; au
(c) mabadiliko yoyote ya mipaka au maeneo ya jimbo au kata moja au zaidi, jimbo au kata ikawa sehemu ya jimbo au kata nyingine au eneo la uchaguzi la jimbo au kata moja ikawa eneo la uchaguzi au sehemu ya eneo la uchaguzi la jimbo au kata nyingine,

mabadiliko hayo hayatamlazimu mpiga kura ambaye jina lake liko katika Daftari lolote lililoathirika na mabadiliko hayo kuomba kuhamishwa jina lake katika Daftari linalostahili, isipokuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, mapema iwezekanavyo, atafanya marekebisho ya mabadiliko hayo kadri itakavyohitajika ili kuwezesha utekelezaji wa mabadiliko hayo kana kwamba maombi ya kuhamishwa yamefanywa na mpiga kura anayehusika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Kupotea, kufutika au kuharibika kwa

**20**.-(1) Endapo kadi ya mpiga kura iliyotolewa kwa mtu yeyote imepotea, imefutika au imeharibika, mtu

kadi ya mpiga kura

ambaye kadi hiyo ilitolewa kwake anaweza kuomba yeye mwenyewe kwa afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura kupewa kadi mpya ya mpiga kura.

(2) Baada ya maombi hayo kufanyika, afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura ikiwa atajiridhisha kuwa maombi yamefanywa ipasavyo na kwamba mwombaji bado ana sifa za kuandikishwa, atampa mwombaji kadi mpya ya mpiga kura baada ya mwombaji kulipa ada iliyoainishwa, ikiwa ipo, na iwapo maombi yatafanyika kutokana na kuharibika au kufutika kwa kadi ya mpiga kura, mwombaji atarudisha kadi hiyo iliyoharibika au iliyofutika.

Marekebisho ya taarifa

**21**.-(1) Endapo taarifa zozote zilizopo katika kadi ya mpiga kura au Daftari la Awali la Wapiga Kura zitahitaji kufanyiwa marekebisho kwa sababu ya kubadilika kwa jina au mabadiliko mengine yoyote katika mazingira ambayo yatamuathiri mtu ambaye kadi ya mpiga kura imetolewa kwake tofauti na mabadiliko ya makazi kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine, mtu ambaye kadi ya mpiga kura imetolewa kwake anaweza kuomba kadi mpya ya mpiga kura.

(2) Baada ya kupokea maombi na kujiridhisha kuwa maombi yamefanywa ipasavyo na kwamba mwombaji bado ana sifa ya kuandikishwa, afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura atamwandikisha mwombaji katika fomu itakayoainishwa na kumpa kadi nyingine ya mpiga kura:

Isipokuwa kwamba, kadi mpya ya mpiga kura haitatolewa chini ya kifungu hiki hadi mwombaji atakaporejesha kadi yake ya mpiga kura au atakapomthibitishia afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya

uandikishaji wa wapiga kura kuwa kadi hiyo imepotea au imeharibika na amelipa ada iliyoainishwa, ikiwa ipo.

Tamko kuhusu kupotea au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura

**22**. Endapo, chini ya masharti ya Sehemu hii, maombi yamefanywa kwa afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura na mtu ambaye anadai kuwa kadi iliyotolewa kwake imepotea au imeharibika, afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura atamtaka mwombaji kutoa tamko katika fomu iliyoainishwa kuhusu kupotea au kuharibika huko, na bila kuathiri mamlaka ya kukataa maombi hayo kwa sababu nyinginezo, afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura, anaweza kukataa maombi hayo isipokuwa kama mwombaji atatoa tamko hilo.

Kukataliwa kwa maombi

**23**.-(1) Endapo mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura atakataa maombi yaliyotolewa chini ya masharti ya Sehemu hii, pale mwombaji atakapohitaji, atatoa maelezo ya maandishi kwa mwombaji akiainisha sababu za kukataa maombi katika fomu iliyoainishwa, na endapo mwombaji hataridhika na kukataliwa huko anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio kwa afisa mwandikishaji ndani ya siku saba baada ya kupokea maelezo hayo.

(2) Endapo mwombaji hataridhika na uamuzi wa afisa mwandikishaji, anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Wilaya dhidi ya kukataliwa huko ndani ya siku kumi na nne baada ya kutolewa kwa uamuzi.

(3) Mahakama ya Wilaya itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya siku kumi na nne tangu siku rufaa ilipowasilishwa.

## SEHEMU YA TATU
## PINGAMIZI DHIDI YA UANDIKISHAJI AU KUENDELEA KUANDIKISHWA

Ukaguzi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura

**24**.-(1) Mtu yeyote anaweza kukagua Daftari la Awali la Wapiga Kura la eneo lolote la uchaguzi katika siku na muda kama afisa mwandikishaji atakavyoelekeza au kwa kadri itakavyoamuliwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi.

(2) Afisa mwandikishaji ataweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura katika kila kata na, ikilazimu, anaweza kufanya marekebisho kwa namna itakavyoelekezwa na Tume.

Kuingizwa kwa jina katika Daftari la Awali la Wapiga Kura

**25**.-(1) Endapo mtu yeyote aliyeandikishwa kuwa mpiga kura na ana kadi halali ya mpiga kura kuhusiana na eneo la uchaguzi, amebaini, kufuatia ukaguzi uliofanyika kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 24, kuwa jina lake halionekani katika Daftari la Awali la Wapiga Kura katika eneo la uchaguzi, mtu huyo anaweza kuomba kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, na Mkurugenzi wa Uchaguzi, au kama itakavyokuwa, afisa mwandikishaji, iwapo ataridhika kuwa jina la mtu huyo lilipaswa kuwemo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura katika eneo la uchaguzi, atafanya marekebisho au kusababisha kufanywa marekebisho katika Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa kuingiza jina la mtu huyo.

(2) Endapo Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa mwandikishaji atakataa kufanya marekebisho katika Daftari la Awali la Wapiga Kura ili kuingiza jina la mtu yeyote, mtu ambaye hataridhika na kukataliwa huko anaweza kupinga kukataliwa huko kwa mujibu wa vifungu vinavyofuata katika Sehemu hii.

Pingamizi

**26**.-(1) Mtu ambaye jina lake lipo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura la eneo lolote la uchaguzi anaweza kupinga kuendelea kuwemo kwa jina lake mwenyewe au jina la mtu mwingine yeyote katika Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa sababu yeye au mtu huyo mwingine hana sifa au amepoteza sifa za kuandikishwa au mtu huyo

mwingine amefariki.

(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa mwandikishaji anaweza kupinga kuendelea kuwemo kwa jina lolote katika Daftari la Awali la Wapiga Kura la eneo lolote la uchaguzi kwa sababu zozote zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1).

(3) Mtu anayeweka pingamizi chini ya kifungu hiki atajulikana kama "mweka pingamizi".

Utaratibu wa kuweka pingamizi

**27**.-(1) Isipokuwa pale ambapo pingamizi linawekwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa mwandikishaji, kila pingamizi litawekwa kwa kujaza nakala mbili za fomu iliyoainishwa na litawasilishwa kwa afisa mwandikishaji ndani ya muda ulioainishwa.

(2) Kila pingamizi, tofauti na pingamizi litakalowekwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa mwandikishaji, litawasilishwa likiambatishwa na malipo ya dhamana ya kiasi cha fedha kitakachoainishwa na Tume kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

(3) Afisa mwandikishaji, mapema iwezekanavyo baada ya kupokea pingamizi lililowekwa kwa mujibu wa Sehemu hii au kwa pingamizi alililoliweka mwenyewe katika kipindi hicho kama itakavyoelekezwa, atapeleka taarifa ya pingamizi hilo kwa mtu aliyewekewa pingamizi:

Isipokuwa kwamba, afisa mwandikishaji hatapaswa kupeleka taarifa endapo pingamizi limewekwa kwa sababu mtu ambaye jina lake limo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura amefariki.

Uchunguzi na uamuzi wa afisa mwandikishaji

**28**.-(1) Afisa mwandikishaji mapema iwezekanavyo atafanya uchunguzi wa wazi kuhusu mapingamizi yote yaliyowekwa ipasavyo, kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa muda usiopungua siku saba kuhusu tarehe, muda na mahali ambapo uchunguzi huo utaanza kwa kila mweka pingamizi na mtu ambaye amewekewa pingamizi, na kwa kila uchunguzi huo wa wazi kila mtu atakayeonekana na afisa mwandikishaji kuwa ana maslahi au ameathirika na uchunguzi huo wa

wazi anaweza kufika na kusikilizwa ama yeye mwenyewe au kupitia mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi na mtu ambaye ana maslahi au aliyeathirika.

(2) Endapo pingamizi limewekwa dhidi ya kuendelea kuwepo au kutokuwepo kwa jina lolote katika Daftari la Awali la Wapiga Kura, afisa mwandikishaji atamuita mweka pingamizi au mtu yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi na mweka pingamizi kwa ajili ya kutoa uthibitisho wa awali wa sababu za pingamizi.

(3) Endapo kwa maoni ya afisa mwandikishaji uthibitisho wa awali umetolewa, afisa mwandikishaji atahitaji uthibitisho wa sifa zilizopo za kuandikishwa kwa mtu aliyewekewa pingamizi na–

(a) ikiwa sifa za mtu huyo hazijathibitika kiasi cha kumridhisha afisa mwandikishaji, afisa mwandikishaji atamtaarifu Mkurugenzi wa Uchaguzi kuhusu hali hiyo na Mkurugenzi wa Uchaguzi atafuta au ataelekeza kufutwa kwa jina la mtu huyo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura; au

(b) ikiwa sifa za mtu huyo zitathibitishwa, afisa mwandikishaji atamtaarifu Mkurugenzi wa Uchaguzi kuhusu hali hiyo na Mkurugenzi wa Uchaguzi atabakiza, au kama itakavyokuwa, ataingiza au ataelekeza kubakizwa au kuingizwa jina la mtu huyo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura.

(4) Endapo katika tarehe iliyopangwa kwa ajili ya uchunguzi wa pingamizi lolote, mweka pingamizi au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba ya mweka pingamizi, atashindwa kuhudhuria au atahudhuria na kushindwa kutoa uthibitisho wa awali wa kumridhisha afisa mwandikishaji, afisa mwandikishaji atalibakiza au kuelekeza kubakizwa kwa jina la mtu huyo aliyewekewa pingamizi katika Daftari au, kama itakavyokuwa, hatachukua hatua ya kufanya marekebisho katika Daftari la Awali la Wapiga Kura ili kubakiza jina la mtu aliyewekewa pingamizi katika Daftari la Awali la Wapiga Kura.

(5) Endapo pingamizi lililowekwa na mtu

mwingine yeyote tofauti na afisa mwandikishaji au Mkurugenzi wa Uchaguzi linakataliwa na afisa mwandikishaji na kwa maoni yake, ataona pingamizi liliwekwa bila sababu za msingi, afisa mwandikishaji anaweza, kwa kadri atakavyoona inafaa, kuagiza kwa maandishi kuwa mweka pingamizi amlipe mtu aliyewekewa pingamizi fidia ya kiasi cha fedha kama Tume itakavyoainisha kwa notisi itakayotolewa katika Gazeti la Serikali.

(6) Kiasi chochote kitakachoagizwa kutolewa kama fidia chini ya kifungu hiki kitapatikana kama vile amri ya afisa mwandikishaji ni amri ya kukaza hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya kwa ajili ya urejeshaji wa fedha.

(7) Endapo pingamizi litakataliwa na afisa mwandikishaji na endapo kwa maoni yake ataona kuwa pingamizi liliwekwa bila sababu za msingi, malipo ya dhamana ya kiasi cha fedha kilichowekwa na mweka pingamizi kwa kadri Tume itakavyoainisha kwa notisi katika Gazeti la Serikali, itataifishwa kwa Serikali kwa amri ya afisa mwandikishaji, au ikiwa hakuna amri iliyotolewa, dhamana itarejeshwa.

(8) Uhalali wa mwenendo chini ya kifungu hiki hautahojiwa kwa sababu tu afisa mwandikishaji alisikiliza na kuamua pingamizi aliloweka yeye mwenyewe, na katika hali yoyote ile utaratibu katika uchunguzi wowote chini ya kifungu hiki utaanza katika hatua ambayo afisa mwandikishaji atakapohitaji uthibitisho wa sifa zilizopo za mtu ambaye pingamizi limewekwa dhidi yake.

(9) Afisa mwandikishaji atatoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa chini ya Sehemu hii ndani ya siku saba tangu siku ya mwisho ya kutolewa kwa notisi ya uchunguzi.

Mweka pingamizi au mtu aliyewekewa pingamizi anaweza kukata rufaa

**29**.-(1) Endapo mweka pingamizi au mtu aliyewekewa pingamizi hataridhika na uamuzi wa afisa mwandikishaji chini ya kifungu cha 28, mweka pingamizi au mtu huyo anaweza, ndani ya siku saba tangu tarehe ya uamuzi huo kutolewa, kukata rufaa katika Mahakama ya Wilaya.

(2) Mahakama ya Wilaya itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya siku kumi na nne tangu siku rufaa ilipowasilishwa.

## SEHEMU YA NNE
## RUFAA NA KUONGEZWA AU KUFUTWA KATIKA DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA

Rufaa kwenda Mahakama ya Wilaya

**30**.-(1) Kila rufaa chini ya kifungu cha 23 au 29 itaeleza kwa kifupi sababu za rufaa, na itaambatishwa na kiasi cha fedha ambacho Tume, kupitia notisi katika Gazeti la Serikali, itaainisha kiwe dhamana.

(2) Mahakama ya Wilaya itasikiliza kila rufaa katika sehemu ya wazi kwa kutoa taarifa ya muda, tarehe na mahali rufaa itakaposikilizwa kwa pande zinazohusika na itakuwa na hiari ya kusikiliza au kutosikiliza ushahidi wowote, na uamuzi wa rufaa itakaoutoa utakuwa ni wa mwisho na hautahojiwa na mahakama yoyote.

(3) Endapo Mahakama ya Wilaya itaamua rufaa ambayo imekatwa kuhusiana na Daftari la Awali la Wapiga Kura kuhusu kadi ya mpiga kura, itampa afisa mwandikishaji maelezo yaliyotiwa saini na hakimu yenye majina ambayo Mahakama imeamua yafutwe kutoka katika Daftari la Awali la Wapiga Kura au maelezo ya jina la mtu yeyote atakayepewa kadi ya mpiga kura, na afisa mwandikishaji atamtaarifu Mkurugenzi wa Uchaguzi kuhusu matokeo ya rufaa, na Mkurugenzi wa Uchaguzi atafanya marekebisho au ataelekeza kufanywa marekebisho katika Daftari la Awali la Wapiga Kura na kutoa kadi ya mpiga kura ipasavyo:

Isipokuwa kwamba-

(a) Mahakama ya Wilaya haitamtaka afisa mwandikishaji kutoa kadi nyingine ya mpiga kura pale ambapo kadi ya mpiga kura iliyotolewa awali imepotea au imeharibika, hadi pale mtu huyo atakapotoa tamko kwa afisa mwandikishaji kama inavyohitajika chini ya kifungu cha 22; na

(b) katika hali yoyote ile ambayo kifungu cha 19, 20 au 21 kinatumika na ikiwa hakuna tamko

lililotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 22, afisa mwandikishaji anaweza kukataa kuelekeza kutolewa kwa kadi nyingine ya mpiga kura mpaka kadi ya mpiga kura iliyotolewa awali kwa mhusika iwe imerejeshwa.

(4) Endapo rufaa imetupiliwa mbali, na Mahakama ya Wilaya ina maoni kuwa rufaa ilikatwa bila sababu za msingi inaweza kuamuru kuwa dhamana ya kiasi cha fedha ambacho Tume itaainisha kwa notisi katika Gazeti la Serikali, itaifishwe kwa Serikali au kama hakuna amri hiyo dhamana hiyo itarejeshwa.

(5) Wadaawa katika rufaa hawatastahili kulipwa gharama za kesi au fidia:

Isipokuwa kwamba, kama rufaa imekatwa na kukubaliwa na Mahakama ya Wilaya na endapo Mahakama itaona kuwa rufaa hiyo imekatwa bila sababu za msingi, Mahakama inaweza, kama itaona inafaa, kuamuru mrufani kulipa fidia ya kiasi cha fedha ambacho Tume itaainisha kwa notisi katika Gazeti la Serikali, na kiasi chochote kitakachoamriwa kitapatikana kana kwamba amri hiyo ni amri ya kukaza hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya kwa ajili ya urejeshwaji wa fedha.

(6) Endapo rufaa imekatwa chini ya kifungu hiki, Mahakama ya Wilaya, iwe ilikubali au kukataa rufaa, inaweza kuamuru kuwa dhamana yoyote iliyotaifishwa au itakayotaifishwa kwa Serikali au kiasi chochote cha fedha kilicholipwa au kitakacholipwa kama fidia kwa mujibu wa amri ya afisa mwandikishaji chini ya kifungu cha 28, au kiasi chochote cha dhamana au kiasi cha fedha ambacho Mahakama ya Wilaya inaweza kuainisha kisilipwe au kutaifishwa, au kurudishwa kwa mweka pingamizi, kadri itakavyokuwa, na kiasi chochote kitakachoamriwa kurudishwa kitarejeshwa kana kwamba amri hiyo ilikuwa ni amri ya kukaza hukumu ya Mahakama ya Wilaya kwa ajili ya urejeshwaji wa fedha.

(7) Shahidi anaweza kuitwa na kuapishwa wakati wa kusikiliza rufaa chini ya masharti ya kifungu hiki kwa utaratibu unaofanana kwa karibu na mazingira ya

uendeshaji wa kesi katika Mahakama ya Wilaya pale inapotekeleza mamlaka yake ya kuendesha kesi za jinai, na bila kuathiri masharti ya sheria nyingine yoyote, anaweza kuwajibishwa kwa adhabu sawa na inayotolewa kwa kutoa ushahidi wa uongo au kutohudhuria.

(8) Mtu anayestahili kuhudhuria kama mdaawa katika rufaa iliyowekwa chini ya masharti ya kifungu hiki anaweza kuhudhuria mwenyewe au kupitia wakili.

(9) Taratibu na mwenendo wa usikilizaji wa rufaa chini ya kifungu hiki zitakuwa kwa namna ambayo Mahakama ya Wilaya itaamua, na bila kuathiri ujumla wa masharti yaliyotangulia, Mahakama ya Wilaya, ikiwa itaridhika kuwa rufaa mbili au zaidi zinahusu hoja inayofanana, inaweza kutamka kuwa uamuzi iliyoutoa katika rufaa iliyosikilizwa awali itapaswa kuzingatiwa na wadaawa wa rufaa hiyo nyingine au rufaa hizo kwa kadri itakavyoelekeza.

Masharti yatokanayo na jina kuongezwa au kufutwa katika Daftari la Awali la Wapiga Kura

**31**.-(1) Endapo jina la mtu yeyote limeongezwa katika Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa mujibu wa kifungu cha 28, au kadi yoyote ya mpiga kura imetolewa kwa mtu yeyote kwa kuzingatia kifungu hicho, afisa mwandikishaji atachukua hatua kuhusu mtu huyo kana kwamba hakukataa maombi yanayohusika na rufaa hiyo.

(2) Endapo jina la mtu yeyote limefutwa kutoka katika Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa mujibu wa kifungu cha 28, afisa mwandikishaji atamtaka mtu huyo-

(a) kurejesha kadi yoyote ya mpiga kura ambayo imetolewa kwake chini ya Sheria hii; au

(b) kutoa na kuwasilisha tamko kwa afisa mwandikishaji kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 22,

ndani ya kipindi kisichopungua siku kumi, kama afisa mwandikishaji atakavyoelekeza, na afisa mwandikishaji ataelekeza kufutwa kwa kadi yoyote iliyorejeshwa.

## SURA YA TATU
## UCHAGUZI WA RAIS

### SEHEMU YA KWANZA

## UTEUZI WA WAGOMBEA WA KITI CHA RAIS NA MAKAMU WA RAIS

Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

**32**. Kila unapofanyika uchaguzi wa Rais, kila chama cha siasa kilichosajiliwa na kinachokusudia kushiriki katika uchaguzi wa Rais kitawasilisha kwa Tume jina la mgombea wa kiti cha Rais na jina la mgombea wa nafasi ya Makamu wa Rais wa chama hicho.

Idadi ya wadhamini

**33**.(1) Ili kuweza kuteuliwa kuwa mgombea halali wa kiti cha Rais, mtu anapaswa kudhaminiwa kwa maandishi na wadhamini walioandikishwa kuwa wapiga kura kwa madhumuni ya uchaguzi chini ya Sheria hii wasiopungua mia mbili kwa kila mkoa, angalau kwa mikoa kumi ya Jamhuri ya Muungano, kati ya hiyo angalau mikoa miwili kutoka Tanzania Zanzibar.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), wadhamini wa mgombea wa nafasi ya kiti cha Rais na nafasi ya Makamu wa Rais watathibitishwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo ambalo wadhamini husika wameandikishwa.

Uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais

**34**.-(1) Tume itatoa fomu za uteuzi kwa mgombea wa kiti cha Rais aliyependekezwa na chama cha siasa au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi na kwa idadi kadri itakavyoelekezwa na Tume.

(2) Kila mgombea wa kiti cha Rais atawasilisha fomu za uteuzi kwa utaratibu na mahali kadiri Tume itakavyoelekeza, si zaidi ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi.

(3) Fomu za uteuzi zitawasilishwa zikiwa na maelezo yafuatayo:

(a) jina na anwani ya mgombea wa kiti cha Rais na cha Makamu wa Rais ambaye atakuwa ni mgombea mwenza;

(b) tamko la mgombea kwamba yupo tayari na ana sifa za kuwa mgombea katika uchaguzi;

(c) kiapo cha mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano

kitakachojazwa na kusainiwa mbele ya Jaji;

(d) majina na anwani za wadhamini;

(e) namba za kadi za kupigia kura za wadhamini; na

(f) uthibitisho wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu wadhamini kutoka katika jimbo husika:

Isipokuwa kwamba, ikiwa Tume itaona kuna sababu za msingi za mgombea kushindwa kuwasilisha mwenyewe fomu za uteuzi, kiongozi wa chama kilichomteua anaweza kuwasilisha fomu hizo kwa niaba yake.

(4) Kila fomu ya uteuzi itaambatishwa na-

(a) idadi ya picha za mgombea kama Tume itakavyoelekeza, zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi; na

(b) taarifa yoyote binafsi inayomhusu mgombea kama itakavyohitajika kutolewa na kanuni katika fomu hiyo kama itakavyokuwa imeelekezwa.

(5) Endapo, kwa vyovyote vile fomu ya uteuzi haijaambatishwa na nyaraka zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (4), uteuzi wa mgombea utachukuliwa kuwa ni batili:

Isipokuwa kwamba, Tume, katika mazingira yoyote mahususi na kama itaona kuna sababu ya kufanya hivyo, inaweza kuelekeza kuwa fomu ya uteuzi ikubaliwe kuwa halali bila kujali kuwa fomu hiyo haikuambatishwa na nyaraka zozote ikiwa nyaraka zinazohusika zitawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ndani ya muda mwingine kama ambavyo Tume inaweza kuruhusu.

(6) Kwa madhumuni ya Sehemu hii, "siku ya uteuzi" maana yake ni siku iliyotangazwa na Tume kuwa siku ya mwisho ya kupokea majina ya watu wenye nia ya kugombea kiti cha Rais.

(7) Tume, mapema iwezekanavyo itabandika nakala ya fomu ya uteuzi katika sehemu ya wazi inayoonekana nje ya ofisi yake.

(8) Mtu hatamdhamini mgombea zaidi ya mmoja wa kiti cha Rais na iwapo msimamizi wa uchaguzi ametoa hati chini ya kifungu kidogo cha (3)(f) kwa ajili

ya udhamini wa mgombea mmoja, atakataa kutoa hati ya udhamini wa mtu huyo kwa mgombea mwingine katika uchaguzi mmoja:

Isipokuwa kwamba, mtu hatazuiwa kusaini fomu ya uteuzi kwa sababu tu amekwisha saini fomu ya mgombea aliyefariki au aliyejitoa kabla ya kuwasilisha fomu ya uteuzi ya mwanzo.

(9) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (8), iwapo mdhamini atamdhamini mgombea zaidi ya mmoja katika uchaguzi mmoja na hati zimetolewa chini ya kifungu kidogo cha (3)(f) kwa ajili ya uandikishwaji wa mtu huyo, udhamini wa wagombea wote wawili utakuwa ni halali.

(10) Mtu yeyote ambaye kwa kujua anamdhamini mgombea zaidi ya mmoja anatenda kosa, na akitiwa hatiani atalipa faini isiyozidi shilingi laki mbili.

(11) Endapo msimamizi wa uchaguzi ataridhika kuwa mtu yeyote ametenda kosa chini ya kifungu kidogo cha (10), kwa amri iliyotolewa kwa idhini yake anaweza kufifilisha kosa na kuamuru mtu huyo kulipa kiasi cha fedha:

Isipokuwa kwamba-

(a) kiasi cha fedha hakitazidi kiasi cha juu cha faini iliyowekwa kwa kosa hilo;
(b) mamlaka yaliyotolewa na kifungu hiki kidogo yatatumika kama mtu atakiri kwa maandishi kuwa ametenda kosa; na
(c) msimamizi wa uchaguzi atatoa stakabadhi ya malipo kwa mtu aliyetoa kiasi hicho cha fedha.

(12) Msimamizi wa uchaguzi, atakapoombwa na mgombea, au kwa niaba yake, kutoa hati kuhusu mdhamini aliyeandikishwa katika eneo la uchaguzi analohudumu, atatoa hati hiyo ipasavyo.

(13) Endapo baada ya siku ya uteuzi, jina la mtu aliyemdhamini mgombea litafutwa kutoka katika Daftari katika eneo la uchaguzi husika, hakutabatilisha udhamini wa mgombea.

Dhamana

**35**.-(1) Wakati wa kuwasilisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti mengine ya Sehemu hii, kila

mgombea wa kiti cha Rais ataweka dhamana katika ofisi ya Tume ya kiasi cha fedha kitakachoainishwa katika kanuni.

(2) Dhamana itakayowekwa na mgombea itataifishwa kwa Serikali ikiwa-

(a) mgombea wa kiti cha Rais atajitoa kugombea baada ya siku ya uteuzi; au

(b) idadi ya kura alizopata baada ya kuhesabiwa katika uchaguzi ni chini ya moja ya kumi ya kura zote halali zilizopigwa,

isipokuwa dhamana hiyo haitataifishwa kama mgombea atafariki kabla ya uchaguzi.

(3) Endapo dhamana iliyowekwa haitataifishwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (2), mapema iwezekanavyo baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa, dhamana hiyo itarejeshwe kwa mgombea wa kiti cha Rais au kulipwa kwa mwakilishi wake wa kisheria.

Kukataa uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais

**36**. Tume inaweza, katika siku ya uteuzi, kukataa kumteua mtu kuwa mgombea wa kiti cha Rais iwapo itajiridhisha kuwa mtu huyo ameondolewa sifa za kushiriki katika mchakato wa uteuzi na Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

Sura ya 278

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

**37**.-(1) Pingamizi linaweza kuwekwa dhidi ya fomu ya uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais kutokana na sababu zote au yoyote kati ya sababu zifuatazo:

(a) taarifa zilizotolewa kuhusu mgombea hazitoshelezi kumtambulisha;

(b) fomu ya uteuzi haikidhi au haikuwasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii;

(c) ni dhahiri kutokana na yaliyomo kwenye fomu ya uteuzi kwamba mgombea hana sifa za kugombea;

(d) masharti yaliyoainishwa katika kifungu cha 34(2) cha Sheria hii hayakutimizwa; na

Sura ya 278

(e) masharti ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi

hayakutimizwa.

(2) Pingamizi dhidi ya fomu ya uteuzi halitakubaliwa isipokuwa kama limewasilishwa Tume si zaidi ya saa kumi kamili alasiri ya siku inayofuatia siku ya uteuzi.

(3) Pingamizi linaweza kuwekwa na mgombea mwingine, Msajili wa Vyama vya Siasa au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, isipokuwa kwa pingamizi chini ya kifungu kidogo cha (1)(e) ambalo linaweza kuwekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa pekee, na litawekwa kwa maandishi na kusainiwa na mweka pingamizi na kubainisha sababu za pingamizi.

(4) Tume, kabla ya kuamua juu ya uhalali wa pingamizi lolote na bila kuchelewa-

(a) itamtaarifu mtu aliyewekewa pingamizi; na

(b) itampa mtu huyo nafasi ya kusikilizwa.

(5) Endapo Tume itatoa uamuzi kuhusiana na pingamizi lolote chini ya kifungu kidogo cha (3), itamjulisha kwa maandishi mgombea anayehusika kuhusu uamuzi na sababu za uamuzi huo.

(6) Uamuzi wa Tume chini ya kifungu hiki utakuwa ni wa mwisho na hautahojiwa na mahakama yoyote.

(7) Bila kujali masharti yoyote ya kifungu hiki, endapo Msajili wa Vyama vya Siasa ataweka pingamizi chini ya kifungu kidogo cha (3), pingamizi hilo litawasilishwa ndani ya siku kumi na nne baada ya siku ya uteuzi.

Mgombea pekee wa kiti cha Rais

**38**.-(1) Endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa kiti cha Rais aliyeteuliwa, Tume itamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee wa kiti cha Rais.

(2) Mgombea wa kiti cha Rais aliyetangazwa chini ya kifungu kidogo cha (1) atapigiwa kura ya ndio au hapana na atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa Rais endapo atapata kura nyingi zaidi ya kura zote halali zilizopigwa.

(3) Endapo mgombea pekee wa kiti cha Rais atashindwa kupata kura nyingi zaidi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), Tume itatangaza siku nyingine ya

uteuzi kwa ajili ya uchaguzi wa Rais kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Kujitoa ugombea

**39**.-(1) Mgombea wa kiti cha Rais anaweza kujitoa ugombea kwa kutoa taarifa ya maandishi aliyoisaini na kuiwasilisha yeye mwenyewe Tume na nakala kwa Katibu Mkuu wa chama kilichomdhamini kabla ya saa kumi kamili alasiri siku ya uteuzi.

(2) Kila taarifa ya kujitoa chini ya kifungu kidogo cha (1) itaambatishwa na tamko katika fomu itakayoainishwa, ambayo itajazwa na kusainiwa na mgombea mbele ya Jaji.

(3) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), endapo mgombea atajitoa kugombea baada ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi, chama chake hakitaruhusiwa kuweka mgombea mwingine mbadala na dhamana iliyotolewa na mgombea itataifishwa.

Kifo au kukosekana kwa wagombea

**40**.-(1) Endapo-

(a) baada ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi hakuna mgombea halali aliyeteuliwa, Tume, mapema iwezekanavyo kupitia notisi katika Gazeti la Serikali, itapanga siku nyingine ya uteuzi; au

(b) muda wowote baada ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi na kabla ya kumalizika kwa uchaguzi, mgombea yeyote wa kiti cha Rais au Makamu wa Rais atafariki, Tume, mapema iwezekanavyo kupitia notisi katika Gazeti la Serikali, itateua siku nyingine ya uteuzi si zaidi ya siku kumi na nne baada ya tarehe ya kifo ili kutoa muda kwa chama cha siasa kinachohusika kuteua mgombea mwingine wa kiti cha Rais au Makamu wa Rais, kadri itakavyokuwa.

(2) Endapo siku nyingine ya uteuzi itapangwa chini ya kifungu hiki, Tume itapanga siku nyingine ya uchaguzi wa Rais na taratibu husika zitaanza upya, isipokuwa kwamba hakutakuwa na uteuzi mpya utakaohitajika kwa wagombea wengine wa kiti cha Rais

kama wapo.

## SEHEMU YA PILI
## TARATIBU ZA UCHAGUZI WA URAIS NA SIFA ZA MGOMBEA

Siku ya uchaguzi wa Rais

**41**.-(1) Tume itapanga siku ambayo kwa mujibu wa Sheria hii itajulikana kama siku ya uchaguzi wa Rais, kwa ajili ya kupiga kura katika kila jimbo kwa ajili ya uchaguzi wa Rais.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, Tume inaweza kupanga siku tofauti za uchaguzi wa Rais katika majimbo tofauti na inaweza kutengua siku ya uchaguzi wa Rais na kupanga siku nyingine ya uchaguzi wa Rais.

(3) Tume itapanga siku ya uchaguzi wa Rais-

(a) ikiwa uchaguzi wa Rais unafanyika kwa sababu ya kuvunjwa kwa Bunge tofauti na mazingira yaliyoainishwa katika ibara ndogo ya (2)(b), (c), (d) au (e) ya ibara ya 38 ya Katiba-

(i) kwa kila jimbo ambalo kuna uchaguzi wa Wabunge, siku itakayopangwa kuwa siku ya uchaguzi wa Wabunge;

(ii) kwa kila jimbo lingine lolote, siku zisizopungua arobaini na zisizozidi hamsini baada ya siku ya uteuzi;

(b) ikiwa ni uchaguzi wa Rais ambao aya (a) ya kifungu kidogo hiki haitumiki, kwa kila jimbo, siku zisizopungua arobaini na zisizozidi hamsini baada ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais.

(4) Siku tofauti zinaweza kupangwa chini ya kifungu kidogo cha (3)(a)(ii) au (b) kwa majimbo tofauti.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3), jimbo ambalo uchaguzi wa Wabunge unaanza upya, litachukuliwa kuwa ni jimbo ambalo hakuna uchaguzi wa Wabunge.

Watu wanaostahili kupiga kura katika uchaguzi wa Rais

**42**.-(1) Kila mtu aliyeandikishwa kuwa mpiga kura chini ya Sheria hii atastahili kupiga kura katika uchaguzi wa Rais.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3), mpiga kura aliyeandikishwa anaweza kupiga kura-

(a) katika siku ya uchaguzi wa Rais iliyopangwa kwa ajili ya jimbo alilojiandikisha kuwa mpiga kura; na

(b) katika kituo cha kupigia kura alichopangiwa katika eneo la uchaguzi aliloandikishwa.

(3) Tume inaweza kutoa maelekezo na kuweka masharti ambayo mtu anaweza, katika siku ya uchaguzi wa Rais, kuruhusiwa kupiga kura katika kituo cha kupigia kura tofauti na kile alichopangiwa.

Sifa za mgombea katika uchaguzi wa Rais

**43**. Mtu hatakuwa na sifa ya kuwa mgombea wa uchaguzi wa Rais isipokuwa kama ana sifa za kuchaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 39 ya Katiba.

Matumizi ya Sura ya Sita

**44**. Kura ya uchaguzi wa Rais katika kila jimbo itapigwa kwa utaratibu kama ilivyo katika uchaguzi wa ubunge na masharti ya Sura ya Sita ya Sheria hii yatatumika kwa kuzingatia maboresho yatakayohitajika.

Majumuisho ya kura katika uchaguzi wa Rais

**45**.-(1) Watu wafuatao wataruhusiwa kuwepo katika kituo cha majumuisho ya kura-

(a) mjumbe wa Tume;

(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(c) Katibu Mkuu wa chama cha siasa au mwakilishi wake kwa barua;

(d) afisa wa Tume;

(e) mgombea;

(f) wakala wa kuhesabu kura;

(g) afisa wa polisi au mtu mwingine anayehusika na usalama wa mahali pa kuhesabia kura;

(h) mtazamaji wa uchaguzi aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume; au

(i) mtu mwingine atakayeruhusiwa na Tume.

(2) Baada ya taarifa zote za matokeo na masanduku ya kura yenye karatasi za kura kuhusu uchaguzi wa Rais kupokelewa kutoka katika vituo vya kupigia kura katika jimbo, msimamizi wa uchaguzi, baada ya kuamua uhalali wa kura zote zenye mgogoro, atajumlisha-

(a) kura zote zilizopigwa katika jimbo la uchaguzi;

(b) kura alizopigiwa kila mgombea; na

(c) kura zilizokataliwa.

(3) Msimamizi wa uchaguzi, baada ya kujumuisha matokeo ya kura za Rais katika jimbo, atabandika matokeo hayo katika sehemu ya wazi.

(4) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), msimamizi wa uchaguzi ataandaa na kuwasilisha kwa Tume, taarifa ya matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais katika jimbo.

(5) Msimamizi wa uchaguzi atathibitisha na kutoa nakala ya taarifa ya matokeo kwa kila wakala au wagombea wa kiti cha Rais, kama wapo.

(6) Tume inaweza kuelekeza kwamba, msimamizi wa uchaguzi, baada ya kuandaa taarifa ya matokeo chini ya kifungu kidogo cha (3), abandike nakala ya taarifa hiyo katika sehemu ya wazi inayoonekana.

(7) Endapo kuna shaka yoyote kuhusu usahihi katika kujumlisha kura za Rais katika jimbo lolote, Tume inaweza kuelekeza kurudiwa kujumlishwa kwa idadi ya kura za matokeo ya awali kutoka baadhi au vituo vyote vya kupigia kura katika jimbo.

(8) Baada ya kupokea matokeo yaliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (4), Tume itatangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais kwa jimbo husika.

(9) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), Tume, baada ya kujumlisha kura zote zilizowasilishwa na kila msimamizi wa uchaguzi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4), itatangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais ya nchi nzima.

(10) Mgombea yeyote wa kiti cha Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo amepata kura halali nyingi zaidi kuliko mgombea

mwingine yeyote.

Marudio ya upigaji kura

**46**.-(1) Endapo katika upigaji kura wa awali hakuna mgombea wa kiti cha Rais aliyepata kura nyingi zaidi kati ya kura halali zilizopigwa, Tume, kwa notisi katika Gazeti la Serikali, itapanga siku nyingine itakayofaa isiyozidi siku arobaini baada ya siku ya uchaguzi, kwa ajili ya marudio ya upigaji kura katika uchaguzi wa Rais.

(2) Endapo kutatokea kufungana kwa kura za wagombea waliopata kura nyingi zaidi, wagombea wa kiti cha Rais waliofungana ndio watakuwa wagombea pekee katika uchaguzi wa marudio.

Uchaguzi wa Rais kuchukuliwa kuwa uchaguzi wa Makamu wa Rais

**47**. Endapo mgombea wa kiti cha Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa, mgombea mwenza atachukuliwa kuwa amechaguliwa kuwa Makamu wa Rais.

## SURA YA NNE
## UCHAGUZI WA WABUNGE

### SEHEMU YA KWANZA
### SIFA ZA MGOMBEA UBUNGE

Sifa za wagombea katika uchaguzi wa ubunge

**48**. Mtu hatakuwa na sifa ya kuwa mgombea katika uchaguzi wa Ubunge au kuchaguliwa kuwa Mbunge isipokuwa kama atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 67 ya Katiba.

### SEHEMU YA PILI
### UTEUZI WA WAGOMBEA

Siku ya uteuzi

**49**.-(1) Endapo uchaguzi wa Wabunge utafanyika katika jimbo au ikiwa uchaguzi huo umesitishwa na taratibu za uchaguzi kutakiwa kuanza upya, Tume, kwa notisi katika Gazeti la Serikali, itapanga siku ya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge:

Isipokuwa kwamba-

(a) iwapo uchaguzi wa Wabunge utafanyika baada ya kuvunjwa kwa Bunge, siku ya uteuzi kwa jimbo lolote itakuwa si chini ya siku tano na si zaidi ya siku ishirini na tano baada ya kuvunjwa kwa Bunge;

(b) iwapo uchaguzi mdogo utafanyika, siku ya uteuzi itakuwa si chini ya siku ishirini na si zaidi ya siku hamsini baada ya kutokea kwa tukio ambalo ndiyo sababu ya uchaguzi kufanyika.

(2) Endapo Mbunge atajiuzulu, kufariki au vinginevyo ataachia ofisi kwa sababu nyingine tofauti na zilizo chini ya kifungu cha 142, Spika atamtaarifu kwa maandishi Mwenyekiti wa Tume, na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge.

(3) Tume inaweza kupanga siku tofauti za uteuzi kwa ajili ya majimbo tofauti, na inaweza kutengua siku yoyote ya uteuzi iliyopangwa na kupanga siku nyingine ya uteuzi:

Isipokuwa kwamba, siku hiyo nyingine iliyopangwa kuwa siku ya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi wa Ubunge itakuwa ndani ya kipindi kilichoainishwa chini ya kivuo cha kifungu kidogo cha (1).

(4) Tume itatoa taarifa ya siku ya uteuzi angalau siku saba, na iwapo uchaguzi wa Ubunge utafanyika pale ambapo Rais ametoa taarifa ya kusudio la kuvunja Bunge, taarifa ya siku ya uteuzi inaweza kutolewa kabla ya kuvunjwa kwa Bunge.

(5) Endapo uchaguzi mdogo unatakiwa kufanyika na tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge imetangazwa au imejulikana kwa mujibu wa matukio yaliyoainishwa katika Ibara ya 90(3) ya Katiba, uchaguzi mdogo hautafanyika katika muda wowote wakati wa kipindi cha miezi kumi na mbili mara tu baada ya tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge.

Uteuzi wa wagombea ubunge

**50**.-(1) Ili kuweza kuteuliwa kuwa mgombea halali wa uchaguzi wa Wabunge, mtu atapaswa

kudhaminiwa kwa maandishi na wadhamini wasiopungua ishirini na tano ambao ni wapiga kura walioandikishwa katika maeneo ya uchaguzi ndani ya jimbo ambalo mtu huyo ni mgombea.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza, katika siku ya uteuzi, kukataa kumteua mtu kuwa mgombea iwapo itajiridhisha kuwa mtu huyo ameondolewa sifa za kushiriki katika mchakato wa uteuzi na Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

Sura ya 278

(3) Uteuzi utafanyika kwa kutumia fomu itakayoainishwa ambayo itazingatia matumizi ya watu wenye mahitaji maalumu, itakayosainiwa na mgombea na wadhamini na itakuwa na taarifa zifuatazo:

(a) jina, anwani na kazi ya mgombea;
(b) majina na anwani za wadhamini na namba za kadi zao za kupigia kura;
(c) tamko la mgombea kwamba yupo tayari na ana sifa za kuwa mgombea katika uchaguzi;
(d) uthibitisho wa msimamizi wa uchaguzi katika jimbo ambalo wadhamini wameandikishwa; na
(e) kiapo cha mgombea kitakachojazwa na kusainiwa na mgombea mbele ya hakimu na kitakachoonesha sifa za mgombea na kuwa hajapoteza sifa kwa ajili ya uchaguzi.

(4) Kila fomu ya uteuzi itaambatishwa na-

(a) idadi ya picha za mgombea kama Tume itakavyoelekeza, zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi; na
(b) taarifa yoyote binafsi inayomhusu mgombea kama itakavyohitajika kutolewa na kanuni katika fomu hiyo kama itakavyokuwa imeelekezwa.

(5) Endapo, kwa vyovyote vile fomu ya uteuzi haijaambatishwa na nyaraka zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (4), uteuzi wa mgombea utachukuliwa kuwa ni batili:

Isipokuwa kwamba, Tume, katika mazingira maalumu na kama itaona kuna sababu ya kufanya hivyo,

inaweza kuelekeza kuwa fomu ya uteuzi ikubaliwe kuwa halali bila kujali kuwa fomu hiyo haikuambatishwa na nyaraka zozote ikiwa nyaraka zinazohusika zitawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi ndani ya muda mwingine kama ambavyo Tume inaweza kuruhusu.

(6) Msimamizi wa uchaguzi atatoa fomu za uteuzi kwa mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi na atampa idadi ya fomu za uteuzi kama itakavyoelekezwa na Tume.

(7) Kila mgombea atawasilisha fomu za uteuzi zilizosainiwa kama ilivyoainishwa chini ya kifungu hiki, katika ofisi ya msimamizi wa uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi:

Isipokuwa kwamba, ikiwa Tume itaona zipo sababu za msingi za mgombea mwenyewe kushindwa kuwasilisha fomu hizo, kiongozi wa chama kilichomdhamini anaweza kuwasilisha fomu hizo kwa niaba yake.

(8) Msimamizi wa uchaguzi, mapema iwezekanavyo atabandika nakala ya fomu ya uteuzi katika sehemu ya wazi inayoonekana nje ya ofisi yake.

(9) Mtu hatamdhamini mgombea zaidi ya mmoja kwa uchaguzi mmoja na iwapo msimamizi wa uchaguzi ametoa hati chini ya kifungu kidogo cha (3)(d) kwa ajili ya udhamini wa mgombea mmoja, atakataa kutoa hati ya udhamini wa mtu huyo kwa mgombea mwingine katika uchaguzi mmoja:

Isipokuwa kwamba, mtu hatazuiwa kusaini fomu ya uteuzi kwa sababu tu amekwisha saini fomu ya mgombea aliyefariki au aliyejitoa kabla ya kuwasilisha fomu ya uteuzi ya mwanzo.

(10) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (9), iwapo mdhamini atamdhamini mgombea zaidi ya mmoja katika uchaguzi mmoja na hati zimetolewa chini ya kifungu kidogo cha (3)(d) kwa ajili ya uandikishwaji wa mtu huyo, udhamini wa wagombea wote wawili utakuwa ni halali.

(11) Mtu yeyote atakayemdhamini mgombea zaidi ya mmoja anatenda kosa, na akitiwa hatiani atalipa faini

isiyozidi shilingi laki mbili.

(12) Endapo msimamizi wa uchaguzi ataridhika kuwa mtu yeyote ametenda kosa chini ya kifungu kidogo cha (11), kwa amri iliyotolewa kwa idhini yake anaweza kufifilisha kosa na kuamuru mtu huyo kulipa kiasi cha fedha:

Isipokuwa kwamba-

(a) kiasi cha fedha hakitazidi kiasi cha juu cha faini iliyowekwa kwa kosa hilo;

(b) mamlaka yaliyotolewa na kifungu hiki kidogo yatatumika kama mtu atakiri kwa maandishi kuwa ametenda kosa; na

(c) msimamizi wa uchaguzi atatoa stakabadhi ya malipo kwa mtu aliyetoa kiasi hicho cha fedha.

(13) Msimamizi wa uchaguzi, atakapoombwa na mgombea, au kwa niaba yake, kutoa hati kuhusu mdhamini aliyeandikishwa katika eneo la uchaguzi analohudumu, atatoa hati hiyo ipasavyo.

(14) Endapo baada ya siku ya uteuzi, jina la mtu aliyemdhamini mgombea litafutwa kutoka katika Daftari katika eneo la uchaguzi husika, hali hiyo haitabatilisha udhamini wa mgombea.

Dhamana

**51**.-(1) Wakati wa kurudisha fomu ya uteuzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 50, mgombea ataweka dhamana kwa msimamizi wa uchaguzi ya kiasi cha fedha kitakachoainishwa.

(2) Dhamana ya mgombea anayepingwa itataifishwa kwa Serikali ikiwa atajiondoa kugombea baada ya siku ya uteuzi au ikiwa idadi ya kura alizopigiwa katika uchaguzi ni chini ya moja ya kumi ya kura zote zilizohesabiwa katika jimbo ambalo alikuwa ni mgombea, isipokuwa dhamana hiyo haitataifishwa ikiwa mgombea atafariki.

(3) Endapo dhamana ya mgombea haitataifishwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (2), mapema iwezekanavyo baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi atamrejeshea mgombea au mwakilishi wake wa kisheria kama

itakavyokuwa.

Mgombea kuteuliwa kwa jimbo moja tu

**52**. Mtu hatateuliwa kuwa mgombea wa uchaguzi katika jimbo zaidi ya moja au nafasi nyingine yoyote ya kuchaguliwa.

Pingamizi na uamuzi juu ya uhalali wa fomu ya uteuzi

**53**.-(1) Pingamizi linaweza kuwekwa dhidi ya fomu ya uteuzi kutokana na sababu zote au yoyote kati ya sababu zifuatazo:

(a) taarifa zilizotolewa kuhusu mgombea hazitoshelezi kumtambulisha;

(b) fomu ya uteuzi haikidhi au haikuwasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii;

(c) ni dhahiri kutokana na taarifa zilizomo katika fomu ya uteuzi kwamba mgombea hana sifa za kugombea;

(d) masharti yaliyoainishwa katika kifungu cha 50(3) hayajazingatiwa; na

Sura ya 278

(e) masharti ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi hayajazingatiwa.

(2) Pingamizi dhidi ya fomu ya uteuzi halitakubaliwa isipokuwa kama limewasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili alasiri ya siku inayofuatia siku ya uteuzi.

(3) Pingamizi linaweza kuwekwa na mgombea mwingine ndani ya jimbo, Msajili wa Vyama vya Siasa au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, isipokuwa kwa pingamizi chini ya kifungu kidogo cha (1)(e) ambalo linaweza kuwekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa pekee, na litawekwa kwa maandishi na kusainiwa na mweka pingamizi, na litabainisha sababu za pingamizi.

(4) Msimamizi wa uchaguzi, kabla ya kuamua juu ya uhalali wa pingamizi lolote na bila kuchelewa-

(a) atamtaarifu mtu aliyewekewa pingamizi; na

(b) atampa mtu huyo nafasi ya kusikilizwa.

(5) Endapo msimamizi wa uchaguzi atatoa uamuzi kuhusiana na pingamizi lolote chini ya kifungu kidogo cha (4), atamjulisha kwa maandishi mgombea anayehusika kuhusu uamuzi na sababu za uamuzi huo.

(6) Mgombea yeyote ambaye hataridhika na

uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu uhalali wa pingamizi, kwa kuzingatia utaratibu na ndani ya muda utakaoainishwa na Tume, anaweza kukata rufaa kwa Tume, na uamuzi wa Tume utakuwa ni wa mwisho na hautahojiwa na mahakama yoyote, isipokuwa kwa njia ya mashauri ya uchaguzi yatakayowasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sura ya Nane kutokana na sababu moja au nyinginezo zilizoainishwa katika Sura hiyo.

(7) Bila kujali masharti yoyote ya kifungu hiki, endapo Msajili wa Vyama vya Siasa ataweka pingamizi chini ya kifungu kidogo cha (3), pingamizi hilo litawasilishwa ndani ya siku kumi na nne baada ya siku ya uteuzi.

Mgombea pekee nafasi ya ubunge au kukosekana kwa mgombea

**54**.-(1) Endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya ubunge aliyeteuliwa, msimamizi wa uchaguzi atamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee wa nafasi ya ubunge.

(2) Mgombea wa nafasi ya ubunge aliyetangazwa chini ya kifungu kidogo cha (1) atapigiwa kura ya ndio au hapana na atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa Mbunge endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa.

(3) Endapo mgombea pekee wa kiti cha ubunge atashindwa kupata idadi ya kura zinazohitajika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), msimamizi wa uchaguzi ataitaarifu Tume kuhusu matokeo hayo na Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, itapanga siku nyingine ya uteuzi na upigaji kura itakayofaa sio zaidi ya siku arobaini baada ya siku ya uchaguzi.

(4) Ikiwa msimamizi wa uchaguzi ataamua kuwa hakuna mgombea aliyeteuliwa kihalali kwa ajili ya kiti cha ubunge katika jimbo, msimamizi wa uchaguzi ataitaarifu Tume.

Picha

**55**.-(1) Kwa madhumuni ya kuwasaidia wapiga kura kumtambua mgombea wakati wa kupiga kura, kila mgombea atatambuliwa kwa kutumia picha ya mgombea ambayo imeidhinishwa na msimamizi wa uchaguzi.

(2) Picha ya mgombea itakayooneshwa wakati wa kampeni za uchaguzi itakuwa chini ya usimamizi wa msimamizi wa uchaguzi.

## SURA YA TANO
## UCHAGUZI WA MADIWANI

### SEHEMU YA KWANZA
### KUENDESHA UCHAGUZI NA MUDA WA KUWEPO MADARAKANI KWA MADIWANI

Uchaguzi wa madiwani

**56**.-(1) Kutafanyika uchaguzi wa madiwani katika mamlaka za serikali za mitaa kila mwaka wa tano baada ya uchaguzi wa madiwani uliopita, na wakati wowote Halmashauri mpya inapoanzishwa.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), uchaguzi wa madiwani hautafanyika pale ambapo uanzishwaji wa Hamashauri mpya haujabadilisha mipaka ya majimbo ya ubunge.

(3) Uchaguzi wa madiwani wa mamlaka za serikali za mitaa utafanyika katika kila kata au kadri itakavyokuwa, kwa kata ya mamlaka ya serikali za mitaa katika tarehe itakayotangazwa na Tume kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

(4) Notisi itakayotolewa chini ya kifungu hiki itaainisha siku na saa ambayo wasimamizi wa uchaguzi wanaweza kupokea fomu za uteuzi wa wagombea wa uchaguzi katika kata yoyote ambayo notisi hiyo inahusika.

(5) Uendeshaji wa kila uchaguzi utakuwa kwa mujibu wa maelekezo na usimamizi wa Tume katika eneo ambalo uchaguzi unafanyika.

Uchaguzi mdogo

**57**.-(1) Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa atatangaza kiti cha diwani yeyote wa halmashauri kuwa wazi mara atakapotaarifiwa kwa maandishi na Mwenyekiti wa Halmashauri kuwa-

(a) mjumbe amefariki au amejiuzulu;

(b) mjumbe, kwa mujibu wa masharti ya au chini ya Sheria hii au Sheria nyingine yoyote,

ameondolewa au ametangazwa kuwa hana uwezo wa kuwa au kuendelea kuwa mjumbe;

(c) uchaguzi wa mjumbe umetangazwa kuwa batili;

(d) kiti cha mjumbe kinachukuliwa kuwa wazi chini ya Sheria hii; au

(e) mjumbe amekoma kuwa mwanachama wa chama cha siasa ambacho kilimdhamini mjumbe huyo kuwa mgombea.

(2) Kwa madhumuni ya kujaza nafasi za wazi zilizojitokeza kwenye kata mbalimbali katika kalenda ya mwaka, Tume itaendesha uchaguzi mdogo angalau mara mbili kwa kila mwaka katika tarehe ambazo Tume itaainisha kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

(3) Notisi chini ya kifungu hiki itaainisha siku na saa ambayo wasimamizi wa uchaguzi wanaweza kupokea fomu za uteuzi wa wagombea wa uchaguzi katika kata ambayo nafasi wazi imetokea.

Uwakilishi katika kata na muda wa madiwani kuwa madarakani

**58**.-(1) Kutakuwa na diwani mmoja aliyechaguliwa kwa kila kata ambapo eneo la halmashauri limegawanywa, na kila diwani baada ya tarehe inayofuata tarehe ambayo matokeo ya uchaguzi yatathibitishwa na msimamizi wa uchaguzi, atakuwa mjumbe aliyechaguliwa kuwa mjumbe wa halmashauri ambayo amechaguliwa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kipindi cha kuwa madarakani kwa mjumbe aliyechaguliwa katika halmashauri kitakuwa ni miaka mitano isipokuwa mjumbe aliyechaguliwa katika uchaguzi mdogo atakuwa madarakani kwa muda uliosalia wa kipindi cha madaraka cha mjumbe aliyetangulia.

(3) Endapo nafasi wazi itatokea ndani ya miezi kumi na mbili kabla ya tarehe ya kawaida ya kumalizika kwa muda wa mjumbe ambaye nafasi yake iko wazi, uteuzi au uchaguzi hautafanyika kujaza nafasi hiyo, isipokuwa nafasi hiyo itajazwa katika uteuzi au uchaguzi wa madiwani utakaofuata.

SEHEMU YA PILI

## SIFA ZA WAGOMBEA UDIWANI

Sifa za mgombea

**59**.-(1) Mtu atachaguliwa kuwa mgombea katika uchaguzi wa udiwani ikiwa ana sifa za kuchaguliwa.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa ikiwa atatimiza masharti yafuatayo-

(a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano;

(b) ametimiza umri wa miaka ishirini na moja;

(c) hajapoteza sifa za kuchaguliwa chini ya masharti ya kifungu cha 60;

(d) ni mkazi wa kawaida ndani ya eneo la mamlaka ya serikali za mitaa;

(e) anajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza;

(f) ni mwanachama na amedhaminiwa na chama cha siasa kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa; na

Sura ya 258

(g) ana kipato halali kinachomwezesha kuishi.

Kukosa sifa ya uteuzi

**60.**-(1) Mtu atakosa sifa ya kuteuliwa katika uchaguzi-

(a) ikiwa ana kiapo cha utii kwa nchi nyingine tofauti na Jamhuri ya Muungano;

(b) ikiwa katika sheria yoyote ile inayotumika Tanzania imethibitika kuwa hana akili timamu;

(c) ikiwa ametiwa hatiani kwa kosa la kukwepa kulipa kodi ndani ya kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi;

(d) endapo amehukumiwa adhabu ya kifo na mahakama yoyote ya Tanzania au amehukumiwa kutumikia kifungo kinachozidi miezi sita gerezani;

(e) endapo yupo kizuizini chini ya amri iliyotolewa chini ya Sheria ya Uwekaji Kizuizini kwa Usalama na amekuwa kizuizini chini ya amri hiyo kwa kipindi kinachozidi miezi sita;

Sura ya 361

(f) endapo ameondolewa nchini, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Uhamisho wa Wahalifu

Sura ya 380

kwa amri iliyotolewa chini ya Sheria hiyo ambayo inaendelea kwa kipindi kinachozidi miezi sita;

(g) iwapo ni sehemu ya, au ni mbia katika shirika, au ni meneja wa kampuni ambayo ni sehemu ya mkataba wowote unaoendelea na mamlaka ya serikali za mitaa ambayo anataka kuchaguliwa na hajatangaza katika magazeti yanayochapishwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza yanayosambazwa ndani ya eneo la mamlaka inayohusika, taarifa inayoelezea aina ya mkataba na maslahi yake au maslahi ya shirika au kampuni katika mkataba;

(h) ikiwa amepoteza sifa za kuwa mjumbe wa mamlaka ya serikali za mitaa kwa Sheria hii au chini ya sheria nyingine yoyote;

(i) ikiwa amepoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya Sheria hii au amepoteza sifa ya kupiga kura katika uchaguzi wowote chini ya Sheria hii au chini ya sheria nyingine yoyote inayohusu makosa ya uchaguzi; na

(j) kwa kuzingatia upekee na ukomo kama Rais anavyoweza kuelekeza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, iwapo anashikilia au anakaimu nafasi katika ofisi yoyote au uteuzi katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano au mamlaka za serikali za mitaa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)(d)-

(a) adhabu mbili au zaidi zinazopaswa kutumikiwa kwa kufuatana zitachukuliwa kuwa ni adhabu tofauti, na iwapo adhabu zote hazizidi miezi sita zitachukuliwa kuwa ni adhabu moja; na

(b) adhabu ya kifungo iliyotolewa kama mbadala wa kulipa faini au kwa kushindwa kulipa faini haitazingatiwa.

## SEHEMU YA TATU
## UTEUZI WA WAGOMBEA UDIWANI

Siku ya uteuzi

**61**.-(1) Endapo uchaguzi wa diwani utafanyika katika kata, au ikiwa uchaguzi huo utasitishwa na taratibu za uchaguzi zitatakiwa kuanza upya, Tume, kwa notisi itakayochapisha katika Gazeti la Serikali, itapanga siku ya uteuzi kwa ajili ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi.

(2) Tume inaweza kupanga siku tofauti za uteuzi kwa ajili ya kata tofauti na inaweza kutengua siku ya uteuzi iliyopangwa na kupanga siku nyingine kuwa siku ya uteuzi.

(3) Tume itatoa taarifa ya angalau siku saba kwa ajili ya uteuzi.

Uteuzi wa mgombea

**62.**-(1) Ili mtu aweze kuteuliwa kihalali kuwa mgombea katika kata, ni lazima awe amedhaminiwa kwa maandishi na wapiga kura wasiopungua kumi walioandikishwa katika kata ambayo yeye ni mgombea.

(2) Uteuzi utafanyika kwa kutumia fomu itakayoainishwa ambayo itazingatia matumizi ya watu wenye mahitaji maalumu, itakayosainiwa na mgombea na watu wanaomdhamini mgombea huyo na itakuwa na taarifa zifuatazo:

(a) jina, anwani na kazi ya mgombea;
(b) majina na anwani za wadhamini na namba za kadi zao za kupiga kura;
(c) tamko la mgombea kuwa yupo tayari na anazo sifa za kuwa mgombea katika uchaguzi;
(d) uthibitisho wa msimamizi wa uchaguzi katika kata ambayo wadhamini wameandikishwa; na
(e) kiapo cha mgombea kitakachojazwa na kusainiwa na mgombea mbele ya hakimu na kitakachoonesha sifa za mgombea na kuwa hajapoteza sifa kwa ajili ya uchaguzi.

(3) Kila fomu ya uteuzi itaambatishwa na-

(a) idadi ya picha za mgombea kama Tume itakavyoelekeza, zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi; na
(b) taarifa binafsi zinazomhusu mgombea kama

itakavyohitajika kutolewa na kanuni katika fomu hiyo kama itakavyokuwa imeelekezwa.

(4) Endapo, kwa vyovyote vile, fomu ya uteuzi haijaambatishwa na nyaraka zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (3), uteuzi wa mgombea utachukuliwa kuwa batili:

Isipokuwa kwamba, Tume, katika mazingira yoyote mahsusi na kama itaona kuna sababu ya kufanya hivyo, inaweza kuelekeza kuwa fomu ya uteuzi ikubaliwe kuwa halali bila kujali kuwa fomu hiyo ya uteuzi haikuambatishwa na nyaraka zozote iwapo nyaraka zinazohusika zitawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi ndani ya muda mwingine kama ambavyo Tume inaweza kuruhusu.

(5) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), katika siku ya uteuzi, Tume inaweza kukataa kumteua mtu kuwa mgombea iwapo itaridhika kuwa mtu huyo ameondolewa kushiriki katika mchakato wa uteuzi na Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

Sura ya 278

(6) Msimamizi wa uchaguzi atatoa fomu za uteuzi kwa mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi na atampa idadi ya fomu za uteuzi kama itakavyoelekezwa na Tume.

(7) Kila mgombea atawasilisha fomu za uteuzi zilizosainiwa kama ilivyoainishwa chini ya kifungu hiki, katika ofisi ya msimamizi wa uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi.

Isipokuwa kwamba, ikiwa Tume itaona zipo sababu za msingi za mgombea mwenyewe kushindwa kuwasilisha fomu hizo, kiongozi wa chama kilichomdhamini anaweza kuwasilisha fomu hizo kwa niaba yake.

(8) Msimamizi wa uchaguzi, mapema iwezekanavyo atabandika nakala ya fomu ya uteuzi katika sehemu ya wazi inayoonekana nje ya ofisi yake.

(9) Mtu hatamdhamini mgombea zaidi ya mmoja kwa uchaguzi mmoja na iwapo msimamizi wa uchaguzi ametoa hati chini ya kifungu kidogo cha (4)(b) kwa ajili

ya udhamini wa mgombea mmoja, atakataa kutoa hati ya udhamini wa mtu huyo kwa mgombea mwingine katika uchaguzi mmoja:

Isipokuwa kwamba, mtu hatazuiwa kusaini fomu ya uteuzi kwa sababu tu amekwisha saini fomu ya mgombea aliyefariki au aliyejitoa kabla ya kuwasilisha fomu ya uteuzi ya mwanzo.

(10) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (9), iwapo mdhamini atamdhamini mgombea zaidi ya mmoja katika uchaguzi mmoja na hati zimetolewa chini ya kifungu kidogo cha (2)(d) kwa ajili ya uandikishwaji wa mtu huyo, udhamini wa wagombea wote wawili utakuwa ni halali.

(11) Mtu yeyote atakayemdhamini mgombea zaidi ya moja anatenda kosa, na akitiwa hatiani atalipa faini isiyozidi shilingi laki mbili.

(12) Endapo msimamizi wa uchaguzi ataridhika kuwa mtu yeyote ametenda kosa chini ya kifungu kidogo cha (11), anaweza kufifilisha kosa na kuamuru mtu huyo kulipa kiasi cha fedha:

Isipokuwa kama-

(a) kiasi hicho cha fedha kitakachotozwa hakitakuwa zaidi ya kiasi cha juu cha faini iliyowekwa kwa kosa hilo;

(b) mamlaka yaliyotolewa na kifungu hiki kidogo yatatumika kama mtu atakiri kwa maandishi kuwa ametenda kosa; na

(c) Msimamizi wa uchaguzi atatoa stakabadhi ya malipo kwa mtu aliyetoa kiasi hicho cha fedha.

(13) Msimamizi wa uchaguzi, atakapoombwa na mgombea, au kwa niaba yake, kutoa hati kuhusu mdhamini aliyeandikishwa katika eneo la uchaguzi analohudumu, atatoa hati hiyo ipasavyo.

(14) Endapo baada ya siku ya awali ya uteuzi, jina la mtu aliyemdhamini mgombea litafutwa kutoka katika Daftari la kata husika, hali hiyo haitabatilisha udhamini wa mgombea huyo.

Dhamana

**63**.-(1) Wakati wa kurudisha fomu ya uteuzi kwa

mujibu wa masharti ya kifungu cha 62, mgombea ataweka dhamana kwa msimamizi wa uchaguzi ya kiasi cha fedha kitakachoainishwa.

(2) Dhamana ya mgombea anayepingwa itataifishwa kwa Serikali ikiwa atajiondoa kugombea baada ya siku ya uteuzi au ikiwa idadi ya kura alizopigiwa katika uchaguzi ni chini ya moja ya kumi ya kura zote zilizohesabiwa katika kata ambayo alikuwa ni mgombea, isipokuwa dhamana hiyo haitataifishwa ikiwa mgombea atafariki.

(3) Endapo dhamana ya mgombea haitataifishwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (2), mapema iwezekanavyo baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi atamrejeshea mgombea au mwakilishi wake wa kisheria kama itakavyokuwa.

Mgombea kuteuliwa kwa nafasi moja tu

**64**. Mtu hatateuliwa kuwa mgombea wa uchaguzi katika kata zaidi ya moja.

Pingamizi na uamuzi kuhusu uhalali wa fomu ya uteuzi

**65**.-(1) Pingamizi linaweza kuwekwa dhidi ya fomu ya uteuzi kutokana na sababu zote au yoyote kati ya sababu zifuatazo:

(a) taarifa zilizotolewa kuhusu mgombea hazitoshelezi kumtambulisha;

(b) fomu ya uteuzi haikidhi au haikuwasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii;

(c) ni dhahiri kwamba kutokana na taarifa zilizomo katika fomu ya uteuzi mgombea hana sifa za kugombea katika uchaguzi;

(d) masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 62(2) hayajazingatiwa; na

Sura ya 278

(e) masharti ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi hayajazingatiwa.

(2) Hakuna pingamizi dhidi ya fomu ya uteuzi litakalokubaliwa isipokuwa tu limewasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi, si zaidi ya saa kumi kamili alasiri ya siku inayofuatia siku ya uteuzi.

(3) Pingamizi linaweza kuwekwa na mgombea

mwingine ndani ya jimbo, Msajili wa Vyama vya Siasa au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, isipokuwa kwa pingamizi chini ya kifungu kidogo cha (1)(e) ambalo linaweza kuwekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa pekee, na litawekwa kwa maandishi na kusainiwa na mweka pingamizi, na litabainisha sababu za pingamizi.

(4) Msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi kabla ya kuamua juu ya uhalali wa pingamizi lolote na bila kuchelewa-

(a) atamtaarifu mtu aliyewekewa pingamizi; na

(b) atampa mtu huyo nafasi ya kusikilizwa.

(5) Endapo msimamizi msaidizi wa uchaguzi anatoa uamuzi kuhusiana na pingamizi lolote chini ya kifungu kidogo cha (4), atawasilisha uamuzi huo kwa msimamizi wa uchaguzi ambaye bila kuchelewa, atapitia uamuzi unaohusika, na anaweza kukubaliana au kutengua uamuzi wa msimamizi msaidizi wa uchaguzi.

(6) Endapo msimamizi wa uchaguzi anatoa uamuzi kuhusiana na pingamizi lolote chini ya kifungu kidogo cha (4) au (5), atamjulisha mgombea anayehusika kuhusu uamuzi wake na sababu za uamuzi wake.

(7) Mgombea yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu uhalali wa pingamizi, kwa kuzingatia utaratibu na ndani ya muda utakaoainishwa na Tume, anaweza kukata rufaa kwa Tume, na uamuzi wa Tume utakuwa ni wa mwisho na hautahojiwa na mahakama yoyote, isipokuwa kwa njia ya mashauri ya uchaguzi yatakayowasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sura ya Nane kutokana na sababu moja au nyinginezo zilizoainishwa katika Sura hiyo.

(8) Bila kujali masharti yoyote ya kifungu hiki, pingamizi lililowekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, litawasilishwa ndani ya siku kumi na nne baada ya siku ya uteuzi.

Mgombea pekee nafasi ya udiwani

**66.**-(1) Endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa kiti cha udiwani aliyeteuliwa, msimamizi msaidizi wa uchaguzi atamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee wa nafasi ya udiwani.

(2) Mgombea udiwani aliyetangazwa chini ya

kifungu kidogo cha (1) atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa Diwani endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa.

(3) Endapo mgombea pekee wa kiti cha udiwani atashindwa kupata idadi ya kura zinazohitajika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), msimamizi msaidizi wa uchaguzi ataitaarifu Tume kuhusu matokeo hayo na Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, itapanga siku nyingine ya uteuzi na upigaji kura itakayofaa sio zaidi ya siku arobaini baada ya siku ya uchaguzi.

(4) Ikiwa msimamizi wa uchaguzi wa kata yoyote ataamua kuwa hakuna mgombea aliyeteuliwa kihalali kwa ajili ya uchaguzi katika kata hiyo, msimamizi wa uchaguzi ataitaarifu Tume.

Picha

**67**.-(1) Kwa madhumuni ya kuwasaidia wapiga kura kumtambua mgombea wakati wa kupiga kura, kila mgombea atatambuliwa kwa kutumia picha ya mgombea ambayo imeidhinishwa na msimamizi wa uchaguzi.

(2) Picha ya mgombea itakayooneshwa wakati wa kampeni za uchaguzi itakuwa chini ya usimamizi wa msimamizi wa uchaguzi.

## SURA YA SITA
## UCHAGUZI, UTARATIBU WA KUPIGA KURA NA UTEUZI WA WABUNGE NA MADIWANI WANAWAKE VITI MAALUM

### SEHEMU YA KWANZA
### SIKU YA UCHAGUZI

Wagombea walioteuliwa na siku ya uchaguzi

**68**.-(1) Endapo wagombea watateuliwa kwa ajili ya uchaguzi tofauti na uchaguzi mdogo katika jimbo au kata, Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, itapanga si chini ya siku sitini na si zaidi ya siku tisini baada ya siku ya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi katika jimbo au kata:

Isipokuwa kwamba, endapo kuna chaguzi mbili au zaidi zinazoshindaniwa wakati wa uchaguzi wa Wabunge au Madiwani, Tume inaweza kupanga siku tofauti za

uchaguzi kwa majimbo au kata tofauti.

(2) Endapo wagombea watateuliwa kwa ajili ya uchaguzi mdogo katika jimbo au kata, Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, itapanga si zaidi ya siku thelathini baada ya siku ya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi katika jimbo au kata.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2), Tume inaweza, kwa sababu ya msingi au kutokana na kutokea tukio ambalo litazuia uchaguzi kufanyika, kutengua siku ya uchaguzi iliyopangwa awali na kupanga siku nyingine ya uchaguzi.

(4) Endapo uchaguzi utaahirishwa chini ya kifungu kidogo cha (3), muda, utaratibu na namna ya upigaji kura utakaofuata utakuwa kama siku ya mwanzo ya kupiga kura.

Tangazo la uchaguzi

**69**.-(1) Endapo kuna uchaguzi unaoshindaniwa, msimamizi wa uchaguzi, kabla au ifikapo siku nane kabla ya siku ya uchaguzi, atatoa tangazo katika jimbo au kata kwa namna atakavyoona inafaa kuhusu mambo yafuatayo:

(a) siku na muda wa kuanza na kufunga upigaji kura, kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3);
(b) anwani ya kituo au vituo vya kupigia kura;
(c) katika kila eneo la uchaguzi ambalo kuna vituo viwili au zaidi vya kupigia kura, wapiga kura waliopangwa kwa kila kituo cha kupigia kura; na
(d) jina kamili la mgombea, picha zilizopigwa karibuni, finyanzo au nembo ya chama cha siasa kinachomdhamini mgombea, ikiwa ipo.

(2) Siku iliyopangwa kwa ajili ya kupiga kura kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1)(a) katika eneo lolote la uchaguzi, inaweza kutofautiana na siku iliyopangwa kwa eneo lingine la uchaguzi katika jimbo au kata hiyo:

Isipokuwa kwamba-

(a) siku ya uchaguzi katika jimbo itakuwa ni siku ya kupiga kura kwa angalau eneo moja la

uchaguzi katika jimbo au kata hiyo;

(b) siku moja tu ndiyo itakayopangwa kuwa siku ya kupiga kura kwa kila eneo la uchaguzi; na

(c) siku ya mwisho iliyopangwa kwa ajili ya kupiga kura katika eneo lolote la uchaguzi katika jimbo au kata yoyote, itakuwa si zaidi ya muda huo baada ya siku ya uchaguzi katika jimbo au kata hiyo kama Tume itakavyopanga.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)(a), muda wa kuanza kupiga kura utakuwa saa mbili kamili asubuhi na muda wa kufungwa kwa upigaji kura utakuwa ni saa kumi na mbili kamili jioni, isipokuwa kama Tume itaelekeza vinginevyo.

## SEHEMU YA PILI
## KUJITOA, KIFO AU KUTOKUWEPO KWA WAGOMBEA

Kujitoa au kukoma kwa ugombea

**70**.-(1) Mgombea anaweza kujitoa ugombea kwa kutoa taarifa ya maandishi aliyoisaini na kuiwasilisha yeye mwenyewe kwa msimamizi wa uchaguzi na nakala kwa tawi la chama kilichomdhamini kabla ya saa kumi kamili alasiri siku ya uteuzi.

(2) Kila taarifa ya kujitoa chini ya kifungu kidogo cha (1) itaambatishwa na tamko katika fomu itakayoainishwa, ambayo itajazwa na kusainiwa na mgombea mbele ya hakimu.

(3) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), endapo mgombea atajitoa kugombea baada ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi, chama chake hakitaruhusiwa kuweka mgombea mwingine mbadala na dhamana iliyotolewa na mgombea itataifishwa.

Kufariki kwa mgombea

**71**.-(1) Endapo baada ya saa kumi kamili alasiri ya siku ya uteuzi na kabla ya kufunga kupiga kura kwenye uchaguzi, mgombea katika jimbo au kata atafariki, Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya kujiridhisha na taarifa ya kifo atasitisha uchaguzi katika jimbo au kata.

(2) Ikitokea msimamizi wa uchaguzi amesitisha uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo (1), Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la

Serikali, itapanga siku nyingine muafaka si zaidi ya siku thelathini baada ya kusitishwa huko kwa ajili ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi katika jimbo au kata na taratibu za uchaguzi katika jimbo au kata hiyo zitaanza upya:

Isipokuwa kwamba, uteuzi mpya hautafanyika kuhusiana na mgombea mwingine yeyote aliyeteuliwa kihalali katika uteuzi uliopita na kila mgombea atachukuliwa kuwa ameteuliwa kihalali isipokuwa kama atatoa taarifa ya kujitoa.

Kutokuwepo kwa wagombea

**72**. Endapo baada ya siku ya uteuzi kwa sababu ya kifo, kujitoa au kwa sababu nyingine yoyote, hakuna wagombea katika jimbo au kata, Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, itasitisha uchaguzi na kupanga siku nyingine isiyozidi siku thelathini baada ya kusitishwa huko, kwa ajili ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi katika jimbo au kata na taratibu za uchaguzi katika jimbo au kata hiyo zitaanza upya.

## SEHEMU YA TATU
## KAMPENI ZA UCHAGUZI

Kampeni za uchaguzi

**73**.-(1) Endapo kuna uchaguzi unaoshindaniwa katika jimbo au kata, kampeni za uchaguzi zitaendeshwa na mgombea, chama chake au wakala wake.

(2) Mgombea, wakala wake au chama chake cha siasa, kadri itakavyokuwa, atawasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi mapendekezo ya ratiba inayoonesha mpangilio unaopendekezwa kufanya mikutano ya hadhara ya kampeni ya mgombea ikiainisha muda na mahali mikutano itakapofanyika.

(3) Mgombea, wakala wake au chama cha siasa kwa idhini au ridhaa ya mgombea anaweza kuitisha na kuhutubia mkutano wowote wa hadhara katika jimbo au kata utakaofanyika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), kwa lengo la kumwezesha mgombea kuchaguliwa au kuendesha kampeni za hadhara au nyumba kwa nyumba.

(4) Kwa madhumuni ya kuhakikisha amani na

utulivu katika mikutano wakati wa kipindi cha kampeni, msimamizi wa uchaguzi ataitisha mkutano wa wagombea wote au mawakala wa vyama na kupitia ratiba za kampeni za wagombea wote na kama italazimu kuwashauri wagombea kufanya mabadiliko katika ratiba zao kwa lengo la kuepuka migongano ya mikutano.

(5) Kila msimamizi wa uchaguzi atawasilisha nakala ya ratiba iliyoratibiwa kwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Polisi wa Wilaya katika jimbo au kata na ratiba hiyo itachukuliwa kuwa ni taarifa ya mikutano inayopendekezwa kwa madhumuni ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi.

Sura ya 258
Sura ya 332

(6) Bila kujali kifungu kidogo cha (5), mikutano ya hadhara haitafanyika katika jimbo au kata kwa madhumuni ya kuwezesha kampeni za uchaguzi za mgombea katika siku yoyote ya uchaguzi au pale ambapo siku mpya ya uchaguzi imepangwa kwa mujibu wa kifungu cha 71(2), siku nyingine yoyote baada ya siku ya awali ya uchaguzi iliyopangwa.

Upatikanaji na wajibu wa vyombo vya habari vya umma

**74**.-(1) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na vyama vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi huo watakuwa na haki ya kutumia huduma ya vituo vya umma vya kurushia matangazo ya redio na runinga wakati wa kipindi cha kampeni za uchaguzi.

(2) Baada ya kushauriana na wagombea, vyama vya siasa vinavyohusika na maafisa wanaohusika na vyombo vya habari vya umma, Tume itaratibu matumizi ya haki za matangazo chini ya kifungu hiki.

(3) Kila chombo cha habari kinachomilikiwa na Serikali kinachochapisha taarifa kuhusu mchakato wa uchaguzi kitaongozwa na misingi ya kutokuwa na upendeleo na kuepuka ubaguzi kwa namna kitakavyowatendea wagombea katika uandishi wa habari na kwa kiwango cha nafasi kitakachotengwa kwa ajili wagombea.

(4) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu hiki, Tume inaweza kutoa maelekezo kwa maandishi

ambayo yatapaswa kuzingatiwa na chombo chochote cha habari kinachomilikiwa na Serikali.

## SEHEMU YA NNE
## UTARATIBU WA UCHAGUZI

Siku na muda wa kupiga kura

**75**. Katika uchaguzi unaoshindaniwa, upigaji kura utafanyika katika kila eneo la uchaguzi kwa utaratibu ulioelekezwa katika Sehemu hii, katika siku iliyopangwa kwa ajili ya kupiga kura katika eneo hilo la uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 69.

Mpangilio wa chaguzi zinazoshindaniwa

**76**. Msimamizi wa uchaguzi-

(a) ataandaa idadi ya kutosha ya vituo vya kupigia kura katika kila eneo la uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya tangazo lolote lililotolewa chini ya kifungu cha 69;

(b) atateua kwa kila eneo la uchaguzi idadi ya watu watakaojulikana kama wasimamizi wasaidizi wa vituo, kama atakavyoona inafaa kumsaidia msimamizi wa kituo wakati wa kupiga kura katika uchaguzi;

(c) atateua kutoka miongoni mwa wasimamizi wasaidizi wa vituo, mtu atakayekuwa kiongozi wa kituo ambaye atajulikana kama msimamizi wa kituo;

(d) atagawa kwa kila kituo cha kupigia kura vituturi kwa idadi ambayo kwa maoni ya msimamizi wa uchaguzi ataona vinahitajika, ambamo wapiga kura wanaweza kupiga kura zao kwa siri;

(e) atabandika au kuwezesha kubandikwa nje ya kila kituo cha kupigia kura katika sehemu ya wazi tangazo linaloonesha majina kwa mpangilio wa alfabeti za majina ya ukoo au kwa mpangilio mwingine kama Tume itakavyoelekeza, jina kamili la mgombea, picha ambayo imepigwa karibuni ndani ya miezi mitatu na finyanzo au nembo ya chama cha siasa kinachomdhamini mgombea;

(f) ataweka ndani na nje ya kila kituo cha kupigia kura, taarifa zenye maelekezo ya utaratibu wa kufuatwa wakati wa kupiga kura;

(g) atagawa kwa kila msimamizi wa kituo idadi ya masanduku ya kupigia kura na karatasi za kura ambazo kwa maoni ya msimamizi wa uchaguzi ataona zinahitajika;

(h) atagawa kwa kila kituo cha kupigia kura vifaa vya kuandikia ambavyo wapiga kura watatumia kuweka alama katika karatasi ya kura na zana zitakazotumika kuweka alama rasmi katika karatasi za kura;

(i) kwa kuzingatia maelekezo yoyote ambayo Tume inaweza kutoa kwa madhumuni hayo, atagawa kwa kila kituo nakala ya Daftari katika eneo la uchaguzi au sehemu ya Daftari hilo ambayo itakuwa na majina ya wapiga kura walioruhusiwa kupiga kura katika kituo hicho; na

(j) atafanya jambo lingine lolote au kutekeleza majukumu mengine yoyote kama Tume itakavyoelekeza.

Mawakala wa upigaji kura

**77**.-(1) Kila chama cha siasa kinaweza, baada ya kupata ridhaa ya wagombea, kuteua mtu mmoja atakayejulikana kama wakala wa upigaji kura kwa kila kituo ndani ya jimbo au kata ambayo ina mgombea au wagombea kwa madhumuni ya-

(a) kuwabaini watu wanaodanganya kuwa wanastahili kupiga kura;

(b) kumwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea au wagombea katika kituo cha kupigia kura;

(c) kushirikiana na msimamizi wa kituo na wasimamizi wasaidizi wa kituo ili kuhakikisha sheria na taratibu zinazohusu upigaji kura na chaguzi zinazingatiwa katika kituo.

(2) Taarifa ya maandishi ya uteuzi, inayotaja jina na anwani ya kituo cha kupigia kura ambacho wakala amepangiwa, kwa kadri itakavyowezekana, itatolewa kwa msimamizi wa uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya

siku ya uchaguzi au ndani ya muda mfupi zaidi kama Tume itakavyoruhusu:

Isipokuwa kwamba, chama cha siasa kinaweza, kwa taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo hiki, kuteua wakala mbadala wa upigaji kura, ambaye anaweza kuwepo na kutekeleza majukumu yoyote ya wakala wa upigaji kura pale ambapo wakala wa upigaji kura anayehusika hatakuwepo katika kituo, ama kwa kudumu au kwa muda.

(3) Endapo wakala yeyote wa upigaji kura atafariki au kushindwa kutekeleza majukumu yake, chama cha siasa kinachohusika kinaweza kumteua wakala wa upigaji kura mwingine badala yake na mapema iwezekanavyo kitatoa taarifa kwa maandishi kwa msimamizi wa uchaguzi anayehusika kuhusu jina na anwani ya wakala wa upigaji kura aliyeteuliwa na kituo cha kupigia kura alichopangiwa.

(4) Msimamizi wa kituo, kwa kusaidiana na kushirikiana na wakala wa upigaji kura, atatatua au vinginevyo atashughulikia malalamiko katika kituo mara yatakapotokea na kuletwa kwake na mgombea, wakala wa kituo cha kupigia kura, mpiga kura au mtu yeyote aliyeandikishwa na anayestahili kupiga kura katika kituo husika.

Masanduku ya kura

**78**.-(1) Kila sanduku la kura litatengenezwa kwa namna ambayo itaruhusu wapiga kura kuweka karatasi za kura ndani yake bila kuweza kuzitoa karatasi za kura.

(2) Mapema kabla ya kuanza kupiga kura, msimamizi wa kituo katika kila kituo cha kupigia kura ataonesha sanduku tupu la kura kwa watu watakaokuwepo kihalali ili waweze kuona kwamba liko tupu, na atalifunga na kuweka lakiri kwa namna itakayozuia kufunguliwa bila kuvunja lakiri na ataliweka lionekane ili kuweka karatasi za kura na ataendelea kuliweka likiwa limefungwa na kuwekwa lakiri.

Muundo wa karatasi za kura

**79**. Kila karatasi ya kura-

(a) itakuwa na-

(i) jina kamili la mgombea;

(ii) picha iliyopigwa karibuni ndani ya miezi mitatu; na
(iii) finyanzo au nembo ya chama cha siasa kinachomdhamini mgombea, ikiwa ipo;

(b) iwe inaweza kukunjwa; na
(c) itashikizwa katika kishina chenye namba zinazofuatana.

Katazo la kuweka wazi kura

**80**. Mtu aliyepiga kura katika uchaguzi hatatakiwa, katika mwenendo wowote wa mashauri ya kuhoji matokeo ya uchaguzi, kueleza ni mgombea yupi alimpigia kura:

Isipokuwa kwamba, kifungu hiki hakitatumika katika mwenendo wa shauri lolote ambalo hoja inayobishaniwa ni iwapo msimamizi wa kituo katika kutekeleza majukumu chini ya masharti ya kifungu cha 84(3)(b), (c) na (i) alitenda hivyo kwa nia njema.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUPIGA NA KUHESABU KURA

Watu wanaostahili kupiga kura

**81**.-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, kila mtu, ambaye ni raia wa Jamhuri ya Muungano na ambaye wakati uchaguzi wowote unafanyika katika jimbo au kata yoyote chini ya Sheria hii ameandikishwa katika jimbo au kata hiyo kuwa mpiga kura, atastahili kupiga kura katika uchaguzi huo katika jimbo au kata ambayo ameandikishwa au aliandikishwa.

(2) Kila mtu, anapotaka kupiga kura katika uchaguzi chini ya Sheria hii, atajitambulisha kwa msimamizi wa uchaguzi kwa namna ambayo itaelekezwa na mtu hatastahili kupiga kura zaidi ya mara moja katika uchaguzi huo.

Kupoteza sifa za kupiga kura

**82**. Bila kujali masharti ya kifungu cha 81, mtu ambaye ameandikishwa kuwa mpiga kura hatastahili kupiga kura katika uchaguzi wowote iwapo mazingira yatajitokeza kuhusiana na mtu huyo, kama angekuwa hajaandikishwa, yangesababisha mtu huyo kupoteza sifa

za kuandikishwa kama mpiga kura.

Mahali pa kupigia kura

**83.** Kila mtu anayestahilli kupiga kura chini ya masharti ya kifungu cha 81 atapiga kura katika jimbo au kata ambayo ameandikishwa kuwa mpiga kura kwa madhumuni ya uchaguzi, na si mahali pengine.

Utaratibu wa kupiga kura

**84**.-(1) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 77(3) na 109, kila wakala wa kituo cha kupigia kura atakuwepo wakati wa ufunguzi wa upigaji kura katika kituo ambacho ameteuliwa kuwa wakala wa upigaji kura.

(2) Kabla ya kuanza kupiga kura katika kituo cha kupigia kura, wakala wa upigaji kura atatakiwa na msimamizi wa kituo cha kupigia kura kwa namna itakayoainishwa kuwasilisha kwake malalamiko yoyote alilonayo au aliyoyapokea, au maelezo yoyote ya kuridhika kwake namna mpangilio wa upigaji kura katika kituo cha kupigia kura ulivyowekwa.

(3) Upigaji kura katika uchaguzi utafanyika kwa namna ifuatayo:

(a) kila mpiga kura anayetaka kupiga kura atakwenda mwenyewe katika kituo cha kupigia kura alichopangiwa katika eneo la uchaguzi ambalo ameandikishwa, na atamridhisha msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo hicho cha kupigia kura, kuwa yeye ni mpiga kura kama anavyodai na kuwa hajapiga kura katika kituo hicho cha kupigia kura au mahali pengine popote, na mtu huyo anaweza kumridhisha msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo kuwa yeye ni mpiga kura kama anavyodai kwa kuonesha kwa afisa huyo au msimamizi msaidizi wa kituo kadi ya mpiga kura au ushahidi wowote wa maandishi kama Mkurugenzi wa Uchaguzi atakavyoelekeza;

(b) ikiwa mpiga kura hawezi kupiga kura kwa sababu ya ulemavu wa kutoona au sababu nyingine ya kimaumbile au hawezi kusoma, mpiga kura huyo anaweza kumuomba mtu

atakayemchagua isipokuwa msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo, karani mwongozaji, mlinzi wa kituo au wakala wa upigaji kura kumsaidia kupiga kura kwa mujibu wa aya (c) mpaka (k) ya kifungu hiki kidogo na mtu huyo aliyechaguliwa chini ya aya hii atamsaidia mpiga kura asiyezidi mmoja:

Isipokuwa kwamba, pale ambapo katika kaya kutakuwa na mtu zaidi ya mmoja ambao wanahitaji msaada chini ya aya hii, itakubalika kisheria kwa watu wa kaya hiyo kumchagua mtu mmoja wa kuwasaidia;

(c) baada ya kuridhishwa na utambulisho wa mpiga kura na kuwa jina la mpiga kura huyo lipo katika Daftari la eneo hilo la uchaguzi na mpiga kura amepangiwa kupiga kura katika kituo hicho cha kupigia kura, msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo atampa mpiga kura husika karatasi ya kura;

(d) kabla ya msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo kutoa karatasi ya kura kwa mtu yeyote-

(i) karatasi ya kura itagongwa muhuri wenye alama rasmi;

(ii) namba na taarifa za mpiga kura, kama zilivyoainishwa katika nakala ya Daftari au sehemu ya Daftari linalotunzwa katika kituo cha kupigia kura, zitatajwa;

(iii) namba ya mpiga kura katika nakala ya Daftari au sehemu ya Daftari itawekwa alama katika kishina; na

(iv) alama itawekwa mkabala na namba ya mpiga kura katika nakala ya Daftari au sehemu ya Daftari kuonesha kuwa mpiga kura huyo amepokea karatasi ya kura;

(e) kwa kuzingatia masharti ya aya (h), mpiga kura baada ya kupokea karatasi ya kura

atakwenda mara moja kwenye moja ya vituturi vya kupigia kura katika kituo cha kupigia kura na kupiga kura yake kwa siri kwa utaratibu uliolekezwa katika aya (f), atakunja karatasi ya kura ili kuficha kura yake na atakwenda katika sanduku la kura kumuonesha msimamizi msaidizi wa kituo alama rasmi iliyo nyuma ya karatasi ya kura na atatumbukiza karatasi ya kura iliyokunjwa ndani ya sanduku la kupigia kura;

(f) mpiga kura atapiga kura yake kwa kuweka alama katika jina la mgombea anayetaka kumchagua;

(g) mpiga kura hataweka maandishi au alama yoyote inayoweza kumtambulisha katika karatasi ya kura;

(h) mpiga kura atapiga kura bila ya kuchelewa;

(i) iwapo mpiga kura hajui kusoma au haelewi jinsi ya kupiga kura msimamizi wa kituo anaweza, mbele ya wakala wa upigaji kura, kumuelekeza utaratibu wa kupiga kura;

(j) kwa kuzingatia masharti ya aya (b) na (i), mpiga kura hataonesha alama aliyoweka katika karatasi yake ya kura kwa mtu yeyote, na kama atafanya hivyo karatasi ya kura itachukuliwa kuwa imeharibika:

Isipokuwa kwamba, masharti ya aya hii hayatatumika ikiwa karatasi ya kura imeoneshwa na mpiga kura kwa msimamizi wa kituo kwa madhumuni tu ya kuhakikisha kama mpiga kura ametimiza wajibu wake kwa usahihi;

(k) mpiga kura ambaye kwa bahati mbaya ametumia karatasi yake ya kura kwa namna ambayo haitaweza kuhesabika kama karatasi halali ya kura, baada ya kuwasilisha karatasi hiyo kwa msimamizi wa kituo, na kumridhisha msimamizi wa kituo kwamba karatasi hiyo ya kura imeharibika kwa bahati mbaya, atapewa karatasi nyingine badala ya ile iliyoharibika na

mara moja karatasi ya kura iliyoharibika na kishina chake kitawekwa alama kuwa imefutwa.

(4) Kabla ya mchakato wowote wa upigaji kura kuanza, msimamizi wa kituo atamtaka wakala wa upigaji kura wa kila mgombea kujaza kwenye fomu itakayoainishwa na kuwasilisha kwa msimamizi wa kituo-

(a) malalamiko yoyote aliyonayo, kuhusu maandalizi ya kupiga kura;

(b) kuridhishwa kwake na maandalizi ya utaratibu wa upigaji kura katika eneo linalohusika; au

(c) malalamiko yoyote yaliyowasilishwa na mpiga kura yeyote kuhusiana na maandalizi ya upigaji kura katika eneo linalohusika.

(5) Endapo mpiga kura ana malalamiko yoyote kuhusu mwenendo wa uchaguzi katika kituo cha kupigia kura au kata ambayo ameandikishwa kupiga kura, anaweza kuandika malalamiko yake kwenye fomu itakayoainishwa na kuiwasilisha fomu hiyo kwa msimamizi wa kituo cha kupigia kura kabla mpiga kura hajaondoka katika kituo cha kupigia kura.

(6) Endapo malalamiko ya uchaguzi yaliyorejewa katika kifungu kidogo cha (5) yanamhusu msimamizi wa kituo cha kupigia kura, mpiga kura atawasilisha fomu ya malalamiko mbele ya mawakala wa upigaji kura wa wagombea.

Kuruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura

**85**.-(1) Mtu hataruhusiwa kupiga kura katika kituo chochote cha kupigia kura isipokuwa katika kituo cha kupigia kura alichopangiwa katika eneo la uchaguzi ambalo amejiandikisha kama mpiga kura.

(2) Mtu hataruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura isipokuwa wafuatao-

(a) msimamizi wa kituo;

(b) msimamizi msaidizi wa kituo;

(c) wakala wa upigaji kura;

(d) mpiga kura;

(e) mtu anayemsaidia mpiga kura asiyeweza kupiga kura, kwa mujibu wa kifungu cha 84(3)(b);

(f) mtazamaji aliyeidhinishwa na Tume kwa maandishi;
(g) mgombea;
(h) mjumbe wa Tume;
(i) Mkurugenzi wa Uchaguzi;
(j) afisa wa Tume;
(k) mratibu wa uchaguzi wa Mkoa;
(l) afisa anayeshughulikia uchaguzi;
(m) afisa wa polisi au mtu mwingine yeyote anayehusika na usalama katika kituo cha kupigia kura; na
(n) msimamizi wa uchaguzi na msimamizi msaidizi wa uchaguzi.

(3) Msimamizi wa kituo anaweza kwa hiari yake kuwaruhusu angalau watazamaji wasiopungua wawili kama wapo kuingia katika kituo cha kupigia kura.

(4) Tume inaweza kualika watazamaji wa ndani na wa kimataifa na kuandaa mwongozo kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa watazamaji.

(5) Endapo mtu yeyote ataonesha utovu wa nidhamu ndani ya kituo cha kupigia kura au atashindwa kutii amri halali ya msimamizi wa kituo, anaweza mapema iwezekanavyo, kwa amri ya msimamizi wa kituo kuondolewa katika kituo cha kupigia kura na afisa wa polisi yeyote aliyepo ndani au karibu na kituo au na mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi na msimamizi wa kituo au msimamizi wa uchaguzi, na mtu huyo aliyeondolewa hataruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura isipokuwa kwa ruhusa ya msimamizi wa kituo.

(6) Mtu aliyeondolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (5), iwapo atashtakiwa kwa kutenda kosa lolote katika kituo hicho cha kupigia kura, anaweza kuwekwa chini ya ulinzi mpaka atakapofikishwa mbele ya hakimu na mamlaka yaliyotolewa na kifungu hiki hayatatumika kwa lengo la kumzuia mpiga kura yeyote, ambaye kwa namna yoyote anastahili kupiga kura katika kituo chochote cha kupigia kura, kutumia nafasi ya kupiga kura katika kituo hicho cha kupigia kura.

Tuhuma za ukiukwaji wa taratibu

**86**.-(1) Endapo msimamizi wa kituo chochote cha kupigia kura atakuwa na sababu za kuamini, au pale ambapo mgombea au wakala wa upigaji kura aliyepo katika kituo chochote cha kupigia kura anatuhumu kuwa, mtu yeyote anayetaka kupiga kura katika kituo hicho, sio mpiga kura anayestahili kupiga kura katika kituo hicho cha kupigia kura, msimamizi wa kituo atamuonya mtu huyo kuwa kama atapiga kura atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Iwapo, bila kujali onyo hilo, mtu huyo atasisitiza kutaka kupiga kura na-

(a) akatoa ushahidi wowote kuonesha kuwa anastahili kupiga kura katika kituo cha kupigia kura kinachohusika; na

(b) baada ya kutakiwa kutoa na kusaini tamko kama ilivyoelekezwa na kifungu cha 87, atatoa na kutia saini tamko moja au matamko yote ambayo kifungu hicho kimeyaainisha,

msimamizi wa kituo atampa karatasi ya kura mtu huyo na kumruhusu kupiga kura katika kituo hicho.

(3) Msimamizi wa kituo atanakili jina na anwani kamili ya mtu aliyeonywa chini ya kifungu kidogo cha (1) ambavyo mtu huyo ametoa kama jina na anwani yake, na ikiwa mtu huyo amepiga kura, msimamizi wa kituo ataeleza suala hilo katika kumbukumbu.

(4) Kabla ya kumuonya mtu kwa mujibu ya kifungu kidogo cha (1), msimamizi wa kituo atamueleza mtu huyo sababu za kuamini kwake kwamba mtu huyo si mpiga kura anayestahili kupiga kura katika kituo husika cha kupigia kura au, kama tuhuma zinazotajwa katika kifungu kidogo cha (1) zimetolewa na mgombea au wakala wa upigaji kura aliye katika kituo husika cha kupigia kura, atamtaka mgombea au wakala kueleza mbele yake na mbele ya mtu anayetaka kupiga kura sababu za tuhuma, na ikiwa mgombea au wakala atakataa kutekeleza sharti hilo, msimamizi wa kituo atapuuza tuhuma zilizotolewa.

Tamko la kapiga kura

**87.**-(1) Msimamizi wa kituo katika kituo chochote cha kupigia kura anaweza, kwa ridhaa yake, na kwa

maombi ya mgombea aliye katika kituo cha kupigia kura au wakala wa upigaji kura, kumtaka mtu yeyote anayetaka kupiga kura kabla ya kupewa karatasi ya kura, kutoa ushahidi ambao utamtambulisha kwamba mtu huyo ndiye aliyeelezwa katika kadi ya mpiga kura ambayo ameitoa, kama msimamizi wa kituo ataona ni lazima na kumtaka kutoa na kusaini tamko moja au matamko yote yaliyotolewa.

(2) Endapo mtu yeyote atashindwa kutoa ushahidi wa utambulisho wake au atakataa kutoa tamko lolote, msimamizi wa kituo anaweza kukataa kumpa karatasi ya kura.

Kuahirishwa kwa upigaji kura wakati inapotokea vurugu

**88**.-(1) Endapo mwenendo wa upigaji kura katika kituo chochote unakatizwa au kuzuiliwa kwa ghasia au vurugu wakati kuna wapiga kura waliobaki ambao hawajamaliza utaratibu wa kupiga kura, msimamizi wa kituo ataahirisha zoezi mpaka siku inayofuata na mapema iwezekanavyo atampa taarifa msimamizi wa uchaguzi.

(2) Endapo upigaji kura unaahirishwa katika kituo chochote cha kupigia kura-

(a) saa za kupiga kura katika siku ambayo upigaji kura umeahirishwa zitakuwa sawa na siku ya awali ya kupiga kura; na

(b) rejea katika Sheria hii kuhusu kufunga upigaji kura itatafsiriwa ipasavyo.

Kufunga zoezi la upigaji kura

**89**. Endapo muda wa kupiga kura umeisha katika kituo chochote cha kupigia kura na kuna wapiga kura waliopo ambao hawajapata nafasi ya kupiga kura, kituo cha kupigia kura kitakuwa wazi kwa muda wa kutosha kuwawezesha wapiga kura hao kupiga kura.

Utaratibu wa kufunga upigaji kura

**90**.-(1) Kabla ya kufunga kituo cha kupigia kura baada ya upigaji kura kumalizika, wakala wa upigaji kura atapewa nafasi ya mwisho kuwasilisha katika fomu itakayoainishwa kama ameridhika au hajaridhika na mwenendo wa upigaji kura au ana malalamiko kuhusu namna upigaji kura ulivyoendeshwa katika kituo cha kupigia kura na malalamiko yoyote yaliyowasilishwa

yatatatuliwa au yatashughulikiwa kwa namna bora kadri iwezekanavyo.

(2) Wakati wa kuhitimisha upigaji kura, msimamizi wa kituo ataandaa taarifa akieleza kwa kina malalamiko yote yaliyotolewa wakati na baada ya kumalizika kwa upigaji kura na hatua zilizochukuliwa kwa kila malalamiko na taarifa hiyo itasomwa kabla na kuthibitishwa na kusainiwa na wakala wa upigaji kura, msimamizi wa kituo na msimamizi msaidizi wa kituo, na itawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi kwa mujibu wa kifungu cha 102.

Wakala wa upigaji kura kuwa wakala wa kuhesabu kura

**91**.-(1) Kila wakala wa upigaji kura au wakala mbadala wa upigaji kura aliyeteuliwa na chama cha siasa kwa mujibu wa kifungu cha 77 cha Sheria hii, wakati wa kuhesabu kura atakuwa wakala wa kuhesabu kura.

(2) Kila mgombea katika uchaguzi wa Rais, Wabunge au Madiwani anaweza kumteua wakala wa kuhesabu kura kumwakilisha mgombea huyo mahali na wakati wa majumuisho ya matokeo ya uchaguzi yatakayofanywa na Tume, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kadri itakavyokuwa.

Mahali pa kuhesabia kura

**92**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2), kura zote za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani zilizopigwa katika kituo cha kupigia kura zitahesabiwa katika kituo hicho cha kupigia kura.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi au msimamizi wa uchaguzi anaweza, kwa sababu za kiusalama, ufinyu wa nafasi ya kuhesabia au huduma nyingine au kwa sababu nyingine za msingi, kuelekeza kuwa kura za vituo kadhaa vya kupigia kura vilivyo karibu au vituo vyote vya kupigia kura katika eneo la uchaguzi au mchanganyiko wa maeneo ya uchaguzi yaliyo jirani, zitahesabiwa katika sehemu moja.

(3) Endapo maelekezo yametolewa kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), kura kutoka kila kituo cha kupigia kura zitahesabiwa kwa kutenganishwa kwa utaratibu kama vile kura zimehesabiwa katika kituo

ambacho zimepigwa.

(4) Wakati wa kuhitimisha kuhesabu kura katika kituo cha kupigia kura, msimamizi wa kituo kwa msaada wa msimamizi msaidizi wa kituo atazifunga kura zilizohesabiwa katika vifurushi tofauti vya kura zilizohesabiwa na zilizokataliwa.

(5) Wakati wa kuhitimishwa kwa utaratibu chini ya kifungu kidogo cha (4), kila mgombea au wakala wake wa kuhesabu kura ataeleza katika fomu itakayoainishwa iwapo ameridhika au kama ana malalamiko yoyote kuhusu utaratibu huo.

(6) Malalamiko yoyote yaliyowasilishwa chini ya kifungu hiki ambayo yanaweza kutatuliwa, yatashughulikiwa mapema iwezekanavyo na msimamizi wa kituo na tukio hilo litajumuishwa katika taarifa itakayowasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi.

(7) Endapo mgombea au wakala wake wa kuhesabu kura anakataa kujaza au kusaini fomu yoyote chini ya kifungu hiki, msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo atamtaka mgombea huyo au wakala wake kutoa sababu za kukataa kwake kwa maandishi na msimamizi huyo wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo ataandika kukataa huko katika taarifa atakayowasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi.

(8) Mgombea au wakala wake anayekataa kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (7) atazuiliwa kutoa malalamiko yoyote kuhusu mwenendo wa kupiga na kuhesabu kura katika kituo hicho.

Kuhesabu kura

**93**.-(1) Msimamizi wa kila kituo cha kupigia kura akisaidiwa na msimamizi msaidizi wa kituo aliyepangiwa katika kituo hicho, mapema iwezekanavyo baada ya kufunga upigaji kura, mbele ya watu waliorejewa katika kifungu cha 94, ikiwa wapo, atahesabu kura kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa katika Sehemu hii hadi hapo kuhesabu kura kutakapomalizika.

(2) Katika hitimisho la kila hatua ya mchakato wa kuhesabu kura, wagombea au mawakala wa kuhesabu kura kama wapo, watatakiwa kueleza kwa utaratibu uliowekwa kama wameridhika au wana malalamiko

yoyote na kueleza malalamiko hayo ikiwa yapo, kuhusu kila hatua iliyohitimishwa katika kuhesabu kura.

(3) Malalamiko yaliyotolewa ambayo yanaweza kutatuliwa au kuamuliwa, yatatatuliwa au yataamuliwa katika hatua ambayo yametolewa na msimamizi wa kituo ataandaa taarifa katika fomu itakayoainishwa, kuhusu malalamiko hayo na jinsi yalivyotatuliwa.

(4) Kila maelezo yaliyoandikwa na msimamizi wa kituo kwa mujibu wa kifungu hiki yatathibitishwa na wakala wa upigaji kura, msimamizi wa kituo na msimamizi msaidizi wa kituo na yatasainiwa na kuwasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi.

Watu wanaoweza kuwepo wakati wa kuhesabu kura

**94**.(1) Mtu hataruhusiwa kuwepo wakati wa kuhesabu kura isipokuwa wafuatao:

(a) msimamizi wa kituo;
(b) msimamizi msaidizi wa kituo;
(c) wakala wa kuhesabu kura au wakala mbadala wa kuhesabu kura;
(d) mgombea;
(e) afisa wa polisi au mtu mwingine anayehusika na usalama katika sehemu ambayo kura zinahesabiwa;
(f) msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi au mratibu wa uchaguzi wa Mkoa;
(g) mjumbe wa Tume;
(h) Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa wa Tume;
(i) mtazamaji wa uchaguzi aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume; na
(j) afisa anayeshughulikia uchaguzi.

(2) Mtu yeyote tofauti na aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (1) hataruhusiwa kuwepo katika eneo ambalo kura zinahesabiwa.

Taratibu za kuhesabu kura

**95**.-(1) Kabla msimamizi wa kituo na wasimamizi wasaidizi wa kituo hawajaanza kuhesabu kura mbele ya watu waliorejewa katika kifungu cha 94, ikiwa wapo-

(a) watahakiki na kuandika idadi ya watu wote waliopiga kura katika kituo cha kupigia kura;

(b) watahesabu na kuandika idadi na karatasi za kura zote ambazo hazikutumika, zikijumuisha karatasi za kura zozote zilizoharibika na kuzifunga katika bahasha maalumu;
(c) watakagua lakiri na kuhakikisha kama imefunguliwa au imechezewa;
(d) watafungua lakiri; na
(e) watafungua sanduku la kura.

(2) Kwa madhumuni ya Sehemu ya Pili ya Sura ya Sita ya Sheria hii, neno "lakiri" litajumuisha kufuli na utaratibu mwingine wowote, mfumo au kitu ambacho kimeidhinishwa na Tume kwa ajili ya kutunza usalama wa vitu vilivyomo katika sanduku la kupigia kura, na maneno lakiri, fungua, funga au fungua lakiri na mabadiliko yake ya kisarufi na misemo inayofanana itakapotumika kwa ajili ya lakiri au sanduku la kura, yatakuwa na maana inayofanana.

(3) Baada ya sanduku la kura kufunguliwa, msimamizi wa kituo atatoa na kuhesabu kwa sauti kila karatasi ya kura na kuandika jumla ya kura zilizopatikana ndani ya sanduku la kura.

(4) Baada ya kuhakikisha jumla ya karatasi za kura katika sanduku la kura, kura hizo zitahesabiwa kama ifuatavyo:

(a) msimamizi wa kituo atakunjua kila karatasi ya kura, ataionesha kwa watu wote waliopo na atataja kwa sauti mgombea ambaye amepigiwa kura hiyo au kama karatasi ya kura haikujazwa, imeharibika au vinginevyo si halali;
(b) karatasi za kura ambazo zimetajwa zitawekwa kwa mpangilio na katika mafungu tofauti zikionesha upande wa juu, kulingana na mgombea aliyepigiwa kura hiyo au kura isiyojazwa au isiyo halali;
(c) msimamizi wa kituo atahesabu kwa sauti na kuandika idadi ya kura katika kila fungu na kuhakiki jumla yake kwa kulinganisha na jumla ya idadi ya karatasi za kura zilizopatikana ndani ya sanduku la kura na

idadi ya wapiga kura waliopiga kura katika kituo cha kupigia kura.

Karatasi ya kura ambayo haitahesabika kuwa halali

**96**.-(1) Karatasi ya kura haitahesabiwa kuwa halali iwapo-

(a) haina alama rasmi;
(b) kura iliyopigwa imepigwa kinyume na kifungu cha 84 au inatakiwa chini ya kifungu hicho kuchukuliwa kuwa imeharibika;
(c) imeandikwa kitu chochote au kuwekwa alama ambayo inaweza kumtambulisha mpiga kura tofauti na namba iliyochapwa kwenye karatasi ya kura; au
(d) haijawekwa alama au ni batili kwa kutoeleweka.

(2) Kura yoyote itakayopigwa kwa mgombea yeyote aliyejitoa ugombea chini ya Sheria hii itachukuliwa kuwa kura iliyoharibika.

Uthibitisho wa msimamizi wa kituo

**97**.-(1) Msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo ataandika neno “imekataliwa” juu ya karatasi ya kura ambayo, chini ya masharti ya kifungu cha 96 haijahesabiwa.

(2) Msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo ataongeza kwa kuandika maneno “kukataliwa kumepingwa” kama pingamizi dhidi ya uamuzi wake limetolewa na wakala yeyote wa kuhesabu kura.

Karatasi za kura zilizokataliwa

**98**. Msimamizi wa kituo ataandaa maelezo yanayoonesha idadi ya karatasi za kura zilizokataliwa yenye vichwa vya taarifa vifuatavyo:

(a) kukosekana kwa alama rasmi;
(b) kura imepigwa kinyume na ilivyoelezwa katika kifungu cha 84(3)(c) au ichukuliwe kuwa imeharibika chini ya masharti ya kifungu cha 84(3)(j);
(c) maandishi au alama ambayo itamtambulisha mpiga kura;
(d) haina alama au batili kwa kutoeleweka; na
(e) kura imepigwa kwa wagombea zaidi ya wale

ambao mpiga kura anastahili kuwapigia kura chini ya kifungu cha 84(3)(f),

na kwa maombi, atamruhusu wakala wa kuhesabu kura yeyote kutoa nakala ya maelezo hayo.

Kufungana kwa kura na kurudia kuhesabu katika uchaguzi unaoshindaniwa

**99**.-(1) Endapo kwa mujibu wa kifungu cha 103 au 104 kunatokea kufungana kwa kura baina ya wagombea katika uchaguzi unaoshindaniwa kiasi kwamba nyongeza ya kura moja ingefanya yeyote kati yao kutangazwa kuchaguliwa, msimamizi wa uchaguzi atarudia kuhesabu kura zilizopigwa.

(2) Endapo kuna kufungana tena kwa kura kama ilivyothibitishwa kwa kurudia kuhesabu kura, msimamizi wa uchaguzi, kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki atatoa taarifa ya maelezo hayo kwa Tume, ambayo, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, itapanga siku nyingine inayofaa, si zaidi ya siku thelathini baada ya siku ya uchaguzi, kwa ajili ya kupiga kura kwa wagombea ambao kura zao zilifungana katika upigaji kura wa kwanza.

Wagombea au mawakala wa kuhesabu kura wanaweza kuomba kurudia kuhesabu kura

**100**.-(1) Mgombea au wakala wake wa kuhesabu kura, iwapo watakuwepo wakati wa kuhesabu au kurudia kuhesabu kura kunapomalizika, anaweza, kumtaka msimamizi wa kituo kurudia kuhesabu kura mara moja au mbili lakini msimamizi wa kituo anaweza kukataa kuhesabu mara ya tatu au zaidi kama matokeo ya kurudia kuhesabu kura mara mbili za mwisho yanalingana.

(2) Hatua hazitachukuliwa baada ya kumaliza kuhesabiwa au kurudiwa kuhesabiwa kura mpaka wagombea na mawakala wa kuhesabu kura waliopo kituoni wakati wa kumaliza kuhesabu kura watakapokuwa wamepewa nafasi ya kutosha kutumia haki iliyotolewa katika kifungu kidogo cha (1).

Uamuzi wa msimamizi wa kituo

**101**. Msimamizi wa kituo, baada ya kushauriana na msimamizi msadizi wa kituo, mawakala, au wagombea kama wapo, ataamua hoja itakayojitokeza kuhusu karatasi yoyote yenye mgogoro, uamuzi utatakiwa kurejewa na msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa

uchaguzi wakati wa kujumlisha kura kutoka vituo vyote vya kupigia kura katika jimbo au kata, na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi utakuwa wa mwisho na unaweza tu kuhojiwa kwa kurejewa katika shauri la uchaguzi kwa mujibu wa Sura ya Nane ya Sheria hii.

Wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura

**102**.-(1) Baada ya kuhitimisha kuhesabu kura kwa mujibu wa kifungu cha 93, msimamizi wa kituo-

(a) atafunga katika vifurushi tofauti karatasi za kura halali, zenye mgogoro na zilizokataliwa;
(b) ataandaa taarifa tofauti za matokeo kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa namna Tume itakavyoelekeza, ambazo zitasainiwa na msimamizi wa kituo na mawakala, ikiwa wapo;
(c) atawataka mawakala wa kuhesabu kura, au mgombea kama yupo, kueleza katika fomu maalum malalamiko yoyote au kuthibitisha kuridhika namna kura zilivyohesabiwa;
(d) atabandika katika sehemu ya wazi nakala ya matokeo ya awali ya uchaguzi katika kituo cha kupigia kura;
(e) iwapo fomu za taarifa za matokeo zipo za kutosha, atampa kila wakala wa kuhesabu kura nakala ya taarifa ya matokeo;
(f) ataweka vifurushi vyote vya karatasi za kura ndani ya sanduku la kura na kulifunga kwa lakiri; na
(g) akiwa ameongozana na mawakala wa vituo vya kupigia kura waliopo kwa idadi itakayoelekezwa na tume, atapeleka na kukabidhi kwa msimamizi wa uchaguzi sanduku la kura pamoja na taarifa ya matokeo ya uchaguzi wa kituo cha kupigia kura.

(2) Endapo mgombea au wakala wake atakataa kusaini fomu iliyoainishwa chini ya kifungu hiki, msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo atamtaka mgombea huyo au wakala kutoa sababu za kukataa kwa maandishi.

(3) Endapo mgombea au wakala wake atakataa kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (2) atazuiliwa kutoa malalamiko yoyote kuhusu utaratibu wa kupiga na kuhesabu kura katika kituo husika.

Majumuisho ya kura katika uchaguzi wa wabunge

**103**.-(1) Masharti ya kifungu cha 45 yatatumika kwa kuzingatia maboresho yatakayohitajika kuhusu kujumlisha kura katika uchaguzi wa wabunge.

(2) Watu wafuatao wanaruhusiwa kuwepo katika kituo cha kujumlisha kura:

(a) msimamizi wa uchaguzi;
(b) msimamizi msaidizi wa uchaguzi;
(c) mratibu wa uchaguzi wa Mkoa;
(d) mjumbe wa Tume;
(e) Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa wa Tume;
(f) mgombea;
(g) wakala wa kuhesabu kura;
(h) afisa wa polisi au mtu mwingine anayehusika na usalama wa mahali pa kuhesabia kura;
(i) mtazamaji aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume; au
(j) afisa anayeshughulikia uchaguzi.

(3) Baada ya taarifa zote za matokeo na masanduku ya kura yenye karatasi za kura zinazotokana na uchaguzi wa Wabunge kupokelewa kutoka kwenye vituo vya kupigia kura katika jimbo, msimamizi wa uchaguzi, baada ya kuamua uhalali wa kura zenye mgogoro na kabla ya kujumlisha kura hizo, atatangaza kwa sauti matokeo ya kila kituo cha kupigia kura katika jimbo kwa kufuatana.

(4) Mgombea au wakala wa upigaji kura anaweza kumuomba msimamizi wa uchaguzi kuangalia sehemu yoyote ya majumuisho ili kuhakiki usahihi wake lakini hatastahili kuomba kurudia kuhesabu kura zote au karatasi zote za kura kutoka katika kituo chochote cha kupigia kura, isipokuwa kama usahihi wa taarifa ya matokeo kutoka kituo hicho cha kupigia kura ulipingwa na wakala wa upigaji kura au mgombea aliyekuwepo katika kituo cha kupigia kura.

(5) Endapo maombi yatakuwa yamefanywa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4), msimamizi wa uchaguzi bila sababu za msingi, hatakataa kuhakiki majumuisho au kurudia kuhesabu karatasi za kura katika kituo chochote cha kupigia kura.

Majumuisho ya kura katika uchaguzi wa madiwani

**104**.-(1) Watu wafuatao wanaruhusiwa kuwepo katika kituo cha kujumlisha kura-

(a) msimamizi wa uchaguzi;
(b) msimamizi msaidizi wa uchaguzi;
(c) mratibu wa uchaguzi wa Mkoa;
(d) mjumbe wa Tume;
(e) Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa wa Tume;
(f) mgombea;
(g) wakala wa kuhesabu kura;
(h) afisa wa polisi au mtu mwingine anayehusika na usalama wa mahali pa kuhesabia kura;
(i) mtazamaji aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume; au
(j) afisa anayeshughulikia uchaguzi.

(2) Baada ya taarifa zote za matokeo na masanduku ya kura yenye karatasi za kura zinazotokana na uchaguzi wa madiwani kupokelewa kutoka kwenye vituo vya kupigia kura katika kata, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kadri itakavyokuwa, baada ya kuamua uhalali wa kura zozote zenye mgogoro na kabla ya kujumlisha kura, atatangaza kwa sauti matokeo ya kila kituo cha kupigia kura katika kata kwa kufuatana.

(3) Baada ya kuhitimisha utaratibu chini ya kifungu kidogo cha (2) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi ataendelea kujumlisha pamoja idadi ya-

(a) kura zote zilizopigwa katika kata;
(b) kura zote zilizopigwa kwa kila mgombea; na
(c) karatasi za kura zilizokataliwa.

Kutangaza matokeo ya ubunge

**105**.-(1) Endapo matokeo ya uchaguzi unaoshindaniwa yamehakikiwa, msimamizi wa uchaguzi-

(a) mapema iwezekanavyo atatangaza kuchaguliwa kwa mgombea aliyepigiwa kura nyingi halali;
(b) atamtaarifu mgombea aliyeshinda kuhusu kuchaguliwa kwake;
(c) atahakikisha taarifa kamili ya matokeo inabandikwa kwenye makao makuu ya Halmashauri inayohusika; na
(d) ataandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Tume ikionesha-
    (i) malalamiko yaliyotolewa katika kila hatua ya uchaguzi na hatua au uamuzi uliochukuliwa kwa kila malalamiko;
    (ii) maoni ya wagombea kuhusu uchaguzi; na
    (iii) matokeo ya uchaguzi,

na Tume itaelekeza matokeo, pamoja na idadi ya kura alizopata kwa kila mgombea katika kila jimbo, kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Endapo itatokea Mbunge mteule hana nia ya kuendelea na ubunge au kufariki kabla ya kuapishwa, chama cha siasa kinachomdhamini mwanachama husika, kitaitaarifu Tume kwa maandishi na Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, itateua siku nyingine ya uteuzi wa mgombea kwa mujibu wa kifungu cha 49.

(3) Tume inaweza kusitisha mchakato wa uchaguzi pale itakapobainika kuwa kuna ukiukwaji wa Sheria na taratibu za uchaguzi, na ndani ya siku thelathini itatangaza siku nyingine ya uchaguzi.

Kutangaza matokeo ya udiwani

**106**.-(1) Endapo matokeo ya uchaguzi yamehakikiwa, msimamizi wa uchaguzi-
(a) mapema iwezekanavyo atatangaza kuchaguliwa mgombea aliyepigiwa kura nyingi halali;
(b) atamtaarifu mgombea aliyeshinda kuhusu kuchaguliwa kwake;
(c) atahakikisha taarifa kamili ya matokeo inabandikwa kwenye Ofisi ya Afisa Mtendaji

wa Kata na Makao Makuu ya Halmashauri inayohusika;

(d) ataandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Tume ikionesha-

(i) malalamiko yaliyotolewa katika kila hatua ya uchaguzi na hatua au uamuzi uliochukuliwa kwa kila malalamiko;

(ii) maoni ya wagombea kuhusu uchaguzi; na

(iii)matokeo ya uchaguzi,

na Tume itaelekeza matokeo, pamoja na idadi ya kura alizopata kwa kila mgombea katika kila jimbo, kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Endapo itatokea Diwani mteule hana nia ya kuendelea na udiwani au kufariki kabla ya kuapishwa, chama cha siasa kinachomdhamini mwanachama husika, kitaitaarifu Tume kwa maandishi na Tume, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali itateua siku nyingine ya uteuzi wa mgombea kwa mujibu wa kifungu cha 61.

(3) Tume yaweza kusitisha mchakato wa uchaguzi pale itakapobainika kuwa kuna ukiukwaji wa Sheria na taratibu za uchaguzi, na ndani ya siku thelathini itatangaza siku nyingine ya uchaguzi.

Utunzaji wa nyaraka

**107**.-(1) Msimamizi wa uchaguzi atahakikisha anatunza kwa usalama nyaraka zote zinazohusu uendeshaji wa uchaguzi.

(2) Tume itahakikisha inatunza kwa usalama nyaraka zote zinazohusu uendeshaji wa uchaguzi zilizowasilishwa kwake chini ya masharti ya Sheria hii.

(3) Msimamizi wa uchaguzi na Tume watahakikisha nyaraka zote ambazo kifungu hiki kinatumika, zinateketezwa baada ya kupita kipindi cha miezi sita toka siku ya uchaguzi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo kwa amri ya Mahakama ya wilaya au Mahakama Kuu itakayotolewa kutokana na mwenendo wa mashauri ya uchaguzi ya udiwani au ubunge mtawalia.

Mamlaka ya wasimamizi wasaidizi wa vituo

**108**. Msimamizi msaidizi wa kituo anaweza kuruhusiwa na msimamizi wa kituo kufanya jambo lolote au kitu chochote ambacho msimamizi wa kituo ametakiwa kufanya au ameruhusiwa kufanya katika kituo cha kupigia kura na Sheria hii, isipokuwa hawezi kutoa amri ya kukamatwa mtu yeyote, au kumtenga au kumuondoa mtu yeyote katika kituo cha kupigia kura.

Mamlaka ya wagombea

**109**. Mgombea anaweza kutenda kitendo chochote au kitu chochote ambacho wakala wa upigaji kura ameidhinishwa au ametakiwa kufanya, na anaweza kumsaidia wakala wa upigaji kura au wakala wa kuhesabu kura kufanya kitendo au kitu hicho.

Kutokuwepo kwa mawakala hakutabatilisha mwenendo

**110**. Endapo katika Sheria hii, kitendo chochote au kitu chochote kimetakiwa au kimeidhinishwa kufanyika mbele ya wakala wa upigaji kura au wakala wa kuhesabu kura au mgombea, kutokuwepo kwa mawakala hao au mgombea kwa muda na mahali palipopangwa kwa ajili hiyo, kama kitendo au kitu hicho kimefanywa kwa usahihi, hakutabatilisha kitu au kitendo kilichofanywa.

Chaguzi zinazofanyika kwa wakati mmoja

**111**. Endapo katika eneo la uchaguzi inatokea siku moja inapangwa kuwa siku ya uchaguzi unaoshindaniwa wa Rais, Wabunge na Madiwani-

(a) upigaji kura katika chaguzi tatu, utafanyika kwa pamoja katika vituo vyote vya kupigia kura katika eneo hilo;

(b) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa masanduku ya kura yaliyotenganishwa na yanayotofautiana na kila msimamizi wa kituo ataandaa na kusimamia kituo chake cha kupigia kura na ataweka masanduku ya kupigia kura kwa utaratibu ambao utaepuka mkanganyiko wowote unaoweza kutokea kwa sababu ya upigaji kura wa chaguzi tofauti zinazofanyika kwa pamoja:

Isipokuwa kwamba, kwa kuzingatia maelekezo yoyote ya Tume kwa ajili hiyo,

sanduku moja la kura linaweza kutolewa kwa kila kituo cha kupigia kura kwa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani;

(c) karatasi za kura kwa chaguzi hizo zitakuwa na rangi tofauti ili kuzitofautisha kwa urahisi;

(d) mpiga kura ambaye ataondoka katika kituo cha kupigia kura baada ya kupiga kura katika mojawapo ya chaguzi hataruhusiwa kuingia tena katika kituo hicho cha kupigia kura kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi mwingine;

(e) matakwa ya aya (c) yatachukuliwa kuwa yamezingatiwa katika chaguzi zote endapo taarifa zilizoainishwa katika aya hiyo zitaitishwa mapema iwezekanavyo kabla ya kumpa mpiga kura karatasi ya kura kwa uchaguzi wowote ambao alipewa kwanza; na

(f) kuhesabu kura kwa chaguzi hizo tatu kutafanyika kwa kutenganishwa.

## SEHEMU YA SITA
## UTEUZI WA WABUNGE NA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUMU

Uteuzi wa wabunge wanawake wa viti maalumu

**112**.-(1) Kutakuwa na Wabunge wanawake wa viti maalumu katika Bunge kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 66 ya Katiba.

(2) Chama cha siasa kinachogombea katika uchaguzi wa Wabunge utakaofanyika baada ya kuvunjwa kwa Bunge kinaweza kupendekeza na kuwasilisha kwa Tume majina ya wagombea wanawake wenye sifa kwa ajili ya uteuzi wa viti maalum vya wanawake si chini ya siku thelathini kabla ya siku ya uchaguzi.

(3) Tume itaainisha idadi ya wagombea wanawake watakaoteuliwa na kila chama cha siasa.

(4) Majina ya wanawake wagombea waliopendekezwa kwa Tume yatakuwa katika mpangilio kwa kuzingatia kipaumbele.

(5) Kila mwanamke mgombea aliyependekezwa kwa Tume atatakiwa kujaza fomu ya uteuzi.

(6) Masharti ya Ibara ya 67 ya Katiba yatatumika

kwa kila mwanamke ambaye amedhaminiwa na chama cha siasa.

(7) Kwa kuzingatia Ibara ya 66, 67 na 78 za Katiba na kwa mujibu wa mpangilio wa kipaumbele uliooneshwa katika orodha iliyopendekezwa na kila chama cha siasa, Tume itateua na kutangaza idadi ya wanawake wagombea kutoka katika vyama vya siasa vinavyohusika kuwa Wabunge Wanawake Viti Maalum.

(8) Tume itatuma taarifa ya uteuzi kwa Spika wa Bunge na kwa Makatibu Wakuu wa vyama vya siasa vinavyohusika.

(9) Orodha ya majina ya wanawake wagombea waliopendekezwa kwa Tume kwa mujibu wa Ibara ya 78(4) ya Katiba na kila chama cha siasa kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu, kwa kuzingatia Ibara ya 76(3) ya Katiba, itakuwa ndio orodha itakayotumiwa na Tume kwa madhumuni ya kujaza nafasi wazi ya ofisi ya Mbunge wa viti maalum vya wanawake wakati wa kipindi chote cha uhai wa Bunge:

Isipokuwa kwamba, inapotokea orodha ya majina iliyowasilishwa Tume imemalizika, Tume itakitaka chama husika kuwasilisha orodha ya nyongeza ya majina ya wagombea wanawake viti maalumu wanaopendekezwa kwa ajili ya uteuzi.

Uteuzi wa madiwani wanawake viti maalumu
Sura ya 287 na 288

**113.**-(1) Kutakuwa na viti maalumu vya wanawake katika Mamlaka ya Serikali za Mitaaa kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji).

(2) Kila chama cha siasa ambacho kitagombea uchaguzi wa udiwani katika uchaguzi mkuu, chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ndani ya Halmashauri, kinaweza kupendekeza kwa Tume, majina ya wanawake ambao wana sifa za kuteuliwa kuwa wagombea wa viti maalumu vya wanawake.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) au kadri itakavyokuwa, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Tume

itaainisha idadi ya wagombea wanawake watakaoteuliwa na kila chama cha siasa.

(4) Kila chama cha siasa kinachowadhamini wagombea wanawake katika uchaguzi kitapendekeza kwa Tume orodha ya wagombea si chini ya siku thelatihini kabla ya siku ya uchaguzi.

(5) Orodha ya majina ya wanawake wanaopendekezwa kwa Tume yatakuwa katika mpangilio wa kipaumbele.

(6) Kila mwanamke mgombea aliyependekezwa kwa Tume atatakiwa kujaza fomu ya uteuzi.

(7) Masharti ya kifungu cha 58 yatatumika kwa kila mwanamke aliyedhaminiwa na chama cha siasa kuwa mgombea.

Sura ya 287 na Sura ya 288

(8) Kwa mujibu wa kifungu cha 58, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) na kwa mujibu wa mpangilio wa kipaumbele ulioainishwa katika orodha iliyopendekezwa na kila chama cha siasa, Tume itatangaza idadi ya wanawake wagombea kutoka katika vyama vya siasa vinavyohusika ambao watachaguliwa kuwa Madiwani Wanawake Viti Maalumu.

(9) Tume itapeleka taarifa ya uteuzi kwa Halmashauri na Makatibu Wakuu wa vyama vya siasa vinavyohusika.

(10) Orodha ya majina ya wanawake wagombea waliopendekezwa kwa Tume na kila chama cha siasa wakati wa uchaguzi mkuu itakuwa ndio orodha itakayotumiwa na Tume kwa madhumuni ya kujaza nafasi wazi ya ofisi ya Diwani wa viti maalum wanawake wakati wa kipindi chote cha miaka mitano baada ya uchaguzi mkuu:

Isipokuwa kwamba, inapotokea orodha ya majina iliyowasilishwa kwa Tume imemalizika, Tume itakitaka chama husika kuwasilisha orodha ya nyongeza ya majina ya wagombea wanawake viti maalum wanaopendekezwa kwa ajili ya uteuzi.

## SURA YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

SEHEMU YA KWANZA
MAKOSA YANAYOHUSU UANDIKISHAJI NA UTEUZI

Makosa yanayohusu uandikishaji

**114**.-(1) Mtu ambaye-

(a) kwa madhumuni ya kutaka kuandikishwa yeye mwenyewe au mtu mwingine yeyote au kupata kadi ya mpiga kura, kutoka kwa afisa mwandikishaji au kutoka kwa mtu mwingine yeyote ambaye ana wajibu juu ya maombi ya kuandikishwa au kutoa kadi ya mpiga kura, atatoa taarifa yoyote ya uongo kuhusu ombi lake mwenyewe au kwa niaba ya mtu mwingine kuandikishwa au kupewa kadi ya mpiga kura;

(b) kwa kujua au akiwa na sababu ya kuamini kuwa ameandikishwa katika eneo la uchaguzi, anaomba kuandikishwa bila kuzingatia matakwa ya kifungu cha 25, na bila kueleza kwa afisa mwandikishaji kuhusu uandikishwaji wake wa awali katika eneo lingine la uchaguzi;

(c) anaomba kuandikishwa katika eneo la uchaguzi wakati ameshaomba kuandikishwa katika eneo lingine la uchaguzi na maombi yake ya awali hayajaamuliwa kwa kusubiri uchunguzi wowote kuhusu sifa za mwombaji au kuondolewa;

(d) baada ya kupewa kadi ya mpiga kura, anaomba kupewa yeye binafsi kadi mpya ya mpiga kura kinyume cha mazingira yaliyowekwa katika kifungu cha 19, 20 au 21 na bila kueleza kwa afisa mwandikishaji mazingira ambayo maombi yamefanywa au ambayo haamini kwamba ni ya kweli kulingana na hali halisi;

(e) kwa kujua, anatoa tamko lolote lililoainishwa katika kifungu cha 22 ambalo ni la uongo, au ambalo haamini kuwa ni la kweli kulingana na hali halisi,

(f) ananunua au anaiba kadi yoyote ya mpiga kura ili aonekane kuwa ni mpiga kura aliyeandikishwa kihalali; au

(g) ananunua, anauza, anaiba, anafuta au kwa namna yoyote anaharibu kadi ya mpiga kura ili kumzuia mpiga kura yeyote asimpigie kura mgombea wa chama fulani cha siasa au kwa madhumuni ya kufanya kura nyingi zaidi zipigwe kwa mgombea wa chama fulani cha siasa,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu ambaye jina lake limefutwa katika Daftari na ametakiwa na afisa mwandikishaji kurudisha kadi ya mpiga kura iliyotolewa kwake au kutoa na kuwasilisha kwa afisa mwandikishaji tamko lililoainishwa katika kifungu cha 22 katika muda ulioainishwa na afisa mwandikishaji bila sababu za msingi, ama harudishi kadi hiyo wala hatoi na kuwasilisha tamko hilo katika muda uliaonishwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki moja au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(3) Mtu ambaye kwa namna yoyote anamzuia au anajaribu kumzuia msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi katika kutekeleza majukumu yake au kutekeleza mamlaka yake chini ya Sheria hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu.

Kutumia wadhifa kushawishi watu wengine ili wasiombe kuteuliwa

**115**.-(1) Mtu mwenye madaraka katika ofisi au mwenye dhamana katika ofisi ambaye, katika kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo au wadhifa huo, anatoa maelezo yoyote au anafanya kitendo chochote kwa nia ya kumkatisha tamaa mtu mwingine yeyote kuomba kuteuliwa chini ya Sheria hii au anamshawishi mtu yeyote ambaye ameteuliwa kujitoa ugombea wake, anatenda

kosa, na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(2) Mashtaka hayatafunguliwa dhidi ya mtu yeyote kwa kosa lolote kinyume na kifungu hiki bila ya kupata idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

(3) Katika kifungu hiki "ofisi" na "wadhifa" ina maana na inajumuisha ofisi katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano na ofisi nyingine yoyote au wadhifa ambao aliyeshika ana nafasi yenye ushawishi kwa mgombea fulani au mgombea mtarajiwa.

Mwenendo usiofaa wa mtendaji wa uchaguzi

**116**.-(1) Mtendaji wa uchaguzi ambaye kwa kujua au kwa makusudi anafanya au anaacha kufanya kitu chochote kinachohusu mchakato wa uchaguzi na kikasababisha matokeo ya uchaguzi kubatilishwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Endapo katika shauri la uchaguzi Mahakama inaamua kwamba mtendaji wa uchaguzi amefanya au ameacha kufanya kitu chochote kuhusu mchakato wa uchaguzi ambacho kimesababisha kuharibika kwa mchakato wa uchaguzi, Mahakama itathibitisha uamuzi huo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(3) Endapo shtaka limefunguliwa kwa kosa lililo chini ya kifungu hiki, hati iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) itakuwa ni uthibitisho wa mwisho wa kile kilichomo ndani yake.

(4) Kwa madhumuni ya kuondoa shaka, hati iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) haitazuia upande wa mashtaka kuitisha ushahidi zaidi ili kuthibitisha shtaka.

Sura ya 20
Sura ya 6

(5) Masharti ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai au Sheria ya Ushahidi yatatumika kwa kuzingatia maboresho yatakayohitajika katika uendeshaji wa kesi itakayofunguliwa chini ya kifungu hiki.

Kufidia hasara
Sura ya 76

**117**. Bila kujali masharti ya kifungu cha 116, masharti ya Sheria ya Urejeshaji wa Madeni ya Maafisa wa Umma yatatumika kwa kuzingatia maboresho yatakayohitajika kwa mtendaji wa uchaguzi ambaye ameisababishia Serikali hasara, gharama au uharibifu kutokana na kutenda au kutokutenda kwake katika mchakato wa uchaguzi.

Tafsiri ya mtendaji wa uchaguzi

**118**. Kwa madhumuni ya kifungu cha 116 na 117, mtendaji wa uchaguzi inajumuisha mratibu wa uchaguzi wa Mkoa, msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi, afisa anayeshughulikia uchaguzi, msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo na mtu mwingine yeyote atakayeteuliwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Tume.

Makosa yanayohusu Daftari na kadi ya mpiga kura

**119**.-(1) Mtu ambaye-

(a) anaghushi au kwa udanganyifu anafuta au anaharibu Daftari lolote la wapiga kura; au

(b) anaghushi, anatengeneza au kwa udanganyifu anaharibu kadi yoyote ya mpiga kura au nakala rasmi ya kadi ya mpiga kura au alama yoyote rasmi katika kadi ya mpiga kura,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka minne au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu ambaye anamiliki au anayo katika himaya yake kadi yoyote ya mpiga kura ambayo imetolewa kwa mtu mwingine yeyote na ambaye anakataa au anazembea bila sababu ya msingi kurudisha kadi hiyo kwa mtu ambaye alipewa, itakapohitajika na mtu huyo au afisa mwandikishaji, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Mwenendo usiofaa wa

**120**.-(1) Afisa mwandikishaji yeyote ambaye kwa

maafisa waandikishaji

kujua anafanya au anaacha kufanya kitu chochote kuhusu uandikishaji na hivyo kuvuruga mchakato wa uandikishaji, anatenda kosa na akitiwa hatiani-

(a) ikiwa ni afisa aliyeainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2)(a), atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili, au vyote kwa pamoja;

(b) ikiwa ni afisa aliyeainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2)(b), atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, afisa mwandikishaji inajumuisha-

(a) afisa mwandikishaji na afisa mwandikishaji msadizi; na

(b) mwandishi msaidizi.

Makosa yanayohusu fomu za uteuzi au karatasi za kura

**121**.-(1) Mtu ambaye-

(a) anaghushi au kwa udanganyifu anafuta au anaharibu fomu ya uteuzi au karatasi ya kura au anawasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi fomu ya uteuzi akijua kuwa fomu hiyo imeghushiwa;

(b) anaghushi au anatengeneza au kwa udanganyifu anaharibu karatasi yoyote ya kura au alama rasmi katika karatasi yoyote ya kura;

(c) akiwa ni msimamizi wa uchaguzi au msimamizi wa kituo kwa kujua au kwa uzembe, anashindwa kuweka alama rasmi katika karatasi ya kura;

(d) bila ya kuwa na mamlaka stahiki, anasambaza karatasi za kura kwa mtu yeyote;

(e) kwa udanganyifu anaweka ndani ya sanduku la kura karatasi yoyote tofauti na karatasi ya kura iliyoidhinishwa kisheria kuwekwa humo;

(f) bila ya kuwa na mamlaka stahiki, anatoa nje

ya kituo chochote cha kupigia kura karatasi ya kura au anakutwa na karatasi ya kura nje ya kituo cha kupigia kura; au

(g) bila kuwa na mamlaka stahiki, anaharibu, anachukua, anafungua au vinginevyo anazuia sanduku la kura au kifurushi cha karatasi za kura kinachotumika kwa ajili ya uchaguzi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu ambaye kwa madhumuni ya kuteuliwa yeye mwenyewe au mtu mwingine yeyote, kuwa mgombea, kwa kujua, anatoa maelezo ya uongo kuhusu uteuzi katika fomu ya uteuzi, fomu ya maelezo binafsi au tamko la kisheria lililowasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(3) Katika shtaka lolote kuhusu kosa linalohusiana na fomu ya uteuzi, sanduku la kura, kishina cha karatasi ya kura, vifaa vya kuwekea alama na vitu vingine vinavyotumika katika uchaguzi, vitu vilivyomo katika karatasi hizo, masanduku, zana na vitu vinaweza kuelezwa kuwa katika miliki ya msimamizi wa uchaguzi kwa uchaguzi huo.

Matangazo ya uongo ya kujitoa

**122**. Mtu ambaye kwa kujua, kwa kutamka, kuchapisha au kutangaza, anatangaza maelezo yoyote ya kujitoa kwa mgombea yeyote kwa madhumuni ya kumsaidia mgombea mwingine kushinda uchaguzi, anatenda kosa la kitendo haramu na akitiwa hatiani atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Vishawishi vya rushwa kwa ajili ya kujitoa

**123**. Mtu atakayemshawishi au kumsababishia mtu mwingine kujitoa kuwa mgombea katika uchaguzi kwa malipo au kwa ahadi ya malipo na mtu yeyote ambaye atajitoa kutokana na vishawishi au ahadi hizo,

anatenda kosa la kitendo cha rushwa na iwapo atatiwa hatiani atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

## SEHEMU YA PILI
## MAKOSA MENGINEYO YA UCHAGUZI

Makosa mengineyo

**124**. Mtu ambaye kwa kukusudia anatoa ushahidi wa uongo au anatoa maelezo ya uongo katika tamko lililotolewa chini ya kifungu cha 87, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Utunzaji siri katika chaguzi

**125**.-(1) Kila afisa, karani, mkalimani, mgombea na wakala aliyeidhinishwa kuwepo kwenye kituo cha kupigia kura au wakati wa kuhesabu kura, isipokuwa kama ameapa kiapo cha kutunza siri chini ya masharti mengine yoyote ya Sheria hii, kabla ya kuhudhuria, atapaswa kuapa kiapo cha kutunza siri kwa namna iliyoainishwa.

(2) Msimamizi wa uchaguzi atakuwa na mamlaka ya kusimamia viapo vyote vinavyotakiwa kutolewa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Kila afisa, karani, mkalimani, mgombea na wakala atakayekuwepo katika kituo cha kupigia kura, atatunza na kusaidia kutunza siri ya upigaji kura katika kituo hicho na hatatoa kwa mtu yeyote, isipokuwa kwa madhumuni yaliyoidhinishwa kisheria, taarifa yoyote kuhusu jina au namba ya mpiga kura aliyeomba au ambaye hajaomba karatasi ya kura au aliyepiga kura katika kituo au kuhusu alama rasmi.

(4) Afisa, karani, mkalimani, mgombea, wakala au mtu mwingine yeyote, hatapata au kujaribu kupata katika kituo cha kupigia kura taarifa za mgombea kutoka kwa mtu yeyote aliye katika kituo hicho ambaye anakaribia kupiga kura au ameshapiga kura, au kufanya mawasiliano muda wowote na mtu yeyote, kuhusu taarifa zozote zilizopatikana katika kituo cha kupigia kura kuhusu

mgombea ambaye mtu yeyote katika kituo hicho anakusudia kumpigia au amempigia kura.

(5) Kila afisa, karani, mkalimani, mgombea au wakala ambaye atakuwepo wakati wa kuhesabu kura atatunza na kusaidia utunzaji wa siri za upigaji kura na hatathibitisha au kutoa taarifa yoyote aliyoipata wakati wa kuhesabu kura kwa mgombea ambaye kura yoyote imepigwa kwake na karatasi yoyote ya kura.

(6) Mtu isipokuwa msimamizi wa kituo anayehudumu kwa madhumuni yaliyoainishwa na Sheria hii, au mtu anayemsaidia mtu asiyeweza kupiga kura na anayehudumu kwa madhumuni hayo, hatawasiliana au kujaribu kuwasiliana na mtu yeyote baada ya mtu huyo kupokea karatasi ya kura na kabla hajaweka karatasi hiyo ndani ya sanduku la kura.

(7) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Adhabu ya hongo, takrima, n.k

Sura ya 329

**126**. Mtu ambaye atatenda kosa la kutoa hongo, takrima au kurubuni, anatenda kosa la kitendo cha rushwa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Adhabu ya kujifanya mtu mwingine

Sura ya 16

**127**. Mtu anayetenda kosa la kujifanya mtu mwingine au kusaidia kufanya kosa hilo, kushiriki kutenda kosa, kushauri au kuwezesha kutendeka kwa kosa la kujifanya mtu mwingine anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika Sheria ya Kanuni za Adhabu.

Kupoteza sifa kwa kuhukumiwa kwa kosa la kitendo cha rushwa au kitendo haramu

**128**. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kitendo cha rushwa au kitendo haramu na ambaye hukumu yake haijatenguliwa na mahakama yenye mamlaka pamoja na adhabu nyingine yoyote, atapoteza sifa ya kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa kipindi cha miaka mitano tangu tarehe aliyopatikana na hatia na hataweza kuandikishwa

kuwa mpiga kura au kupiga kura katika uchaguzi wowote chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote.

Watu wanaodaiwa kuwa na hatia ya ushawishi mbaya

**129**. Mtu ambaye kwa dhahiri au kwa kificho, yeye mwenyewe au mtu mwingine kwa niaba yake, atakayetumia au kutishia kutumia nguvu, vurugu au kizuizi, au akasababisha au akatishia kusababisha yeye mwenyewe au mtu mwingine yeyote, jeraha la mwili au la kiroho, uharibifu, madhara, au hasara kwa au dhidi ya mpiga kura yeyote, kwa ajili ya kumshawishi au kumlazimisha mpiga kura huyo kupiga kura au kuacha kupiga kura, au ikiwa mpiga kura huyo amepiga kura au ameacha kupiga kura katika uchaguzi wowote au ambaye, kwa kumteka nyara, vitisho au hila ya aina yoyote, kumkwamisha au kumzuia kutumia uhuru wa kupiga kura mpiga kura yeyote ama kupiga au kuacha kupiga kura katika uchaguzi wowote, atakuwa ametenda kosa la ushawishi mbaya kwa maana ya Sheria hii.

Hongo, rushwa na ushawishi mbaya kwa wajumbe na maafisa wa Tume

**130**. Endapo mtu yeyote anatenda kitendo chochote ambacho ni hongo, rushwa au ushawishi mbaya kwa mjumbe au afisa wa Tume aliyerejewa katika Sheria hii kwa nia ya kwamba mjumbe au afisa, kadri itakavyokuwa, afanye ubaguzi kwa kumpendelea mgombea mmoja au wagombea wengine katika uchaguzi, au pale ambapo mjumbe huyo au afisa anatenda kitendo hicho kwa nia ya kubagua au baada ya kubagua ili kumpendelea mgombea mmoja au wengine, mtu huyo atachukuliwa, kwa mujibu wa mazingira ya kesi, kuwa ametenda kosa la rushwa, hongo au ushawishi mbaya.

Watu wanaochukuliwa kuwa na hatia ya kujifanya watu wengine

**131**. Mtu ambaye katika uchaguzi wowote-

(a) anaomba karatasi ya kura kwa jina la mtu mwingine au kwa kujua anapiga kura kwa jina la mtu mwingine, iwe jina hilo ni jina la mtu anayeishi au amefariki au mtu wa kufikirika; au

(b) kwa madhumuni ya kupewa yeye mwenyewe karatasi ya kura, akiwa anafahamu, anatoa kadi ya mpiga kura iliyotolewa kwa mtu

mwingine,

anatenda kosa la kujifanya mtu mwingine kwa maana ya Sheria hii.

Adhabu kwa watu wenye hatia ya vitendo vya rushwa na vitendo haramu

**132**.-(1) Mtu ambaye-

(a) anapiga au anajaribu kupiga kura, au anashawishi au anamtumia mtu mwingine kupiga kura katika uchaguzi wowote akiwa yeye, au kwa kufahamu kuwa mtu huyo mwingine ameshapiga kura katika uchaguzi huo au ikiwa ni uchaguzi mkuu, katika uchaguzi mwingine wowote uliofanyika wakati wa uchaguzi mkuu; au

(b) kwa madhumuni ya kuwezesha kutolewa kwa karatasi yoyote ya kura kwa mtu mwingine yeyote au yeye mwenyewe, anatoa kadi yoyote ya mpiga kura iliyotolewa kwake au mtu mwingine wa tatu kwa mtu huyo mwingine au anashawishi, au anamwezesha mtu wa tatu kutoa kadi ya mtu huyo wa tatu kwa yeye mwenyewe au mtu huyo mwingine,

anatenda kosa la kitendo cha rushwa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Sura ya 329

(2) Mtu ambaye-

(a) anapiga kura au anamshawishi mtu mwingine kupiga kura katika uchaguzi wowote huku akijua kwamba yeye mwenyewe au mtu huyo mwingine hastahili kupiga kura au amekatazwa na Sheria hii au sheria nyingine yoyote kupiga kura katika uchaguzi huo; au

(b) kwa madhumuni ya kujipatia karatasi ya kura huku akijua anatoa kadi batili ya mpiga kura,

anatenda kosa la kitendo haramu na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki mbili au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Kuingilia mikutano halali ya hadhara kuwa

**133**. Mtu ambaye, katika mkutano halali wa hadhara unaofanyika kwa ajili ya uchaguzi wa mtu yeyote

ni kitendo haramu

kati ya siku ya kutoa notisi ya siku ya uteuzi na siku ambayo matokeo ya uchaguzi yatatangazwa, anafanya au anachochea wengine kufanya vurugu kwa madhumuni ya kuzuia shughuli ambazo zimepangwa kufanyika katika mkutano ulioitishwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki mbili au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Katazo la kufanya mikutano siku ya uchaguzi na kuonesha nembo eneo la karibu na kituo cha kupigia kura siku ya uchaguzi

**134**.-(1) Mtu hatafanya mkutano siku ya kupiga kura au ndani ya jengo au eneo lolote ambamo upigaji kura katika uchaguzi unaendelea, au mahali popote ndani ya eneo la mita mia tatu ya eneo au jengo hilo, hatavaa au kuonesha kadi, picha au nembo nyingine yoyote inayoonesha kuunga mkono mgombea fulani katika uchaguzi.

(2) Mtu anayekiuka kifungu hiki anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki moja.

Kuchafua matangazo

**135**. Mtu ambaye bila ya mamlaka halali, anaharibu, anakata, anachafua au anaondoa tangazo lolote ambalo limewekwa kwa mujibu wa Sheria hii au nyaraka yoyote ambayo imewekwa kwa ajili ya ukaguzi kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini na isiyozidi shilingi laki moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Nyaraka kuwa na jina na anwani ya mpiga chapa na mchapishaji

**136**.-(1) Mtu-

(a) hatachapa au kuchapisha au kuwezesha kuchapa au kuchapishwa tangazo lolote, bango au kipeperushi kinachohusiana na uchaguzi au nyaraka yoyote iliyochapishwa na kusambazwa kwa madhumuni ya kumtangaza na kumwezesha mgombea kuchaguliwa;

(b) hatabandika au kuwezesha kubandikwa kwa tangazo lolote, bango au vipeperushi; au

(c) hatasambaza au kuwezesha kusambazwa nyaraka yoyote iliyochapwa kwa madhumuni yaliyoainishwa katika aya (a),

isipokuwa bango, tangazo, kipeperushi au nyaraka katika sehemu ya mbele zina jina na anwani ya mpigachapa na mchapishaji na-

(i) ikiwa ni uchaguzi wa kiti cha Rais, tangazo hilo, bango, kipeperushi au nyaraka ziwe zimeidhinishwa na Tume;

(ii) ikiwa ni uchaguzi wa wabunge au madiwani, tangazo hilo, bango, kipeperushi au nyaraka ziwe zimeidhinishwa na msimamizi wa uchaguzi.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, zoezi la kudurufu nakala za nyaraka tofauti na kunakili nyaraka hizo kwa mkono, kutachukuliwa kuwa ni kuchapa na neno “mpigachapa” litatafsiriwa ipasavyo.

(3) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini na isiyozidi shilingi laki moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

(4) Masharti ya kifungu hiki hayatatumika kwa tangazo, bango, kipeperushi au nyaraka zilizochapishwa na au kwa niaba ya Tume au msimamizi wa uchaguzi.

## SURA YA NANE
## KUPINGA MATOKEO YA UCHAGUZI KWA NJIA YA SHAURI LA UCHAGUZI

### SEHEMU YA KWANZA
### SHAURI LA UCHAGUZI KUPINGA MATOKEO YA UBUNGE

Kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya shauri la uchaguzi

**137**.-(1) Kwa mujibu wa ukomo uliowekwa na Ibara ya 41(7) ya Katiba, masharti ya kifungu hiki yatatumika kwa uchaguzi wa Mbunge.

(2) Uchaguzi wa Mbunge utatangazwa kuwa batili

kwa shauri la uchaguzi na si kwa sababu nyingine isipokuwa mojawapo ya sababu zifuatazo zimethibitishwa kwa kiwango cha kuiridhisha Mahakama Kuu:

(a) kwamba, wakati wa kampeni za uchaguzi, maelezo yaliyotolewa na mgombea, au kwa niaba yake na kwa ufahamu wake na ridhaa au idhini yake, kwa nia ya kutumia hoja za ukabila, rangi au udini au tofauti zinazohusu uchaguzi au kuhusu yeyote kati ya wagombea au iwapo wagombea si wa jinsi moja, kwa nia ya kutumia tofauti hizo;

(b) kutozingatia masharti ya Sheria hii kuhusu uchaguzi, iwapo itajitokeza kuwa uchaguzi haukufanyika kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika masharti hayo na kuwa kutozingatia huko kumeathiri matokeo ya uchaguzi; au

(c) kwamba mgombea wakati wa kuchaguliwa kwake hakuwa mtu mwenye sifa ya kuchaguliwa kama Mbunge.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2), pale ambapo wakati wa usikilizaji wa shauri la uchaguzi kuhusu uchaguzi chini ya Sheria hii, Mahakama Kuu ikibaini kuwa kitendo cha rushwa au kitendo haramu kuhusu uchaguzi kimetendwa na au kwa ufahamu na ridhaa au idhini ya wakala yeyote wa mgombea na Mahakama Kuu ikibaini zaidi, baada ya kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwakilishi wake nafasi ya kusikilizwa, kwamba mgombea ameithibitishia Mahakama Kuu-

(a) kwamba, hakuna kitendo cha rushwa au kitendo haramu kilichotendwa na mgombea mwenyewe au kwa ufahamu na ridhaa au idhini ya mgombea huyo;

(b) kwamba mgombea alichukua hatua zote zinazostahili kuzuia kufanyika kwa kitendo chochote cha rushwa au kitendo haramu katika uchaguzi huo; na

(c) kwamba kwa hali nyingine yoyote uchaguzi haukuwa na kitendo cha rushwa au kitendo haramu kwa upande wa mgombea na wakala wake,

ikiwa Mahakama Kuu itaamua hivyo, kuchaguliwa kwa

mgombea huyo hakutakuwa batili kwa sababu ya kitendo chochote.

Makosa yanayotendwa na watendaji wa uchaguzi

**138**. Endapo katika uchaguzi imethibitika kuwa kosa lolote la hongo, takrima, kitendo cha rushwa au kitendo haramu lilitendwa kwa kujua au kuendelezwa na mjumbe au afisa wa Tume au na mtu anayetekeleza majukumu kwa maelekezo ya Tume, mjumbe au afisa au mtu huyo mwingine akitiwa hatiani atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU NA MAMLAKA YA MAHAKAMA KUU

Mashauri yanayosikilizwa na Mahakama Kuu

**139**.-(1) Kila shauri la uchaguzi wa ubunge litasikilizwa na kuamuliwa na Mahakama Kuu, ambayo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii itajulikana kama "Mahakama".

(2) Mashahidi wataitwa na kuapishwa kwa namna ambayo mazingira yataruhusu kama ilivyo katika shauri la mahakama inapotekeleza mamlaka yake ya mwanzo ya kuendesha mashauri ya madai na, bila ya kuathiri masharti ya sheria nyingine yoyote, watawajibishwa kwa adhabu sawa na ile ya kutoa ushahidi wa uongo au kutohudhuria.

(3) Wakati wa usikilizaji wa shauri la uchaguzi chini ya Sheria hii, Mahakama kwa amri, inaweza kumuamuru mtu yeyote ambaye anaonekana kuhusika katika uchaguzi ambao unatajwa katika shauri kuhudhuria kama shahidi, na mtu yeyote atakayekataa kutii amri hiyo anatenda kosa la kuidharau mahakama na mahakama inaweza kumhoji shahidi yeyote ambaye ameamriwa kuhudhuria au mdaawa yeyote katika shauri na baada ya kuhojiwa na mahakama, shahidi huyo anaweza kudodoswa na au kwa niaba ya mlalamikaji, mlalamikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwakilishi wake, kama yupo, au mtu yeyote kati yao.

(4) Wakati wa usikilizaji wa shauri la uchaguzi, Mahakama itakuwa na mamlaka ya kumuamuru mtu yeyote ambaye anaonekana na Mahakama kuwa

amehusika au kushiriki katika uchaguzi unaolalamikiwa au ambaye ushahidi wake unaweza kuisaidia Mahakama kufikia uamuzi wa haki na wa usawa katika shauri lililo mbele yake kuhudhuria kama shahidi.

Shauri na taratibu za kuweka dhamana ya gharama

**140**.-(1) Shauri la uchaguzi linaweza kuwasilishwa na mmoja au zaidi ya watu wafuatao-

(a) mtu aliyepiga kura kihalali au alikuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi ambao shauri linahusika;

(b) mtu anayedai kuwa alikuwa na haki ya kuteuliwa au kuchaguliwa katika uchaguzi huo;

(c) mtu anayedai kuwa alikuwa mgombea katika uchaguzi huo; au

(d) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(2) Msajili wa Mahakama hatapanga tarehe ya kusikilizwa kwa shauri lolote la uchaguzi isipokuwa kama mlalamikaji amelipa mahakamani, dhamana ya gharama, kiasi kisichozidi shilingi milioni tano kwa kila mlalamikiwa.

(3) Mlalamikaji atatakiwa ndani ya siku kumi na nne baada ya kuwasilisha shauri, kuwasilisha maombi kwa ajili ya uamuzi wa kiasi kitakacholipwa kama dhamana ya gharama, na mahakama itaamua maombi hayo ndani ya siku kumi na nne zinazofuata baada ya tarehe ya kuwasilisha maombi kwa ajili ya uamuzi wa kiasi kitakacholipwa kama dhamana ya gharama.

(4) Endapo mtu yeyote ataunganishwa kama mlalamikiwa kwa mujibu wa amri ya mahakama, mlalamikaji, ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ambayo amri ilitolewa ikielekeza mtu huyo aunganishwe kuwa mlalamikiwa, atalipa mahakamani kiasi kingine kisichozidi shilingi milioni tatu, kama itakavyoelekezwa na mahakama kuhusu mtu huyo.

(5) Endapo kwa maombi yatakayofanywa na mlalamikaji, mahakama itaridhika kuwa utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) au (4) utasababisha ugumu kwa mlalamikaji, inaweza kuelekeza kuwa-

(a) mlalamikaji atoe aina nyingine ya dhamana

ambayo thamani yake haizidi shilingi milioni tano kama ambavyo mahakama itaona inafaa; au

(b) mlalamikaji asamehewe kulipa aina yoyote ya dhamana ya gharama.

(6) Hakuna amri itakayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3), (4) na (5) mpaka nafasi imetolewa kwa mlalamikiwa, au, iwapo kuna walalamikiwa wawili au zaidi, kwa kila mlalamikiwa kujieleza kwa madhumuni hayo.

(7) Endapo dhamana ya gharama haitalipwa mahakamani ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya uamuzi wa mahakama kuhusu kiasi cha malipo ya dhamana ya gharama, hakuna mwenendo wa shauri la uchaguzi utakaoendelea kusikilizwa na shauri hilo litafutwa.

(8) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) hayatatumika kwa namna yoyote ile ikiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mlalamikaji au mmoja wa walalamikaji.

(9) Kiasi cha fedha kilichowekwa kama dhamana ya gharama au salio la dhamana hiyo, iwapo mlalamikaji atashinda katika shauri au rufaa na iwapo hakuna amri iliyotolewa dhidi ya mlalamikaji kulipa gharama, kitarejeshwa kwa mlalamikaji mapema iwezekanavyo.

Nafuu zinazoweza kuombwa

**141**. Katika kuwasilisha shauri la uchaguzi, mlalamikaji anaweza kuomba nafuu zote au yoyote kati ya nafuu zifuatazo anazoweza kustahili:

(a) tamko kwamba uchaguzi ni batili;

(b) tamko kwamba uteuzi wa mtu aliyechaguliwa haukuwa halali; au

(c) endapo kiti kinadaiwa na mgombea ambaye hakushinda kwa madai kwamba alikuwa amepata kura nyingi halali, kufanyika kwa uchunguzi wa kura.

Uthibitisho wa uhalali wa uchaguzi

**142**.-(1) Mahakama, wakati wa kuhitimisha shauri au rufaa ya shauri la uchaguzi, itaamua iwapo Mbunge ambaye uteuzi au uchaguzi wake unalalamikiwa, au mtu

mwingine yeyote aliteuliwa au alichaguliwa ipasavyo, au uchaguzi ni batili, na itathibitisha uamuzi huo kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi.

(2) Baada ya uthibitisho uliofanyika chini ya kifungu kidogo cha (1), uchaguzi utathibitishwa au uchaguzi mdogo utafanyika, kadri itakavyohitajika, kwa mujibu wa uthibitisho.

Taarifa ya Mahakama kuhusu vitendo vya rushwa au vitendo haramu

**143**.-(1) Endapo mahakama inaamua kuwa mtu ana hatia kwa kitendo chochote cha rushwa au kitendo haramu, itathibitisha hivyo kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi na kama mtu anayehusika ameandikishwa kuwa mpiga kura-

(a) Mkurugenzi wa Uchaguzi atafuta jina lake katika Daftari ambalo ameandikishwa; na

(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi atamjulisha kwa maandishi msimamizi wa uchaguzi wa eneo la uchaguzi husika kuhusu kufutwa huko.

(2) Wakati wa kuhitimisha usikilizaji wa shauri la uchaguzi au rufaa, mahakama itathibitisha kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi-

(a) iwapo kitendo chochote cha rushwa au kitendo chochote haramu kimethibitishwa kutendwa na mgombea au kwa uelewa na ridhaa au idhini ya mgombea yeyote katika uchaguzi na aina ya kitendo hicho, kama kipo; na

(b) majina na taarifa nyingine za watu wote, kama zipo, ambao wamethibitishwa kwa kiasi cha kuiridhisha mahakama kuwa wana hatia ya kitendo chochote cha rushwa au kitendo haramu.

(3) Kabla mtu yeyote, ambaye si mhusika katika shauri la uchaguzi wala si mgombea ambaye kwa niaba yake, nafasi inayogombewa katika shauri la uchaguzi, hajathibitishwa na Mahakama chini ya kifungu hiki, Mahakama itampa mtu huyo nafasi ya kusikilizwa na kutoa ushahidi wa kuonesha kwa nini asithibitishwe.

(4) Endapo mahakama inathibitisha kuwa kosa la kitendo cha rushwa au kitendo haramu kimetendwa na mtu yeyote, mtu huyo atawajibishwa kwa kuondolewa

sifa kama vile katika tarehe hiyo ya hati angekuwa ametiwa hatiani kwa kosa la kitendo haramu.

(5) Endapo mahakama imethibitisha kuwa kitendo cha rushwa au kitendo haramu kimefanyika na mtu yeyote kwa uelewa na ridhaa au ruhusa ya mgombea, pamoja na matokeo mengine yoyote, mgombea atawajibishwa kwa kuondolewa sifa kama vile wakati wa tarehe ya hati, angekuwa ametiwa hatiani kwa kosa la kitendo cha rushwa au kitendo haramu.

(6) Mkurugenzi wa Uchaguzi mapema iwezekanavyo-

(a) ataagiza nakala ya uthibitisho iliyotolewa chini ya kifungu hiki kuchapishwa katika Gazeti la Serikali;

(b) atafuta kwenye Daftari jina la mtu yeyote aliyeandikishwa anayeonekana katika kumbukumbu kuondolewa sifa ya kupiga kura katika uchaguzi; na

(c) atamtaarifu kwa maandishi msimamizi wa uchaguzi wa eneo la uchaguzi linalohusika kuhusu kufutwa kwa jina la mtu huyo ambaye ameandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo hilo la uchaguzi.

(7) Mara baada ya kujulishwa, msimamizi wa uchaguzi atachukua hatua zote kama itakavyolazimu kuhakikisha kuwa mtu anayehusika anarejesha kadi ya mpiga kura na nyaraka nyingine zozote zinazohusika kwa ajili ya kufutwa.

Muda wa kuwasilisha na kuamuliwa kwa shauri la uchaguzi na rufaa

**144**.-(1) Kila shauri la uchaguzi litawasilishwa ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi na msimamizi wa uchaguzi.

(2) Mahakama itasikiliza na kuamua shauri la uchaguzi ndani ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuwasilisha shauri.

(3) Upande wa shauri ambao hautaridhika na uamuzi wa Mahakama chini ya kifungu kidogo cha (2) unaweza kukata rufaa ndani ya siku arobaini na tano kutoka tarehe ya uamuzi.

(4) Rufaa iliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu

kidogo cha (3) itasikilizwa na Mahakama ya Rufani.

(5) Mahakama itasikiliza na kuamua rufaa ndani ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuwasilisha rufaa.

(6) Endapo hakuna uwezekano wa kuamuliwa kwa shauri la uchaguzi ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili, Jaji Mkuu na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, anaweza kuongeza muda kwa kipindi kingine kisichozidi miezi sita, kama atakavyoamua.

Kura zinazoweza kuondolewa wakati wa uchunguzi

**145**.-(1) Wakati wa uchunguzi katika kusikiliza shauri la uchaguzi, kura zifuatazo zitaondolewa:

(a) kura ya mtu yeyote tofauti na mgombea au ya mtendaji aliyepiga kura chini ya kifungu cha 14(4) ambaye jina lake halikuwemo katika Daftari la eneo la uchaguzi ambalo amepigia kura;

(b) kura ya mtu yeyote ambaye kura yake ilipatikana kwa hongo, takrima au kushawishiwa;

(c) kura ya mtu yeyote ambaye ametenda kosa au amesababisha kutendeka kwa kosa la kujifanya mtu mwingine katika uchaguzi;

(d) kura ya mtu yeyote aliyethibitishwa kupiga kura zaidi ya mara moja katika uchaguzi huo isipokuwa kura ya kwanza iliyopigwa na mtu huyo kama kura hiyo ya kwanza inaweza kutambuliwa kiasi cha kuiridhisha mahakama;

(e) kura ya mtu yeyote ambaye, kwa sababu ya kutiwa hatiani kwa kosa la kitendo haramu au kwa sababu ya hati ya mahakama au kwa sababu ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukiuka Sheria hii au sheria nyingine yoyote aliondolewa sifa ya kupiga kura katika uchaguzi.

(2) Kura ya mpiga kura aliyeandikishwa haitaondolewa, wakati wa uchunguzi kwa sababu mpiga kura huyo hakuwa na sifa za jina lake kuingizwa katika Daftari isipokuwa kwa sababu zilizoainishwa katika

kifungu kidogo cha (1)(d).

Kanuni za Mahakama

**146**.-(1) Jaji Mkuu kwa kushauriana na Tume anaweza kutunga kanuni za mahakama kusimamia taratibu na desturi za kufuatwa na kuweka ada itakayolipwa kuhusu mashauri ya uchaguzi na maombi chini ya Sura hii.

(2) Kanuni zitakazotungwa chini ya Sura hii zitachapishwa katika Gazeti la Serikali.

## SEHEMU YA TATU
## SHAURI LA UCHAGUZI KUPINGA MATOKEO YA UDIWANI

Kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya mashauri ya uchaguzi

**147**.-(1) Uchaguzi wa mgombea Udiwani hautahojiwa isipokuwa kwa shauri la uchaguzi.

(2) Uchaguzi wa mgombea Udiwani utatangazwa kuwa batili kutokana na mojawapo kati ya sababu zifuatazo ikiwa zitathibitishwa kwa kiwango cha kuiridhisha Mahakama:

(a) kwamba kwa sababu ya vitendo vya rushwa au vitendo haramu vilivyotendwa kuhusiana na uchaguzi, au mazingira mengine ambayo yanafanana na hayo yaliyotajwa au yasiyotajwa, wapiga kura walio wengi walizuiwa au wanaweza kuwa walizuiwa kumchagua mgombea ambaye walimtaka;

(b) kwamba, wakati wa kampeni za uchaguzi, maelezo yaliyotolewa na mgombea, au kwa niaba yake na kwa ufahamu wake na ridhaa au idhini yake, kwa nia ya kutumia hoja za ukabila, rangi au udini au tofauti zinazohusu uchaguzi au kuhusu yeyote kati ya wagombea au iwapo wagombea si wa jinsi moja, kwa nia ya kutumia tofauti hizo;

(c) kutozingatia masharti ya Sheria hii kuhusu uchaguzi, iwapo itajitokeza kuwa uchaguzi haukufanyika kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika masharti hayo na kuwa kutozingatia huko kumeathiri matokeo ya

uchaguzi;

(d) kwamba kitendo cha rushwa au kitendo haramu kilitendwa kuhusiana na uchaguzi na mgombea au kwa ufahamu na kwa ridhaa au idhini ya mgombea au kwa ufahamu na ridhaa au idhini ya mmoja wa mawakala wake; au

(e) kwamba mgombea wakati wa kuchaguliwa kwake hakuwa mtu mwenye sifa ya kuchaguliwa kuwa Diwani.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2), pale ambapo wakati wa usikilizaji wa shauri la uchaguzi kuhusu uchaguzi chini ya Sheria hii, mahakama inabaini kuwa kitendo cha rushwa au kitendo haramu kuhusu uchaguzi kimetendwa na au kwa ufahamu na ridhaa au idhini ya wakala yeyote wa mgombea, na mahakama ikabaini zaidi baada ya kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nafasi ya kusikilizwa, kwamba mgombea ameithibitishia mahakama-

(a) kwamba hakuna kitendo cha rushwa au kitendo haramu kilichotendwa na mgombea mwenyewe au kwa ufahamu na ridhaa au idhini ya mgombea au wakala wake;

(b) kwamba mgombea alichukua hatua zote zinazostahili kuzuia kufanyika kwa vitendo vya rushwa au vitendo haramu katika uchaguzi huo; na

(c) kwamba kwa namna nyingine yoyote uchaguzi haukuwa na kitendo chochote haramu kwa upande wa mgombea na wakala wake,

ikiwa mahakama itaamua hivyo, kuchaguliwa kwa mgombea huyo hakutakuwa batili kwa sababu ya kitendo chochote kile.

Kusamehewa kwa kutenda au kutokutenda matendo fulani

**148**. Endapo mahakama itaona ama kwa ombi au kwa shauri la uchaguzi-

(a) kwamba kitendo chochote au kutotenda kwa mgombea katika uchaguzi wowote au wakala wake au mtu mwingine yeyote ambacho isipokuwa kwa kifungu hiki kingekuwa ni kitendo cha rushwa au kitendo haramu,

kimetendeka au kilifanyika kwa nia njema kwa kughafilika au kukosea kwa bahati mbaya au kwa sababu nyingine yoyote inayofanana na hizo; na

(b) kwamba kwa sababu ya mazingira itakuwa vema kwa mgombea huyo au wakala wake au mtu mwingine yeyote, au yeyote kati yao, asihusishwe na athari zozote chini ya Sheria hii kwa kutenda au kutotenda,

mahakama inaweza kutoa amri kuruhusu kitendo au kutotenda jambo hilo kutofungwa na masharti ya Sheria hii ambapo vinginevyo kungefanya kutenda au kutotenda kuwa ni kitendo cha rushwa au kitendo haramu, na mgombea, wakala au mtu mwingine yeyote hatahusishwa na athari yoyote chini ya Sheria hii kwa kutenda au kutotenda.

Mashauri yanayosikilizwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi

**149**.-(1) Kila shauri la uchaguzi wa udiwani na maombi chini ya Sehemu hii yatasikilizwa na mahakama ya Hakimu Mkazi, ambayo itajulikana kama “mahakama”.

(2) Upande wa shauri ambao hautaridhika na uamuzi wa mahakama ya Hakimu Mkazi chini ya kifungu kidogo cha (2) unaweza kukata rufaa ndani ya siku arobaini na tano kutoka tarehe ya uamuzi.

(3) Rufaa zote chini ya Sehemu hii zitasikilizwa na Mahakama Kuu.

Mashauri na kuweka dhamana ya gharama

**150**.-(1) Shauri la uchaguzi linaweza kuwasilishwa na mmoja au zaidi ya watu wafuatao:

(a) mtu aliyepiga kura kihalali au alikuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi ambao shauri linahusika;

(b) mtu anayedai kuwa alikuwa na haki ya kuteuliwa au kuchaguliwa katika uchaguzi;

(c) mtu ambaye anadai kuwa alikuwa mgombea katika uchaguzi huo; au

(d) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(2) Msajili wa mahakama hatapanga tarehe ya kusikilizwa shauri isipokuwa kama mlalamikaji amelipa

mahakamani dhamana ya gharama, kiasi kisichozidi shilingi laki tano kwa kila mlalamikiwa.

(3) Mlalamikaji atatakiwa ndani ya siku kumi na nne baada ya kuwasilisha shauri, kufanya maombi kwa ajili uamuzi wa kiasi kitakacholipwa kama dhamana ya gharama na mahakama itaamua maombi hayo ndani ya siku kumi na nne zinazofuata baada ya tarehe ya kuwasilisha maombi yake kwa ajili ya uamuzi wa kiasi kinachopaswa kulipwa kama dhamana ya gharama.

(4) Endapo mtu ameunganishwa kama mlalamikiwa kwa mujibu wa amri ya mahakama, mlalamikaji ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ambayo amri ilitolewa ikielekeza mtu huyo kuunganishwa kuwa mlalamikiwa, atalipa mahakamani kiasi kingine kisichozidi shilingi laki mbili, kama itakavyoelekezwa na mahakama kuhusiana na mtu huyo.

(5) Endapo kwa maombi yatakayofanywa na mlalamikaji, mahakama imeridhika kuwa utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) au (4) utasababisha ugumu kwa mlalamikaji, inaweza kuelekeza kwamba-

(a) mlalamikaji atoe aina nyingine ya dhamana ambayo thamani yake haizidi shilingi laki tano, kama ambavyo mahakama itaona inafaa;

(b) mlalamikaji asamehewe kulipa malipo ya aina yoyote ya dhamana.

(6) Amri haitatolewa chini ya kifungu kidogo cha (3), (4) na (5) mpaka nafasi imetolewa kwa mlalamikiwa, au endapo kuna walalamikiwa wawili au zaidi, kwa kila mlalamikiwa kujieleza kwa madhumuni hayo.

(7) Ikiwa dhamana ya gharama haitalipwa mahakamani ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya uamuzi wa mahakama kuhusu kiasi cha malipo ya dhamana ya gharama, mwenendo wa shauri la uchaguzi hautaendelea kusikilizwa na shauri hilo litafutwa.

(8) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) hayatatumika kwa namna yoyote ile ikiwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mlalamikaji au ni mmoja wa walalamikaji.

(9) Kiasi cha fedha kilichowekwa kama dhamana ya gharama au salio la dhamana hiyo kitarejeshwa kwa mlalamikaji mapema iwezekanavyo, endapo mlalamikaji atashinda katika shauri au rufaa na iwapo hakuna amri

iliyotolewa dhidi ya mlalamikaji kulipa gharama.

Nafuu zinazoweza kuombwa

**151**. Nafuu zote au yoyote kati ya zifuatazo ambazo mlalamikaji anaweza kustahili, zinaweza kuombwa katika shauri la uchaguzi:

(a) tamko kwamba uchaguzi ni batili;
(b) tamko kwamba uteuzi wa mtu aliyechaguliwa haukuwa halali;
(c) endapo kiti kinadaiwa na mgombea ambaye hakushinda kwa madai kwamba alikuwa amepata kura nyingi zaidi halali, kufanyika uchunguzi wa kura.

Uthibitisho wa mahakama juu ya uhalali wa uchaguzi

**152**. Wakati wa kuhitimisha usikilizaji wa shauri la uchaguzi, mahakama itaamua iwapo mjumbe ambaye uteuzi au uchaguzi wake unalalamikiwa au mtu mwingine yeyote au mtu aliteuliwa au alichaguliwa ipasavyo, au uchaguzi ni batili, na itathibitisha uamuzi huo kwa Tume na baada ya uthibitisho kutolewa uamuzi utakuwa ni wa mwisho, na uchaguzi utathibitishwa au uchaguzi utafanyika upya kama itakavyohitajika kwa mujibu wa uthibitisho huo.

Muda wa kuwasilisha na kuamuliwa kwa shauri la uchaguzi

**153**.-(1) Kila shauri la uchaguzi litawasilishwa ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi na msimamizi wa uchaguzi:

Isipokuwa kwamba, shauri la uchaguzi linalohoji uchaguzi kwa msingi wa kitendo cha rushwa na hasa tuhuma ya malipo ya fedha au kitendo kingine kuwa kimefanywa au kilitendwa tangu tarehe ya kutangazwa kwa matokeo na msimamizi wa uchaguzi au kwa ufahamu na ridhaa au idhini ya mjumbe ambaye uchaguzi wake unalalamikiwa au kwa ufahamu na ridhaa au idhini ya wakala wa mjumbe kwa kutekeleza au kuendeleza kitendo hicho cha rushwa malalamiko hayo yanaweza kuwasilishwa wakati wowote ndani ya siku ishirini na nane baada ya tarehe ya malipo au kitendo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni zozote za Mahakama zilizotungwa chini ya kifungu cha 155, shauri la uchaguzi lililowasilishwa kwa muda unaostahili linaweza, kwa madhumuni ya kuhoji uchaguzi kuhusu

tuhuma za kitendo cha rushwa au kitendo haramu, kurekebishwa kwa ruhusa ya mahakama ndani ya muda ambao shauri linalohoji matokeo ya uchaguzi kwa kigezo hicho linaweza kuwasilishwa.

(3) Mahakama itasikiliza na kuamua kila shauri la uchaguzi ndani ya miezi kumi na mbili tangu tarehe ya kuwasilishwa kwa shauri la uchaguzi.

(4) Endapo hakuna uwezekano wa kuamuliwa kwa shauri la uchaguzi ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili, Jaji Mkuu na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, anaweza kuongeza muda kwa kipindi kingine kisichozidi miezi sita, kadri atakavyoamua.

Kura zinazoweza kuondolewa wakati wa uchunguzi

**154**.-(1) Wakati wa uchunguzi katika kusikiliza shauri la uchaguzi, kura zifuatazo zitaondolewa:

(a) kura ya mtu yeyote ambaye jina lake halikuwepo kwenye Daftari la kata alikopigia kura;

(b) kura ya mtu yeyote ambaye kura yake ilipatikana kwa hongo, takrima au kushawishiwa;

(c) kura ya mtu yeyote ambaye ametenda kosa au amewezesha kutenda kosa la kujifanya mtu mwingine katika uchaguzi;

(d) kura ya mtu yeyote ambaye amethibitika kuwa amepiga kura zaidi ya mara moja katika uchaguzi;

(e) kura ya mtu yeyote ambaye kwa sababu ya kutiwa hatiani kwa kosa la kitendo cha rushwa au kitendo haramu au kwa sababu ya taarifa ya Mahakama, au kwa sababu ya kutiwa hatiani kwa kosa lolote kinyume cha Sheria hii au Sheria nyingine yoyote iliyomwondolea sifa ya kupiga kura katika uchaguzi.

(2) Kura ya mpiga kura aliyeandikishwa haitaondolewa wakati wa uchunguzi kwa sababu mpiga kura hakuwa na sifa au hana sifa ya jina lake kuingizwa katika Daftari isipokuwa kwa sababu zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1)(e).

Kanuni za Mahakama

**155**. Jaji Mkuu kwa kushauriana na Tume anaweza kutunga kanuni za Mahakama kusimamia taratibu na mwenendo wa kuzingatiwa na kuweka ada itakayolipwa kuhusiana na mashauri ya uchaguzi na maombi chini ya Sehemu hii.

## SURA YA TISA
## MASHARTI YA JUMLA

Maelezo yasiyo sahihi

**156**. Kasoro ya jina au maelezo yasiyo sahihi ya mtu yeyote au sehemu iliyotajwa au kuelezwa katika Daftari, taarifa au nyaraka nyingine, iliyoandaliwa au kutolewa chini au kwa madhumuni ya Sheria hii, haitaathiri kwa namna yoyote matumizi ya Sheria hii kuhusu mtu huyo au sehemu hiyo, kama mtu huyo au sehemu hiyo inaelezwa hivyo katika Daftari, taarifa au nyaraka kama itakavyotambuliwa.

Mamlaka ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na wasimamizi wa uchaguzi kutaka taarifa

**157**.-(1) Katika kutekeleza majukumu yao chini ya Sheria hii, Mkurugenzi wa Uchaguzi na wasimamizi wa uchaguzi au mtu mwingine yeyote anayehusika na uendeshaji wa upigaji kura au uandikishaji wa wapiga kura, wakati wote, watakuwa na uwezo wa kutaka taarifa kutoka kwa mtu yeyote muhimu ili kuhakikisha kama mtu ana sifa ya kuwa mgombea na kumtambua mtu yeyote au mahali anapoishi mtu yeyote, na kuhakikisha iwapo mtu yeyote amepoteza sifa za kupiga kura au kuwa mgombea.

(2) Mtu ambaye, baada ya kutakiwa kisheria kutoa taarifa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1), anashindwa kutoa taarifa hizo ambazo anazifahamu au anazimiliki au bila sababu za msingi anachelewa kutoa taarifa hizo, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki mbili.

Malipo ya watendaji

**158**. Mtu yeyote aliyeajiriwa kwa madhumuni ya Sheria hii, ikiwa hajaajiriwa katika utumishi wa umma, atapokea malipo yanayostahili kwa kazi hiyo kadri Tume itakavyoona inafaa kuidhinisha.

Gharama kulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

**159**. Gharama zote zitakazotumika-

(a) katika kuandaa Daftari, kutoa kadi ya mpiga kura na kufanya mambo mengine au vitu vingine vinavyohitajika kufanywa kwa madhumuni ya kutekeleza masharti ya Sheria hii;

(b) na Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi, wasimamizi wa uchaguzi na mtu mwingine yeyote aliyeajiriwa kutekeleza majukumu ya uchaguzi;

(c) kwa malipo ya maafisa walioainishwa katika kifungu cha 159; na

(d) kwa afisa yeyote wa umma kuhusu shughuli rasmi zinazohusiana au zinazotokana na uchaguzi,

zitatozwa na kulipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Utoaji wa taarifa

**160**. Taarifa chini ya Sheria hii itachukuliwa kuwa imefikishwa au kutolewa kwa mtu yeyote-

(a) ikiwa imefikishwa kwake binafsi;

(b) iwapo imeachwa kwa ajili yake kwenye anwani yake ya mwisho inayofahamika; au

(c) iwapo imetumwa kwake kwa njia ya posta katika anwani yake ya mwisho inayofahamika.

Kanuni

**161**.-(1) Tume inaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii na bila kuathiri ujumla wa yaliyotangulia, inaweza kutengeneza kanuni zinazoainisha-

(a) kitu chochote ambacho chini ya masharti ya Sheria hii kinaweza kuainishwa; na

(b) muundo wa nyaraka na matamko kwa madhumuni ya Sheria hii.

(2) Endapo fomu zozote zimeandaliwa chini ya kifungu hiki, fomu hizo zitatumika kwa madhumuni ambayo zinahusika au kwa namna ambayo zinaweza kutumika au kuweza kurekebishwa na zinaweza kutafsiriwa na kutumika katika lugha yoyote kama Tume itakavyoelekeza.

Kanuni za Maadili ya Uchaguzi

**162**.-(1) Kwa madhumuni ya kusimamia uchaguzi wa haki, huru na amani, na baada ya kushauriana na vyama vyote vya siasa na Serikali, Tume itaandaa na kuchapisha katika Gazeti la Serikali Kanuni za Maadili ya Uchaguzi zitakazoainisha maadili ya vyama vya siasa, Serikali na Tume wakati wa kampeni za uchaguzi na uchaguzi na utaratibu wa utekelezaji wake.

(2) Kanuni za Maadili ya Uchaguzi zitasainiwa na-

(a) kila chama cha siasa;
(b) kila mgombea kabla hajawasilisha fomu ya uteuzi;
(c) Serikali; na
(d) Tume,

na zitapaswa kuzingatiwa na wahusika wote waliosaini.

(3) Mtu ambaye atakiuka masharti ya Kanuni za Maadili ya Uchaguzi atawajibika kwa adhabu ambayo itaelezwa katika Kanuni hizo.

Msamaha wa ushuru wa stempu

**163**. Hati yoyote itakayotolewa kwa kiapo au uthibitisho kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii katika fomu itakayoainishwa itasamehewa kodi ya ushuru wa stempu chini ya sheria yoyote inayotumika kuhusu ushuru wa stempu.

Maelekezo

**164**. Tume inaweza, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kutoa maelekezo ya jumla au mahususi kuhusu majukumu ya wasimamizi wa uchaguzi, wasimamizi wa vituo na watu wengine walioajiriwa au kwa madhumuni mengine yoyote ya Sheria hii:

Isipokuwa kwamba, maelekezo hayo hayatakinzana na masharti yoyote ya Sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Kubadilishwa Daftari n. k

**165**. Endapo, kwa maoni ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, itakuwa ni lazima kubadilisha Daftari kwa sababu yoyote ile, itakuwa ni halali kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kuelekeza Daftari hilo kubadilishwa na daftari jipya.

Matumizi ya teknolojia

**166**. Tume inaweza kutumia teknolojia katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

## SURA YA KUMI
## KUFUTA KWA SHERIA NA MASHARTI YA MWENDELEZO

Kufutwa kwa Sheria Na. 1 ya 1985 na 4 ya 1979

**167**. Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 zinafutwa.

Masharti ya mwendelezo

**168**. Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979-

(a) vitendo vyote na shughuli zote zilizotekelezwa na Tume chini ya Sheria hizo zitaendelea kuwa halali hadi pale zitakapobatilishwa chini ya Sheria hii;

(b) fomu zote zilizoidhinishwa na Tume kwa madhumuni ya Sheria hizo zitachukuliwa kuwa fomu zilizoidhinishwa chini ya Sheria hii; na

(c) sheria ndogo zote zilizotengenezwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 ambazo bado zinatumika, zitachukuliwa kuwa zimetengenezwa chini ya Sheria hii hadi pale zitakapofutwa na Sheria hii au sheria ndogo zitakazotengenezwa chini ya Sheria hii.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka, 2023. Kwa ujumla, Sheria inayopendekezwa kutungwa inakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Hatua hii inatokana na ukweli kwamba masharti ya Sheria hizo yanafanana, tofauti kubwa pekee ikiwa kwamba moja inaweka masharti kuhusu uchaguzi wa Rais na Wabunge na nyingine inaweka masharti kuhusu uchaguzi wa Madiwani. Hivyo basi, kutungwa kwa Sheria inayopendekezwa ambayo itaunganisha masharti yote katika Sheria moja kutarahisisha usimamizi na utekelezaji wa masharti hayo ikizingatiwa kuwa Sheria hizo mbili hutekelezwa na mamlaka moja ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Muswada huu umegawanyika katika Sura Kumi.

Sura ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Sheria inayopendekezwa, mawanda ya matumizi, utaratibu wa kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa. Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, Sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, na itatumika Tanzania kwa uchaguzi wa Madiwani. Sura hii inajumuisha pia masharti kuhusu ugawaji wa maeneo ya uchaguzi na uteuzi wa watendaji mbalimbali wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambao husaidia kufanikisha shughuli mbalimbali za Tume kama vile uandikishaji wa wapiga kura, usimamizi wa uchaguzi na uratibu wa taarifa, upatikanaji wa vifaa, rasilimali na masuala mengine muhimu kwa ajili ya kuendesha uchaguzi.

Sura ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu uandikishaji wa wapiga kura. Sura hii imegawanyika katika Sehemu Nne ambapo Sehemu ya Kwanza inaainisha sifa za mtu kuandikishwa au kukosa sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, sehemu ya kupigia kura na masharti kuhusu Daftari la Awali na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Miongoni mwa sifa muhimu za kuandikishwa kuwa mpiga kura zilizoainishwa katika

Sehemu hii ni kuwa raia wa Tanzania na kutimiza umri wa miaka kumi na nane. Sehemu ya Pili inaweka masharti ya uandikishaji ambayo yanajumuisha muda wa uandikishaji, wakala wa uandikishaji, kadi ya mpiga kura, utaratibu baada ya mtu kubadili makazi, namna ya kupata kadi mpya endapo kadi ya awali imepotea, imefutika au imeharibika na utaratibu wa uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura ambao unapendekezwa ufanyike mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na uchaguzi mkuu unaofuata. Sehemu ya Tatu ya Sura hii inaainisha masharti kuhusu utaratibu wa kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa au dhidi ya jina la mtu kuendelea kubaki katika Daftari. Kwa mujibu wa Sehemu hii, pingamizi dhidi ya uandikishwaji litawasilishwa kwa afisa mwandikishaji. Sehemu ya Nne inajumuisha masharti kuhusu rufaa dhidi ya pingamizi la kuongezwa au kufutwa katika daftari ambapo kwa mujibu wa Sehemu hii, rufaa dhidi ya uamuzi wa afisa mwandikishaji zitawasilishwa katika Mahakama ya Wilaya.

Sura ya Tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu uchaguzi wa Rais na imegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inajumuisha masharti ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, idadi ya wadhamini wanaopaswa kuwa nao na utaratibu wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za uteuzi. Sehemu hii pia inaweka utaratibu wa namna ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea wa kiti cha Urais na Makamu wa Rais. Sehemu ya Pili ya Sura hii inaweka masharti mbalimbali yanayohusiana na taratibu za uchaguzi wa Urais ikijumuisha siku ya uchaguzi wa Rais, watu wanaostahili kupiga kura katika uchaguzi wa Rais, sifa za mgombea katika uchaguzi wa Rais, majumuisho ya kura katika uchaguzi wa Rais, mazingira yanayoweza kusababisha upigaji kura kurudiwa na masharti ya kutambulika kwa uchaguzi wa Rais kuwa uchaguzi wa Makamu wa Rais. Ili kuepuka kurudia masharti kuhusu taratibu za upigaji kura ambazo hufanana kwa uchaguzi wa mgombea wa kiti cha urais, ubunge na udiwani, Sehemu hii inaweka sharti la matumizi ya Sura ya Sita ambayo inaainisha utaratibu wa upigaji kura.

Sura ya Nne ya Muswada inaweka masharti yanayosimamia uchaguzi wa Wabunge na imegawanyika katika Sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu sifa za wagombea katika uchaguzi wa Ubunge. Sehemu ya Pili inahusu uteuzi wa wagombea Ubunge ambapo inaainisha siku ya uteuzi, uteuzi wa wagombea, utaratibu wa namna ya kuweka dhamana kwa mgombea wa nafasi ya ubunge, masharti ya mgombea kuteuliwa kwa jimbo moja tu, pingamizi na uamuzi juu ya uhalali wa fomu ya uteuzi na

inaainisha pia utaratibu wa kufuatwa endapo kuna mgombea mmoja tu halali wa nafasi ya ubunge au endapo hakuna mgombea. Kwa mujibu wa Sehemu hii endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya Ubunge ameteuliwa, mgombea huyo atapaswa kupigiwa kura na atatangazwa kuwa amechaguliwa endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa.

Sura ya Tano ya Muswada inahusu masharti ya uchaguzi wa Madiwani. Sura hii imegawanyika katika Sehemu Tatu, ambapo Sehemu ya Kwanza inabainisha masharti ya uendeshaji wa uchaguzi wa madiwani, muda wa kuwa madarakani kwa Madiwani, namna na wakati wa kuitisha uchaguzi mdogo na uwakilishi katika Kata. Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu sifa za mgombea na mazingira ya mtu kukosa sifa ya kuteuliwa katika uchaguzi. Sehemu ya Tatu inajumuisha masharti kuhusu siku ya uteuzi, uteuzi wa mgombea, dhamana za wagombea, utaratibu wa kuweka pingamizi na utaratibu unaopaswa kufuatwa ikiwa kuna mgombea mmoja tu wa nafasi ya udiwani au ikiwa hakuna mgombea.

Sura ya Sita ya Muswada inaweka masharti kuhusu uchaguzi, utaratibu wa kupiga kura na uteuzi wa wabunge na madiwani wanawake viti maalum. Sura hii imegawanyika katika Sehemu Sita, ambapo Sehemu ya Kwanza inaweka masharti mbalimbali kuhusu siku ya uchaguzi na tangazo la uchaguzi. Kwa mujibu wa masharti hayo, taarifa ambazo zitakuwa katika tangazo la uchaguzi ni pamoja na siku na muda wa kuanza na kufunga upigaji kura, anwani ya vituo vya kupigia kura, wapiga kura waliopangwa kwa kila kituo cha kupigia kura na taarifa za wagombea walioteuliwa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi. Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu mgombea kujitoa na utaratibu unaopaswa kufuatwa endapo mgombea atafariki au hakuna mgombea. Sehemu ya Tatu inaweka masharti kuhusu kampeni za uchaguzi na namna kampeni zinavyopaswa kuendeshwa, ikiwa ni pamoja na masharti kuhusu kuwasilisha ratiba ya mikutano kwa msimamizi wa uchaguzi kwa lengo la kuepuka migongano ya mikutano. Sehemu hii inaweka pia masharti kuhusu upatikanaji na wajibu wa vyombo vya habari vya umma na matakwa ya kutokuwa na upendeleo na kuepuka ubaguzi kwa mgombea yeyote katika utoaji wa matangazo.

Sehemu ya Nne ya Sura hii inaainisha utaratibu wa uchaguzi unaojumuisha masharti kuhusu siku na muda wa kupiga kura, mawakala wa upigaji kura, masanduku ya kura, muundo wa karatasi za kura na

katazo la kuweka wazi kura. Sehemu ya Tano inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kupiga na kuhesabu kura. Masharti hayo yanajumuisha watu wanaostahili kupiga kura, mazingira yanayoweza kumfanya mtu kupoteza sifa za kupiga kura, utaratibu wa kupiga kura, watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura, mazingira yanayoweza kusababisha kuahirishwa kwa upigaji kura inapotokea vurugu, kufungwa kwa zoezi la upigaji kura na utaratibu wa kuhesabu kura. Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, mawakala wa upigaji kura wanatambuliwa kuwa mawakala wa kuhesabu kura. Vilevile Sehemu hii inaainisha wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura, utaratibu wa kujumuisha kura katika uchaguzi wa wabunge na madiwani na utaratibu wa kutangaza matokeo ya ubunge na udiwani. Sehemu ya Sita ya Sura hii inaweka masharti kuhusu uteuzi wa wabunge na madiwani wanawake viti maalum na unatambua utaratibu ulioainishwa katika Katiba na Sheria za Serikali za Mitaa kuhusu wabunge na madiwani wanawake viti maalum.

Sura ya Saba ya Muswada inaweka masharti kuhusu makosa mbalimbali yanayoweza kutendwa wakati wa uandikishaji, uteuzi wa wagombea na uchaguzi. Miongoni mwa makosa hayo ni pamoja na kutumia wadhifa kushawishi watu wengine kutoomba kuteuliwa, mwenendo usiofaa wa watendaji wa uchaguzi na maafisa waandikishaji, makosa yanayohusu fomu za uteuzi au karatasi za kura, vitendo vya ushawishi na rushwa, kutotunza siri katika uchaguzi kwa watu wanaoruhusiwa kuwa katika kituo cha kupigia kura au kuhesabia kura na kuingilia mikutano halali ya hadhara. Sambamba na kuainisha makosa mbalimbali, Sehemu hii inaweka pia adhabu kwa mtu atakayetenda makosa hayo.

Sura ya Nane ya Muswada inaweka masharti kuhusu kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya shauri la uchaguzi. Kwa mujibu wa Sura hii, mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya ubunge yatasikilizwa katika Mahakama Kuu na mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya udiwani yatasikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi. Miongoni mwa taratibu zilizoainishwa katika Sura hii ambazo mtu aliyefungua shauri atapaswa kuzingatia ni utaratibu wa kuweka dhamana ya gharama. Aidha Sehemu hii inaweka pia masharti ya mamlaka ya Jaji Mkuu kutengeneza kanuni zitakazosimamia usikilizwaji wa mashauri ya kupinga matokeo ya uchaguzi. Ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa kanuni hizo, inapendeekzwa kuwa kanuni hizo zitengenezwe kwa kushauriana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Sura ya Tisa ya Muswada inahusu masharti ya jumla ambayo yanajumuisha mamlaka ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi kupata taarifa, malipo ya watendaji wa uchaguzi, mamlaka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria na matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Tume.

Sura ya Kumi ya Muswada inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1979 na kuweka utaratibu kwa masharti yatakayoendelea kutumika hata baada ya kufutwa kwa Sheria hizo.

Dodoma,
17 Oktoba, 2023

KASSIM MAJALIWA MAJALIWA,
*Waziri Mkuu*